**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Kamal Basha Pandu | Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo. |
| 2.Mhe. Ali Mzee Ali | Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais. |
| 3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe. |
| 4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge. |
| 5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni. |
| 6.Mhe. Haji Omar Kheri | Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu. |
| 7.Mhe. Soud Yussuf Mgeni | Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Wawi. |
| 8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani. |
| 9.Mhe. Hamza Hassan Juma | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura. |
| 10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais. |

| | |
|---|---|
| 11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang’ombe. |
| 12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki | MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais. |
| 13. Mhe. Machano Othman Said | Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni. |
| 14.Mhe. Samia Suluhu Hassan | MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake. |
| 15.Mhe. Burhan Saadat Haji | MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni. |
| 16.Mhe. Asha Abdalla Juma | MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais. |
| 17.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi. |
| 18.Mhe. Sultan Moh’d Mugheiry | MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais. |
| 19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki. |
| 20.Mhe. Zainab Omar Moh’d | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake. |
| 21.Mhe. Idi Pandu Hassan | Mwanasheria Mkuu wa Serikali. |
| 22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae. |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Mzee Ali Ussi | Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani. |
| 24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari | Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu. |
| 25.Mhe. Khamis Jabir Makame | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni. |
| 26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan | Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole. |
| 27.Mhe. Tafana Kassim Mzee | Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini. |
| 28.Mhe. Omar Ali Shehe | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Chake-Chake. |
| 29.Mhe. Zakiya Omar Juma | "Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake. |
| 30.Mhe. Abass Juma Muhunzi | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Chambani. |
| 31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga. |
| 32.Mhe. Haji Faki Shaali | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Jimbo la Mkanyageni. |
| 33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake. |
| 34.Mhe. Hamad Masoud Hamad | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole. |

| | |
|---|---|
| 35.Mhe. Said Ali Mbarouk | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Gando. |
| 36.Mhe. Rashid Seif Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani. |
| 37.Mhe. Mohamed Ali Salim | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani. |
| 38.Mhe. Asaa Othman Hamad | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete. |
| 39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake. |
| 40.Mhe. Najma Khalfan Juma | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake. |
| 41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile. |
| 42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja. |
| 43.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini. |
| 44.Mhe. Ali Denge Makame | Jimbo la Amani. |
| 45.Mhe. Ali Haji Ali | Jimbo la Mkwajuni. |
| 46.Mhe. Ali Moh’d Bakari | Jimbo la Tumbe. |
| 47.Mhe. Ali Suleiman Ali | Jimbo la Kwahani. |
| 48.Mhe. Ame Mati Wadi | Jimbo la Matemwe. |

| | |
|---|---|
| 49.Mhe. Ame Ussi Juma | Jimbo la Nungwi. |
| 50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake. |
| 51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila | Jimbo la Fuoni. |
| 52.Mhe. Ashura Abeid Faraji | Nafasi za Wanawake. |
| 53.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Nafasi za Wanawake. |
| 54.Mhe. Dadi Faki Dadi | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba. |
| 55.Mhe. Fatma Abdalla Tamim | Nafasi za Wanawake. |
| 56.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | Jimbo la Mji Mkongwe. |
| 57.Mhe. Haji Mkema Haji | Jimbo la Koani. |
| 58.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji | Uteuzi wa Rais. |
| 59.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani. |
| 60.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba. |
| 61.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope. |
| 62.Mhe. Mkongwe Nassor Juma | Nafasi za Wanawake. |
| 63.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga | Jimbo la Chwaka. |
| 64.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja. |
| 65.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake. |
| 66.Mhe. Omar Ali Jadi | Jimbo la Kojani. |
| 67.Mhe. Pembe Juma Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja. |

| | |
|---|---|
| 68.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu | Jimbo la Muyuni. |
| 69.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake. |
| 70.Mhe. Said Khelef Ali | Jimbo la Bumbwini. |
| 71.Mhe. Salim Abdulla Hamad | Jimbo la Mtambwe. |
| 72.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni. |
| 73.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni. |
| 74.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde. |
| 75.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Nafasi za Wanawake. |
| 76.Mhe. Zahra Ali Hamad | Nafasi za Wanawake. |

**Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**.

**Kikao cha Tano – Tarehe 27 Januari, 2009**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 38**

**Ruhusa ya SMZ Kukopa katika Soko la Ndani**

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu -** Aliuliza:-

Miongoni mwa kero za Muungano zilizoshughulikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), ni SMZ kuruhusiwa kukopa kutoka soko la ndani ya nchi wakati hapo awali ilikuwa hairuhusiwi kukopa.

(a) Nini sababu za msingi zilizoisababisha SMZ isiruhusiwe kukopa katika soko hilo la ndani hapo awali.

(b) Kwa kuwa sasa SMZ imeruhusiwa kukopa katika soko hilo la ndani, ni mara ngapi imewahi kukopa au kukopeshwa katika soko hilo na ni kiasi gani serikali imekopa/imekopeshwa – bidhaa au fedha.

(c) Kabla ya SMZ kuruhusiwa kukopa katika soko hilo hapo awali, ilikuwa inafaidika vipi katika soko hilo wakati suala la mikopo katika soko la ndani ni suala la Muungano linalojulikana tangu zamani.

(d) Nini masharti ya mkopo huo hasa ukizingatia kuwa kila mkopo au chombo kinachotoa mikopo kina masharti yake.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 38 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kutoa ufafanuzi wa swali hili lenye vipengele vinne kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa ikipata mikopo kutoka katika Seriikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kabla ya kuanzishwa kwa soko la ndani, na imekuwa ikitumia soko la ndani tokea lilipoanzishwa Mikopo ya Hati Fungate *(Treasury Bills)* na Hati Fungate za Muda Maalum *(Treasury Bonds)* huchukuliwa na Serikali ya Mapinduzi pale ambapo pengo la nakisi linapojitokeza, au kutofikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato na ikasababisha kuwepo pengo la nakisi au kutopata kima cha msaada wa kibajeti *(General Budget Support)* kwa wakati.

(a) Kwa maelezo niliyoyatoa hapo awali inaonesha wazi kwamba SMZ haijawahi kuzuiliwa kukopa katika soko la ndani kabla na baada ya kuanzishwa kwake.

(b) Mhe. Spika, kwa ufupi kabisa naomba kutoa baadhi ya takwimu za mikopo ya SMZ kuanzia mwaka 2004/2005 hadi 2007/2008 kama ifuatavyo:-

**Takwimu za Mikopo ya Hati Fungate (TZA Bilioni)**

| **Mwaka:** | **Hati Fungate *(Treasury Bills):*** | **Hati Fungate za Muda Maalum *(Treasury Bonds):*** |
|---|---|---|
| 2004/05 | 4.33 billion | 4.40 billion |
| 2005/06 | 6.37 billion | 5.07 billion |
| 2006/07 | 0.00 billion | 0.00 billion |
| 2007/08 | 5.51 billion | 6.00 billion |

(c) Mhe. Spika, kama nilivyokwisha eleza katika maelezo yangu na jawabu yangu ya swali (a) kwamba SMZ ilikuwa inakopa SMT kabla ya kuanzishwa soko la ndani na inaendelea kukopa baada ya kuanzishwa soko hilo.

(d) Mhe. Spika, hakuna masharti inayopewa SMZ katika kukopa na kukopeshwa zaidi ya kuwepo na riba (*interest*) iliyo sawa na chombo chohote kinachohitaji kukopa, isipokuwa serikali yenyewe imejiwekea utaratibu mzuri ambao inautumia kuhakikisha inakuwa na uwezo wa kulipa deni/madeni yanayokopwa kupitia soko hilo.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Ahsante Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Wakati alipokuwa akijibu swali (b) alituletea takwimu za mikopo ambayo imekuwa ikikopwa kuanzia mwaka 2004/2005. Kasema ilikuwa inakopwa SMT. Je, ni chombo gani cha SMT ambacho

kilikuwa kinaikopesha SMZ, ni Benki Kuu au mabenki mengine. Hivi sasa katika mkopo ambao ulikuwa umekopwa ni kiasi gani kimelipwa na kiasi gani kimebakia.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, kama kawaida Tanzania tuna chombo ambacho serikali zote mbili huwa zinakopa pale zinapohitaji, yaani chombo chenyewe ni *BoT*. Sio Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tu peke yake ambayo inayokopa. Lakini tulipokuwa tunasema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inakopa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tulikusudia chombo ambacho tulichokiweka kwa ajili ya kutoa hiyo mikopo ni chombo cha *BoT*.

Swali la kiasi gani kilichokopwa ndio kama hivi nilivyokitaja. Lakini swali la kiasi kilicholipwa Mhe. Spika, kwa sababu sikujitayarisha na takwimu sahihi basi naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwa maandishi.

**Nam. 42**

**Kazi za Baraza la Mji**

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu -** Aliuliza:-

Miongoni mwa kazi za Baraza la Mji ni kuweka mji katika hali ya usafi na kutengeneza barabara ndogo ndogo. Katika mji wa Chake Chake kuna barabara ambazo ziko katika hali mbaya na hazipitiki vizuri – barabara ya Kichungwani hadi Miembeni na Mharitani Msingini hadi Tume ya Uchaguzi.

(a) Kwa nini imepita muda mrefu bila ya barabara hizo kufanyiwa matengenezo.

(b) Ni lini zitafanyiwa matengenezo.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ -**Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza napenda kukubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa miongoni mwa kazi za Baraza la Mji ni kuweka mji katika hali ya usafi na kuzifanyia matengenezo barabara ndogo ndogo.

(a) Umepita muda mrefu bila ya barabara za Kichungwani hadi Miembeni na Mharitani Msingini hadi Tume ya Uchaguzi bila ya kufanyiwa

matengenezo kutokana na ukosefu wa fedha. Kwa jinsi barabara hizo zilivyochakaa zinahitaji kujengwa upya badala ya kufanyiwa matengenezo. Ili kuzijenga upya barabara hizo, kwa makisio ya mwaka 2008 jumla ya Tshs. 380,000,000/- zinahitajika ambazo Baraza la Mji Chake Chake halina uwezo wa kufanya hivyo. Hata hivyo, Serikali kupitia Baraza la Mji Chake Chake imeanza kufanya mazungumzo na baadhi ya Washirika wa Maendeleo ikiwemo *ADB* ili kufikiria uwezekano wa kuzisaidia.

(b) Barabara hizo zitafanyiwa matengenezo fedha zitakapopatikana kutoka Baraza la Mji lenyewe, Serikali au Washirika wa Maendeleo.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa barabara kuu itokayo njia ya *Airport* hadi kufikia Machomane imetengenezwa katika kufikia kilele cha sherehe za Mapinduzi. Je, Mhe. Waziri haoni sababu kuu ya kutokutengenezwa njia hizi ni kwamba hazipitiwi na wakubwa wakati wa sherehe.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nisaidie jibu la swali la nyongeza la Mhe. Rashid Seif Suleiman. Mhe. Spika, lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kujenga barabara kwa manufaa ya wananchi si kwa ajili ya kupita viongozi peke yao. Kama Mhe. Mwakilishi ana kumbukumbu sahihi barabara hii anayoisema ilianza kufanyiwa matengenezo kabla ya uamuzi wa serikali kupeleka sherehe Pemba. Kwa hivyo, sherehe zimeikuta barabara inafanyiwa matengenezo kwa ajili ya wananchi wa Pemba, Zanzibar na wageni wote. Si lengo kwamba barabara zetu tuzitengeneze kwa ajili ya viongozi, isipokuwa ni lengo kwa wote.

Bahati nzuri jana nilikuwa nazungumza na Afisa Mdhamini akanambia kwamba sasa barabara iko Machomane, lengo letu Chake Chake yote tuirembe ile mpaka Wawi, Ziwani kote tufike huko usiwe na wasi wasi.

**Mhe. Haji Mkema Haji:** Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Waheshimiwa Mawaziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Barabara hizi mbili zilizotajwa ziko hali mbaya. Lakini jawabu la Mhe. Waziri anasema lazima pesa hizi zipatikane kwenye Washirika wa Maendeleo na Baraza la Mji lenyewe. Mhe. Spika, kwa sababu Baraza la Mji ni taasisi ya serikali na inaposhindwa kupatiwa ruzuku kutekeleza majukumu yake. Je, Mhe. Waziri haoni iko haja ya kutia kwenye mpango ikaingizwa kwenye bajeti ili serikali yenyewe ibebe mzigo huu.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Spika, kama nilivyosema hapo awali kwamba uwezo wa Baraza la Mji Chake Chake ni mdogo kwa kuweza kutekeleza barabara hizi nilizozitaja. Serikali imekuwa ikitengeneza barabara kila sehemu ambayo barabara iko katika hali mbaya sana. Kwa hivyo, sawa sawa na barabara hizi zitachukuliwa kama zilivyotengenezwa barabara nyengine au zinazoendelea kutengenezwa barabara za aina hii kati ya Unguja na Pemba.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa jibu lake mama Mhe. Waziri alisema kwamba serikali haijawa na pesa ya kutengeneza barabara hizo ambazo thamani yake ni shilingi milioni 300. Je, Mhe. Waziri atawaambia nini wananchi ili waelewe kwamba serikali haina pesa ya kutengenezea barabara hizo.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikifanya mambo na huwa inajitangaza au nyengine huwa haijitangazi lakini yanaonekana nini kinafanyika. Kwa hivyo, kusema kwa barabara hizi tu kwamba serikali ilisema itatengeneza, hilo suala ambalo limo katika utawala mzima wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ilani ya Chama chake inayoitoa kwa kuzikarabati barabara zote bila ya kujali hii inatoka Mharitani Msingini au inatoka *Airport* kuelekea Machomane.

**Nam. 73**

**Matengenezo ya Barabara ya Fuoni/ Kombeni**

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu (Kny: Mhe. Anaclet Thobias Makungila) –** Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwaletea maendeleo wananchi wake imeamua kujenga barabara ili kuimarisha biashara, kilimo, uvuvi, uwekezaji n.k.  Na kwa kuwa mradi wa ujenzi wa barabara ya Fuoni/Kombeni uliokuwa upate ufadhali wa *MCC* umefutwa.

Je, serikali ina mpango gani wa angalau kuichonga barabara hiyo ya Fuoni/Kombeni kwa kutumia pesa za mfuko wa barabara ambao kodi yake inatokana na wale wenye vyombo vya moto wanaotumia barabara hiyo, ambao miongoni mwa wachangiaji hao ni wananchi waishio Jimbo la Fuoni.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi –** Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 73 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali hili kwanza naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Barabara ya Fuoni ni miongoni mwa barabara 16 ambazo zilikuwa zijengwe kwa mradi wa ufadhili wa MCC Unguja na Pemba. Lakini hata hivyo, baada ya majadiliano mbali mbali barabara ambazo zimekubaliwa kujengwa ni barabara 5 tu nazo zote ni za Kaskazini Pemba. Naomba nizitaje barabara ambazo zinakusudiwa kujengwa.

Kwanza ni barabara ya Mzambarauni Takao/Pandani/Finya ambayo ina urefu wa kilomita 7. Barabara ya Mzambarauni Karimu/Mapofu ambayo ina kilomita 8.5, barabara ya Bahanasa/Daya/Makombeni/Mtambwe kilomita 13.5, barabara ya Chwale/Kojani kilomita 3, barabara ya Pangani/Kangani kilomita 3. Zote zinafanya kilomita 35 za barabara ambazo zitajengwa kwa ufadhili wa MCC.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba nijibu swali kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuzijenga barabara zote za Zanzibar ili kuimarisha uchumi kupitia biashara, kilimo, uvuvi, uwekezaji na kadhalika. Dhamira hiyo hiyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliomba ufadhili wa *MCC* kwa barabara ya Fuoni hadi Kombeni. Hata hivyo, ombi hilo la kutaka msaada wa *MCC* kuwa barabara zote za Unguja halikufanikiwa. Badala yake mradi huo wa *MCC* utatekelezwa kwa barabara za Mkoa wa Kaskazini Pemba tu.

Hata hivyo, serikali inaendelea kutafuta washirika wengine wa maendeleo kwa ajili ya kuzijenga na kuzifanyia matengenezo barabara zote zilizokuwemo katika mpango wa *MCC*. Aidha, serikali itachukua hatua za kuzifanyia matengenezo ya dharura barabara zote ambazo zitakuwa hazipitiki katika kipindi hiki cha mpito.

Aidha, kwa kuwa juhudi hizo zitachukua muda mrefu kutokana na taratibu mbali mbali ambazo ziko nje ya uwezo wa wizara yangu, serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi itaingiza barabara hizo katika mpango maalum wa matengenezo ya barabara ambazo zitapatiwa fedha kutoka katika Mfuko wa Barabara.

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Je, Mhe. Waziri ni sababu zipi zinazojulikana na serikali za kwa nini MCC haikutaka kujenga barabara hata moja Unguja.
Swali (b) alizitaja barabara 5, lakini hii ya 5 yenye kilomita 3 ama imekosewa jina au sikusikia vizuri naomba aitaje tena.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, kwanza naomba niseme kwamba barabara ni sehemu ya maendeleo. Maana leo nimesikia kuna watu wanasema barabara si maendeleo. Lakini jibu sahihi barabara ya 5 aliyosema Naibu Waziri ni Kipangani/Kangagani.

Kuhusu kwa nini MCC hawakuchukua barabara za Unguja, nafikiri hili lilitokana na uwezo wao wa fedha hazikuwa nyingi za kutosheleza Unguja na Pemba. Kutokana na hali hiyo, Mkoa wa Kaskazini Pemba hata huko Pemba hizi barabara zote 5 ziko katika Mkoa wa Kaskazini Pemba, ulikuwa uko katika hali mbaya zaidi kuliko mikoa ya Kusini Pemba na Mikoa ya Unguja. Kwa hivyo, MCC wakaamua kwamba waanze Kaskazini Pemba.

Lakini kutokana na hali kwamba SMZ inathamini utendaji na uzuri wa barabara zetu, tumeomba kuna barabara ya Ole/Kengeja yenye urefu wa kilomita 35 tayari OPEC wameshakubali kutusaidia ujenzi wake fedha zipo katika taratibu za kutangaza tenda kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii. Itatoka Ole mpaka Kengeja kwa kupitia Pujini, Vitongoji na sehemu nyengine.

Barabara za Unguja tunaendelea kuziombea tumeshazungumza na World Bank, BADEA na OPEC wenyewe kwa Zanzibar. Kwa hivyo, tunatarajia labda baadae na Zanzibar nako tutafanikiwa. Ziko barabara nyingi kwa Unguja hazipungui 10. Kuna barabara ya Matemwe/Muyuni, Kichwele/Pangeni/Kizimbani, Kiboje/Koani/Jumbi, Njia Nne/Umbuji, Uroa, Fuoni/Kombeni, Jendele/Cheju, Jozani/Ukongoroni na Mkwajuni/Kijini.

Mhe. Spika, barabara hizi zote ziko katika mpango wa serikali. Lakini tunazo barabara 3 za ziada kutoka ring road pale na kuelekea huko Kombeni, pia zina mpango mwengine wa kuombewa fedha serikali. Kwa hivyo, lengo letu tukimaliza barabara kuu hizi tuingie katika barabara nyengine ndogo ndogo na hatutozisahau za Mjini Unguja zikiwemo za Chumbuni na Kwamtipura na sehemu nyengine za mjini Unguja.

**Mhe. Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi nipate kutoa ufafanuzi wa ziada kumalizia pale Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi alipomalizia. Namshukuru Mhe. Machano Othman Said kwa maelezo yake mazuri sana na ya busara. Lakini napenda kutoa maelezo yafuatayo kumjibu Mhe. Hamad Masoud Hamad.

Wakati wa majadiliano ya awali kati ya serikali na watendaji wanaosimamia huu Mfuko wa Changamoto za Milenia (MCC), ilibainika kwamba hazikuwepo fedha za kutosha kwa ajili ya miradi yote ya barabara Unguja na Pemba. Kwa hiyo, wakati wa mjadala huo na serikali hii inaongozwa na wanadam na moja ya sifa ya mwanadam aliye makini ni kusikiliza.

Waheshimiwa Wajumbe mtakubaliana nami kwamba kila bajeti hapa, Waheshimiwa Wajumbe hasa wajumbe kutoka chama cha upinzani wamekuwa wakilalamika hapa serikali jamani haipendi haki, barabara zinajengwa Unguja, Pemba hivi. Sasa moja ya madhumuni ya Baraza lako tukufu hili kuielekeza na kuishauri serikali. Serikali iliyo makini inapokuwa na uwezo ikiambiwa jambo lenye mantiki inasikiliza. Kwa maana hiyo basi, sisi kama serikali hatukuwa na sababu ya kutokusikiliza ushauri huo unaotolewa. Kwa maana hiyo, wakati wa mjadala huu tukalizingatia hilo ili kukidhi mahitaji yote ya wananchi wetu.

Kwa hiyo, tukasema "tukate pua tuunge wajihi". Kwa maana hiyo, wajumbe wamekuwa wakisema barabara za Unguja zinajengwa. Sasa ikawa ni nafasi nzuri na barabara hizo za upande wa pili ambazo zimekuwa zikilalamikiwa, basi serikali ikaona ni jambo jema na la busara nayo kuzingatiwa kwa uzito huo niliousema.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana.

**Mhe. Spika:** Baada ya *gear* zote hizo tena tuendelee na maswali mengine.

**Nam. 34**

**Usajili wa Vyombo vya Moto**

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu -** Aliuliza:-

Pamoja na makusanyo mazuri ya shilingi milioni mia moja na moja (101,000,000/=) yaliyokusanywa na Bodi ya Mapato Zanzibar *(ZRB)* kwa kipindi kifupi toka kuanza upya zoezi la usajili wa magari na vyombo vyengine vya moto, bado kuna malalamiko na madai kwamba kima cha pesa kinacholipwa kwa kazi hiyo (shs. 62,000/=) kwa vepsa, honda, ciao na pikipiki na shs. 150,000/= kwa magari ni kikubwa mno na hakistahili.

(a) Je, ni kwa misingi gani na kwa sababu zipi zilizoifanya serikali kuweka viwango hivyo vikubwa.

(b) Kwa sababu za kudhibiti mapato wizara yako imeanzisha zoezi hilo ili kupata na kuwa na uhakika wa mapato yanayoingia serikalini. Je, ni

vyombo vingapi vinavyotegemewa kusajiliwa kwa kipindi hiki kutoka vilivyosajiliwa.

(c) Serikali inategemea kupata kiasi gani kwa usajili huo utakapokamilika kutokana na idadi gani ya vyombo vinavyotarajiwa kusajiliwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake, naomba kutoa ufafanuzi ufuatao kuhusiana na viwango mbali mbali vya malipo katika suala zima la usajili wa vyombo vya moto.

Mhe. Spika, gharama za malipo ya usajili wa vyombo vya moto unahusisha vipengele vifuatavyo:-

1. Usajili wa Chombo
2. Malipo ya Sahani za Nambari *(Plate Number)*
3. *Sticker* (Kwa ajili ya Udhibiti wa Nambari)
4. Leseni ya Njia

Ufafanuzi wa gharama za usajili wa vyombo mbali mbali vya moto ni kama ifuatavyo:-

| **S.No:** | **Aina ya Chombo:** | **Bei ya Usajili:** | **Bei ya Sahani za Nambari:** | ***Sticker*:** | **Jumla:** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ciao | 10,000.00 | 27,750.00 | 7,500.00 | **45,250.00** |
| 2. | Vespa | 25,000.00 | 21,375.00 | 7,500.00 | **53,875.00** |
| 3. | Pikipiki | 25,000.00 | 27,750.00 | 7,500.00 | **60,250.00** |
| 4. | Gari Ndogo zisizozidi tani tatu na nusu | 50,000.00 | 35,850.00 | 7,500.00 | **93,350.00** |
| 5. | Gari kubwa zenye uzito wa kuanzia tani tatu na nusu | 65,000.00 | 35,850.00 | 7,500.00 | **108,350.00** |

(a) Mhe. Spika, kwa ujumla gharama za usajili wa vyombo vya moto kama nilivyozitaja hapo juu sio kubwa, bali gharama zimeongezeka

kutokana na kuingizwa kwa malipo ya sahani za nambari za *sticker* ya udhibiti wa nambari hizo kwa pamoja kulingana na hapo awali ambapo baadhi ya malipo yalikuwa yanafanywa tofauti na malipo ya usajili mpya. Kwa mfano, hapo awali uchoraji wa nambari ulifanywa mbali na kulikuwa hakuna *sticker* inayotumika kwa ajili ya kudhibiti nambari husika.

Aidha usajili wa vyombo vya moto pia unahusisha malipo ya leseni ya njia, ambayo katika mfumo mpya wa usajili malipo yake yanategemea uzito wa chombo husika.

Bei za leseni ya njia kwa mujibu wa chombo ni kama ifuatavyo:-

| **S.No:** | **Aina ya Chombo:** | **Leseni ya Njia:** |
|---|---|---|
| 1. | Ciao | **6,000.00** |
| 2. | Vespa | **12,000.00** |
| 3. | Pikipiki | **15,000.00** |
| 4. | Gari ndogo zisizozidi tani tatu na nusu | **20,000.00**<br>**70,000.00** |
| 5. | Gari kubwa zenye uzito wa kuanzia tani tatu na nusu na kuendelea | **95,000.00**<br>**200,000.00** |

Mhe. Spika, naomba kutanabahisha kwamba gharama za usajili wa vyombo vya moto, zitakuwa ni mara moja tu kwa kuanzia, na hapo baadae malipo yatakayokuwa yanalipwa ni malipo ya leseni za njia, isipokuwa kwa vyombo vitakavyokuwa vinaingia nchini kwa mara ya kwanza, yaani (*New Vehicle Importation).*

b) Kwa hivi sasa Mhe. Spika, ni vigumu wizara yangu kujua idadi ya vyombo vya moto vinavyoweza kusajiliwa, kutokana na kwamba usajili wa vyombo vya moto vinahusisha pia magari mapya yanayoingia nchini kila siku. Uingizaji wa magari mapya pia unategemea mwenendo mzima wa biashara ya magari hapa Zanzibar. Hadi kufikia mwisho wa mwezi wa Disemba mwaka jana jumla ya vyombo 5,003 vimesajiliwa na zoezi bado linaendelea.

c) Mhe. Spika, kuhusu kiwango cha mapato ambacho serikali inaweza kupata kwa mujibu wa makadirio ya mwaka huu ni Sh. 249,963,000/- kutokana na usajili wa vyombo vya moto, na Sh. 235,000,000/-

kutokana na leseni za barabara. Nachukua fursa hii kumjulisha Mhe. Mwakilishi kwamba zoezi hili halitarajiwi kukamilika kwa sasa, na litakuwa likiendelea kadiri ya vyombo vya moto vitakavyoingia hapa nchini. Mhe. Spika, ahsante.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri katika jibu lake ametueleza kwamba ada hizi zinazotolewa huwa zinatolewa katika mchanganuo mbali mbali ikiwepo usajili. Kwa kuwa vyombo vile vilivyokuwa vikitumika zamani, vimesajiliwa kwa mujibu wa sheria za usajili na kwa kuwa usajili ule ulikuwa ni wa halali, na kwa kuwa sasa hivi vyombo vile ambavyo vilifika zamani inaonekana vina sajiliwa upya.

a) Je, Mhe. Waziri huoni kwamba kuvisajili vyombo vile mara mbili ni kutowatendea vyema wamiliki wa vyombo vile?
b) Ni utaratibu upi mwengine ambao utatumika ili kuona kwamba vyombo vinavyosajiliwa upya ni vile ambavyo ndio kwanza vinaingia nchini, ahsante.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) (MBLM) anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, naomba nitofautiane na Mhe. Salmin kwamba serikali haiwatendei haki wenye vyombo kwa kusajiliwa upya. Nasema hili ni zoezi maalum serikali imelichukua makusudi,

a) Kujaribu kuweka mapato katika njia inayofaa, hiyo ni sababu moja.
b) Ni lazima na sisi twende na wakati.

Usajili uliokuwepo wa kuandika nambari pembeni pembeni ule tena umepitwa na wakati Mhe. Salmin na sisi twende kimataifa. Sasa unakuja gari zote na vibao vya nambari zikiwa zimekubalika kimataifa. Kesho nitakuja kulijibu swali kama hili nafikiri (b) yake. Wenzetu Bara hata vile visahani tu, basi vinathibitishwa na *Tanzania Bureau of Standard*, twende na sisi kimataifa. Sasa bado turudi tena kule kule tuandike kwa mkono, nambari imepinda ya (a) au (z).

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tukubali tu, ndio serikali imeona tuweke utaratibu mpya wa nambari zote. Hawa ambao tayari wameshasajiliwa, basi wanabadili tu. Kwa hivyo, yale magamba yao ya zamani wanakwenda wanabadili tu, na hizi *rate* utaona kwa kweli zimekuwa *reversed*, kama nilivyosema na serikali nayo kwa sababu vyombo vimekuwa vingi, basi na sisi tunufaike kidogo kwa kujaribu kutengeneza hizi barabara. Barabara zote zinataka tuzitunze.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii, nitakuwa na swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Spika, baadhi ya wananchi wanadai kwamba zoezi la kuchora sahani mpya za nambari hizi amepewa mtu binafsi badala ya ZRB wenyewe.

a) Je, suala hilo ni kweli, na kama ni kweli basi serikali kwa hali hiyo itakuwa imezingatia *three quotation* na kwamba mikataba hiyo ipo?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) (MBLM) anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, kweli suala hili ni nambari 35 kwa kesho, labda pengine waliouliza wangeyachanganya pamoja, lakini kwa sababu limeulizwa, basi naomba nijibu moja kwa moja.

Mhe. Spika, ukweli kwamba kazi ile serikali ilipoitoa tumetangaza tenda kwa mujibu wa sheria zetu za manunuzi ya serikali, yaani *procurement act* ya mwaka 2005. Katika tenda hiyo jumla ya kampuni tatu zilitenda. Kampuni zenyewe ni *Masasi Sons Company* ya *Dar es Salaam*, *Buda Auto Parts* ya *Zanzibar* na *Link Way Zanzibar Limited*.

Kampuni hizo tatu zilinunua *tender document* na Kampuni mbili zilirudisha tenda hizo, na Kampuni moja haikurejesha. Baada ya kufanyiwa tathmini ya tenda hizi mbili kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa Kampuni inayotengeneza nambari hivi sasa ndio iliyoshinda.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza maswali ya nyongeza yafuatayo.

Mhe. Spika, suala hili lililokuja azma yake kuu ni kwamba kuna mambo mawili tofauti. Kwanza kuna watu walioingiza magari yao huko nyuma ambayo yameshasajiliwa na wamelipa. Pia kuna magari mapya yameingia, hiyo ni sehemu ya pili.

a) Mhe. Spika, pamoja na majibu yake ambayo kayajibu, lakini wananchi wengi hawajayafahamu pamoja na mimi, kuwa haya magari ya zamani yaliyokwishasajiliwa watu hawa wanafikiriwa vipi kwenda kusajili tena ili kupunguziwa adhabu ya bei kubwa ambayo ipo.

b) Kuna tofauti ya usajili na kuandika namba, kwenye kuandika namba hakuna tatizo. Mhe. Waziri anatoa ufafanuzi gani ili wananchi waridhike na masuala haya.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) (MBLM) anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, naamini na yeye amekubaliana na mimi kama nilivyosema awali kwamba usajili huu tunaouzungumza umegawika sehemu nne.

1) Usajili wa chombo chenyewe.
2) Malipo ya sahani za nambari.
3) Stika kwa ajili ya udhibiti wa nambari.na
4) Leseni ya njia.

Sasa ndio nikasema haya mambo matatu yanafanywa kwa mkupuo, yaani tukishafanya sasa hivi, basi ni mara moja tu. Sasa kwa nini tunafanya tena. Sababu zilizofanya tufanye tena, ni kwamba tumegundua kuna magari mengi hayana usajili, nambari zimeandikwa ovyo ovyo tu. Ukiwafuatilia *traffic* wanayajua mengi kuhusu haya magari. Mimi labda si *traffic* siyajui, lakini ukweli kuna magari mengi hayana usajili, wanachukua kisahani cha nambari wanabandika namba yoyote wala hakuna hasa utaratibu wanaoufuata.

Mhe. Spika, tunakubaliana, wakikaa *traffic* na wakikusudia kuifanya hii kazi kweli, basi watayakamata mengi. Sasa ndio tukasema tulipitie hili zoezi zima na tulifumuwe, ili tuanze upya, kwa hivyo tunaanza upya kwa magari yote. Nina amini yote yakienda kwa mfumo huu, basi sifikiri kama litapatikana gari tena litakalokwepa kwa njia hii. Kwa hivyo, naomba sana mheshimiwa tushirikiane kwa hili zoezi la serikali ambalo tumekusudia tulifanye.

Nakumbuka tulilileta suala hili kwenye *Bajeti Speech* yetu karibu miaka miwili au mitatu iliyopita, lakini tulichelewa kuanza. Katika bajeti kuu yetu ya serikali tulileta na waheshimiwa mlitupa ridhaa yenu.

**Nam. 89**

**Marekebisho Baada ya Kukosekana kwa Umeme Zanzibar**

Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa

**Nam. 29**

**Utaratibu wa Kupeleka Wagonjwa nje ya Nchi**

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu** - Aliuliza:-

Kwa kuwa utaratibu wa kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi kwa matibabu unalalamikiwa sana na wagonjwa wenyewe na familia zao na wananchi kwa

jumla kuwa ni mbaya, hauridhishi na ni hatari hasa kutokana na urasimu, usumbufu na dhana ya upendeleo Wizarani na kwa miongoni mwa magonjwa.

(a) Mhe. Waziri kwa kujisafisha na dhana hiyo tueleze utaratibu wa kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi kwa matibabu ukoje.

(b) Ni kwa maradhi au magonjwa ya aina gani yanapewa kipaumbele kwa mgonjwa kupelekwa matibabu nje ya nchi.

(c) Je kwa maradhi ya kawaida mgonjwa hupaswa kusubiri kwa muda gani mpaka apate ruhusa ya kupelekwa nje kwa matibabu, iwapo mgonjwa wa maradhi kama ya Figo, Moyo na mengine hatari huchukua zaidi ya miezi sita.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 29 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, utaratibu wa kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi kwa matibabu ni kama ufuatao:-

i. Mgonjwa hupendekezwa na daktari wake kutibiwa nje ya nchi baada ya kuonekana kuwa matibabu yake hayapatikani nchini na mgonjwa atafaidika na tiba ya nje.

ii. Mgonjwa hupelekwa kwenye bodi ya Matibabu (*Medical Board*) ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na ikithibitika kuwa kweli anahitaji matibabu nje ya nchi bodi hushauri hivyo.

iii. Ripoti za mgonjwa huyo zote hupelekwa hospitali husika kwa ushauri na makisio ya gharama za matibabu yake.

iv. Baadae taarifa hizo zikipatikana tena Wizara yangu ya Afya na Ustawi wa Jamii, huomba idhini ya matumizi ya fedha hizo Wizara ya Fedha na Uchumi.

v. Fedha hizo zikipatikana mgonjwa husafirishwa kwa matibabu.

(b) Mhe. Spika, magonjwa yote ambayo matibabu yake yameshindikana nchini yanapewa kipaumbele hasa magonjwa ya moyo, figo, mishipa ya fahamu, viungo n.k.

(c) Mhe. Spika, hakuna muda maalum wa kusubiri, utaratibu ulioelezwa kifungu cha (1) ukikamilika mgonjwa huyo tena husafirishwa nje.

**Mhe. Ali Abdalla Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, tumefahamu utaratibu wote wa mgonjwa ambao unachukuliwa na wizara yake hadi akafika kwenda kwenye matibabu ya nje. Lakini katika jibu lake hapa amesema kwamba pamoja na taratibu zote za daktari, kuna kuwa na bodi ambayo inapitia taarifa hizo na kutoa ruhusa ya kupelekwa huko nje.

Je, kwa kuwa maradhi mengine hayataki yachukue muda mwingi, hii bodi hukaa kwa vipindi vingapi kwa mwezi, ili kuweza kuchagua hao wagonjwa wa kwenda nje.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, bodi hukutana mara mbili kwa mwezi, lakini inapotokea dharura au wagonjwa wakawa wengi, basi hufanya kikao cha dharura mara moja.

**Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej:** Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali la ziada, naomba kuuliza kama ifuatavyo. Je, ni utaratibu upi unaofuatwa kwa kupelekwa wagonjwa ambao ni viongozi wa serikali, au viongozi wa kisiasa yaani Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa matibabu nje ya nchi?

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, utaratibu ni huu huu, isipokuwa tu ikiwa Baraza la Wawakilishi litatuletea barua, basi Baraza hili itabidi barua yake na maelezo ya mheshimiwa yule madaktari wetu bingwa waliokuwepo Makao Makuu, Mkurugenzi Mkuu na Katibu Mkuu, watapitia na kuhakikisha kwamba kweli ombi hili linahitaji mheshimiwa huyu apelekwe nchi za nje, basi atapelekwa. Lakini kama ikionekana matibabu haya yanapatikana nchini, basi hakuna umuhimu huo wa kufanya hivyo.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Nakushukuru Mhe. Spika, kwanza nilikuwa naona unaangalia kule, kumbe unaniita mimi, nikashangaa kidogo. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Spika, swali langu ni dogo na ni kama ifuatavyo. Kwa kuwa mara nyingi wananchi wanaposikia kwenye vyombo vya habari kwamba viongozi wanakwenda kuangaliwa afya zao nje na sio kutibiwa, basi wanakuwa na maneno mengi wananchi.

a) Je, hao viongozi wanaokwenda kuangaliwa afya zao nje, ambapo wananchi husema wanakwenda kuangaliwa pele. Ni maradhi gani haswa yanayopaswa viongozi kwenda kuangaliwa nje ya nchi, sio kutibiwa na kuangaliwa hapa.
b) Ni viongozi wa aina gani wenye stahili hii ya kwenda kuangaliwa afya zao nje badala ya hapa nchini.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, utaratibu huo wote anaouzungumza, wizara yangu haipitii jambo hilo, wala haijawahi kupokea jambo hilo. Wizara yangu inapokea, kama mheshimiwa anataka kupelekwa kwenye matibabu nje ya nchi, basi ndio hufanywa utaratibu nilioueleza. Lakini mambo ya kuangalia afya zao huko, wizara yangu haihusiki na jambo hilo, wala sijawahi kuliona jambo hilo Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Mnajua Waheshimiwa Wajumbe mtu akiwa na uhakika wa jambo, basi anakuwa na nguvu kweli kweli.

**Nam. 54**

**Mafanikio ya Mradi wa *PADEP***

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu: (Kny: Anaclet Thobias Makungila)** – Aliuliza:-

Madhumuni ya mradi shirikishi wa maendeleo ya kilimo na uwezeshaji (*PADEP*) ni kukuza maendeleo ya kilimo kwa kuweka kipaumbele kwenye utumiaji wa teknolojia zinazofaa, kwa walengwa na kuiwezesha sekta binafsi kushiriki katika kuboresha soko la pembejeo za kilimo na mazao yanayotokana na kilimo.

(a) Je, mradi huo umefanikiwa kiasi gani hapa Zanzibar.

(b) Ni vigezo gani vinavyotumika kupima mafanikio ya mradi huu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira** – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 54 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa *PADEP* umeweza kuzifikia shehia 96 kwa sasa. Wananchi kuibua miradi ya Jamii na vikundi. Hii ni sawa na asilimia 102% ya lengo. Lengo ilikuwa ni shehia 94, jumla ya

miradi ya jamii iliyofikiwa ni 107 na miradi ya vikundi iliyofikiwa ni 467. Mafanikio mazuri yameonekana katika miradi ya uzalishaji wa mazao ya mifugo, miongoni mwa miradi hiyo ni:-

- Mradi wa uzalishaji ndizi ambao umeongeza tija kutoka wastani wa 4.7 kwa hekta hadi 10.3 kwa hekta.
- Mradi wa muhogo umeingiza tija kutoka tani 3.3. kwa hekta hadi tani 6 kwa hekta.
- Mradi wa mpunga katika maeneo yanayolimwa mpunga wa umwagiliaji, tija imeongezeka kutoka tani 2.7 kwa hekta hadi 4.9 kwa hekta.
- Mradi wa uzalishaji wa mayai ya kuku wa kienyeji walioboreshwa kutoka mayai 9 hadi mayai 30 kwa mtago mmoja kwa kuku walioboreshwa.
- Mradi wa Ng'ombe na Mbuzi wa maziwa: uzalishaji wa maziwa umefikia lita 22 kwa ng'ombe kwa siku na lita 2 kwa Mbuzi kwa siku.
- Wanajamii kumilikishwa ng'ombe wa maziwa 758 na mbuzi wa maziwa 1,374.
- Mradi wa duka la pembejeo za kilimo na mifugo ni kupatikana kwa pembejeo kuwa karibu na wanajamii na kusaidia ongezeko la uzalishaji.
- Mradi wa upandaji wa miti umeboresha uhifadhi wa mazingira hasa zile shehia zilizoathirika na uharibifu wa mazingira.

Mafanikio mengine ni teknolojia zinazotolewa na *PADEP* zimesambaa kwa wakulima walio nje ya mradi na kuwapatia mafanikio. Vile vile wanajamii wameweza kusimamia vyema matumizi ya fedha zao pamoja na kupanga na kuendesha miradi yao wenyewe.

- Fedha zilizotumika ni 3,444.84 milioni ni sawa na asilimia 99.9 ya lengo kwa kugharimia miradi ya jamii na vikundi.

Mhe. Spika, fedha hizi wala si mikopo ya kurejesha wakulima.

(b) Vigezo vinavyotumika ni ufuatiliaji wa mara kwa mara na kutumia uchambuzi yakinifu (*Gross Margin Analysis*) juu ya kuongezeka kwa uzalishaji kabla na baada ya kuwepo mradi wa *PADEP*.

**Mhe. Haji Mkema Haji:** Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Miongoni mwa miradi *PADEP* ni mifugo na mifugo ni wanyama viumbe wanaishi. Lakini tatizo lililonitokezea kwenye miradi hii ya ufugaji ni kuwa na madaktari haba na madawa hali.

Mhe. Waziri, juu ya tatizo hili kwa wananchi waliopata miradi ya ufugaji chini ya *PADEP*. Je, Mhe. Waziri ana mpango gani wa kuhakikisha tunapata madaktari wa kutosha ambao watakuwa wanawapitia wale wafugaji kwa ajili ya kuokoa maisha ya ile mifugo wanayoifuga.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira:** Ahsante Mhe. Spika. Kwa kweli tulikuwa hatujapata tatizo hili kutoka kwa wanajamii kuwa kuna tatizo la madaktari wamekuwa kidogo. Lakini bado tunawaomba kama kawaida yao wanavyofanya, pale mtu anapotokezewa na tatizo, basi aweze kuwafuatilia madaktari wetu na watakuwa tayari kuweza kuwasaidia.

Suala la kuongeza wataalamu. Sasa hivi chuo chetu cha Kizimbani kinasomesha wataalamu wetu na mara itakapomalizika awamu hii ya mwanzo tutaweza kuwagawa sehemu mbali mbali, ili kuweza kuwafikia wakulima wakiwemo na wafugaji wetu kwa wingi zaidi.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza, lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Kabla sijauliza maswali yangu napenda nitowe furaha yangu, kuhusu utaratibu ambao umetumika leo hapa Barazani. Tulivyoingia tulikuta *mike* zote za upande wa kulia zilielekea chini kule na hizi huku za upande wa kushoto zilielekea juu kwa pamoja. Sasa nafikiri ni utaratibu mzuri tuuendeleze.

a) Mhe. Spika, kutokana na majibu mama aliyojibu Mhe. Waziri ni kwamba wamevuka lengo katika kuhudumia huu mradi, lengo lilikuwa ni shehia 94 na wamevuka lengo kwa kufikia shehia 96. Kwa sababu shehia zote katika visiwa vyetu ni zaidi ya 300, nafikiri imetangazwa shehia nyengine mpya, kwa hivyo bila shaka zimeongezeka, kwa hivyo zinazidi 300.

Je, ni sababu zipi zilizopelekea kuweka lengo la shehia 94 tu, kwa sababu walitaka waonekane kuwa wanavuka malengo au vipi?

b) Nilitaka kujua katika shehia hizo 94 ambazo zilipangwa kama lengo Unguja ni ngapi na Pemba ni ngapi. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Kabla sijamuita Mhe. Naibu Waziri, kumbe Waheshimiwa Wajumbe ni wachunguzi kweli kweli, inabidi tukae vizuri humu ndani. Maana mimi nilikuwa sijaona na ndio niko juu huku. *(Vicheko).*

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira:** Ahsante Mhe. Spika, ukweli ni kwamba tulikuwa tuna shehia maalum au tuna Wilaya maalum ambazo tulikuwa tumeziwekea malengo.

a) Mradi wetu huu ulikuwa ni wa miaka mitatu na baada ya kumalizika tutakwenda katika maeneo mengine, ndio maana tumevuka lengo, kwa sababu tulikuwa tuna shehia maalum 94, lakini baadae tukaongeza hizo mbili zikawa ni shehia 96, ndio maana tukasema tumepita ile asilimia ambayo tumeikusudia.

b) Mhe. Mjumbe alitaka kujua ni shehia ngapi kwa Pemba na shehia ngapi kwa Unguja. Kabla sijajibu naomba kutoa maelezo mafupi. Mimi ningewaomba waheshimiwa tukiwa tunauliza suala kama hili mara nyingi watu watakuwa wanatuelewa kama tunagawana, wakati Unguja na Pemba ni kisiwa kimoja.

Nataka niseme hao walioko Pemba ni wenzetu na waliopo Unguja ni wenzetu. Sasa tukiwa tunazungumza lugha kama hiyo wataona kama labda kuna mgawano maalum ndani ya kisiwa hiki. Ukiangalia maeneo ya Daraja Bovu watu wengi wanaoishi ni jamaa zetu na sisi hatugawani katika hali ambayo tunafanya upendeleo maalum. Lakini kwa vile limeulizwa basi bora nilijibu sasa.

Kwa upande wa Pemba ni shehia 29 na Unguja ni shehia 67, lakini hizi za Unguja pia haziwabagui watu. Hata ukiwa Mpemba na wewe unaingia katika shehia hizo, ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Omar Ali Jadi:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipatia nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa sababu mradi huu wa *PADEP* ulikusudiwa kuondoa umasikini katika jamii na Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu alisema katika kugawa shehia Unguja 60 na Pemba 24. kutokana na sehemu ya Wicheweni ina ukame wa mtapia mlo katika umasikini. Je, katika shehia hizo 24 za Pemba Wicheweni ni ngapi zimepelekwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira:** Mhe. Spika, Shehia za Micheweni hazimo kwenye mgao huu. Isipokuwa tunategemea mgawanyo wa pili utakapokuja Wilaya ya Micheweni nayo itaingia. Suala hili tayari tumeshalijibu mara nyingi huko nyuma kwamba moja miongoni mwa sababu zilizotupelekea tuondoe, kwani tulitegemea kupata mradi mwengine mkubwa zaidi kule Micheweni, lakini bahati mbaya haukupatikana.

Hivi sasa kijiji kile cha *Millennium* kinaendelea kutengenezewa miradi mingine mizuri ukiwemo mradi mzima wa umwagiliaji kwa kutumia njia ya ya *drip irrigation*, ambapo tutaweza kupanda migomba kama vile tunavyopanda Kusini Unguja. Mhe. Spika, ahsante sana.

**Nam. 24**

**Wageni Kutofikishwa Safari zao**

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji jana katika Baraza lako hili tukufu aliwajuilisha wananchi wote wa Zanzibar na hasa vijana wetu wanaojitafutia riziki katika sekta ya utalii kuhusu uchukuaji wa abiria wanaotoka kwenye mahoteli mbali mbali kwa ajili ya kuwatembeza sehemu tofauti za nchi yetu. Hiyo ndiyo azma kuu ya Kamisheni ya Utalii kupitia wizara na serikali kwa jumla.

Mimi nimeridhika na majibu hayo mazuri, kwamba wizara hivi sasa imo katika hatua ya mwisho kuhakikisha usumbufu ambao unaojitokeza kwa vijana wetu hautokei tena. Hivyo, kutokana na hali hiyo mimi mwenyewe binafsi ninaliondoa swali langu Nam. 24.

**Nam. 62**

**Utalii wa Daraja la Kwanza**

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu (Kny: Mhe. Anaclet Thobias Makungila) -** Aliuliza:-

Kwa kuwa Kamisheni ya Utalii ni chombo chenye majukumu ya kupanda na kusimamia utekelezaji wa mipango ya utalii Zanzibar, pamoja na kuitangaza Zanzibar kama kituo bora cha utalii nje na ndani ya nchi.

Je, Kamisheni ya Utalii imefanikiwa kwa kiwango gani kuhamasisha na kuendeleza utalii wa daraja la kwanza, ili kusaidia uchumi wa taifa na kuwapatia tija wananchi bila ya kuathiri utamaduni na mazingira ya nchi.
**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji –** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kujibu swali Nam. 62 la Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo.

Ili kuhamasisha na kuendeleza utalii daraja la kwanza, Kamisheni ya Utalii imeliingiza jambo hili katika Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 2004, kwamba serikali hivi sasa imelenga kupata wageni kidogo, lakini watumiaji wakubwa, yaani *low volume high spending tourists*. Ndio maana kuna juhudi za makusudi hivi sasa za kuingia katika masoko tajiri kama vile Marekani, Canada na Mashariki ya mbali.

Vile vile kupitia maonesho na mikutano Kamisheni pamoja na *ZIPA* huwashajihisha wawekezaji wakubwa ambao wangeweza kuwekeza katika hoteli ambazo zitaweza kutoa huduma kwa watalii wa daraja la juu. Matokeo ya juhudi hizo ni kupata hoteli zenye hadhi ya nyota za juu ambazo zinatoa huduma kwa aina hiyo ya watalii. Mfano wa hoteli hizo ni *La Gamma Dellest, Serena Inn, Zanzibar Zamani Kempiski, Fairmonts* na kadhalika.

Mikakati mingine ni kuwa na mahoteli yanayojitangaza pamoja (*hotel chain*) ambazo ni maarufu ulimwenguni na hupokea wageni wa daraja la juu. Mfano wa hoteli hizo ni *Kempiski*, *Serena* na *Plan hotels* ambazo zinajumuisha *La Gemma*, *Neptune* na nyengine. Ahsante.

**Mhe. Ali Abdalla Ali:** Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji naomba nimuulize. Amesema katika jibu mama kwamba watalii wengi tunaowataka ni wale wa daraja la juu. Mwaka jana meli nyingi zilizokuja za watalii huwa zilikuja na watalii wa daraja la juu sana, lakini meli hizi hivi sasa zimepungua.

(a) Tatizo gani linalosababisha meli za kitalii kupungua kuja nchini kwetu.

(b) *Package Tours* pia huwa wanakuja na watalii wa kiwango cha juu, lakini hawa huwa wanalipa huko wanakotoka. Je, ni muda gani unachukua mpaka fedha hizo kufika kwenye Mfuko wetu Mkuu wa Serikali.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Spika, ni kweli kwamba meli za watalii hivi sasa zimepungua na hili ni tatizo la dunia nzima. Hivi sasa watalii wengi wao walikuwa wakipata mikopo, ili kununua tiketi na kujilipia katika safari hizi mikopo ile sasa imesita. Isipokuwa watalii wanakuja na ndio meli zinazokuja ni kidogo, kwa sababu ni wale wanaojilipia wenyewe tu. Kwa maana hiyo meli za kitalii zimepungua.

Hata hivyo, jitihada zinafanywa za kuendelea kuutangaza utalii wa Zanzibar, kwa sababu pale watalii wanapopungua kutokana na hali ya uchumi ndipo unapotakiwa kuongeza jitihada za kujitangaza, ili upate watalii wengi zaidi . Kwa sababu katika kipindi hiki mtalii anaangalia wapi aende, atapata nini na kuna nini.

Mhe. Spika, kuhusu *package* ni kweli kwamba watalii wanaokuja na aina hii hulipa huko wanakotoka. Lakini serikali inapata fedha zake kupitia kodi wanayolipa kupitia *club* zao wanazoingia.

Kwa hivyo, sina jawabu ya kusema kwamba fedha zinazolipwa kule inaingia serikali lini *direct*, kwa sababu haiji *direct*. Isipokuwa inakuja kwa mtindo wa kodi zinazolipwa na *club* au hoteli zao wanazofikia. Ahsante.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, ninaipongeza sana Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji kwa kuitangaza Zanzibar, ili watalii wengi waje nchini kwa ajili ya kuongeza pato. Lakini nilishtushwa sana suala Nam. 24 kuondoshwa baada ya kupata habari kwamba baadhi ya watalii huwa wanawarejesha mahotelini wale wageni wanaotembelea sehemu nyengine. Maana ya utalii ni kutembea na kuona mambo.

(a) Hivyo, hoteli kama hiyo ambayo iliyochukua utaratibu huo wa kuwarejesha watalii wasitembee, haioni kwamba ni ukiritimba.

(b) Kama ukiritimba kabla haujazagaa nchi za nje, wizara yake ina utaratibu gani kulipiga vita mara moja suala hilo.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Spika, kurejeshwa kwa watalii aidha kutoka hotelini wanakuwa wamefika katikati na wanarejeshwa na kama nilivyojibu jana kuna njia mbili. Inawezekana watalii wamepelekwa na *Tours Operator* katika hoteli, lakini wageni wale ni *Tour Operator* ndiye aliyewatoa ambako walikotoka na kuja nchini.

Kinachotokea ni kwamba wanapofika hotelini zile hoteli zinazoendesha *Tour Operation* isivyo halali, wanawachukua na kuwatembeza. Sasa inapobainika hivyo *Tour Operator* huwa wanakimbilia polisi, ili kuzuia msafara ule na wachukue wageni wao wenyewe. Wageni wao hawafahamu taratibu zilizopo ndani, kwa sababu wakeshafika hoteli wanashawishiwa kuna *Tour Operation*

kwamba walipe na kiwango ni hiki na kawaida inakuwa ni kidogo kuliko kile anayotoza *Tour Operatro* aliyewaleta.

Kwa hivyo, kurejeshwa kwa wageni ni kutokana na kufanywa biashara isivyo halali na wala sio kuwasumbua wageni. Kama nilivyosema jana, lengo la Kamisheni na Wizara kwa ujumla ni kurekebisha hali hii na hivi sasa Jumuiya ya Watembezaji Wageni pamoja na Kamisheni wanalifanyia kazi suala hili.

## SHUGHULI ZA SERIKALI

### Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Baharini Zanzibar ya mwaka 2009

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, Zanzibar ni nchi yenye visiwa vyenye historia ndefu ya usafiri wa baharini, ambayo ilikuwa kiungo muhimu na njia maarufu katika ugunduzi wa sehemu mbali mbali za dunia hasa ukanda wa Afrika ya Mashariki.

Vile vile ilikuwa ni sehemu muhimu ya biashara kati ya nchi za Ghuba, Bahari ya Hindi na Kusini mwa Afrika. Umashughuri huo uliipelekea Zanzibar kuwa taifa la bahari lenye umaarufu mkubwa duniani. Zanzibar kama visiwa inategemea sana usafiri wa baharini katika kuendesha shughuli zake za kila siku za kiuchumi pamoja na kijamii.

Hivyo, shughuli za usafiri wa baharini zinahitaji usimamizi madhubuti wa kisheria, ili kuhakikisha kuwa kuna usalama wa vyombo, watu, mali zinazopakiwa kwenye vyombo vya kusafiria pamoja na usalama wa bahari yenyewe.

Mhe. Spika, usafiri wa baharini Zanzibar inasimamiwa na Sheria ya *Maritime Transport Act* ya mwaka 2006. Hata hivyo, hakuna chombo mahsusi kilichopewa majukumu ya kudhibiti shughuli hizo. Isipokuwa kwa sasa kazi hiyo inafanywa na Mrajis wa Meli ambaye anawajibika kwa Katibu Mkuu.

Mhe. Spika, kifungu cha 5 cha Sheria ya *Maritime Transport Act* ya mwaka 2006, kimeelekeza kuundwa kwa taasisi itakayosimamia shughuli za usalama wa baharini katika maeneo ya Zanzibar. Katika utekelezaji wa sheria hiyo wizara imeanza kuchukua hatua za awali za uanzishaji wa Mamlaka wa Kusimamia Shughuli za Usafiri Baharini.

Hatua hizo zinakwenda sambamba na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Zanzibar na Rasimu ya Mpango Mkuu wa Usafiri, ambazo zimeelekeza kuundwa kwa

Taasisi ya Kudhibiti shughuli za usafiri kwa jumla ikiwemo usafari wa baharini Zanzibar.

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Shughuli za Usafiri wa Baharini, kwa upande wa Zanzibar umeshapata baraka za wadau wa shughuli za usafiri wa baharini katika vikao mbali mbali.

Aidha, mswada huu ulijadiliwa na kupitishwa katika vikao vya Kamati ya Makatibu Wakuu, Baraza la Mapinduzi pamoja na Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, sheria hii inapendekeza kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Baharini itakayojulikana *The Zanzibar Maritime Authority Act* ya mwaka 2009 na Mamlaka yenyewe itaitwa *Zanzibar Maritime Authority*.

Msingi mkubwa wa sheria hii unatokana na Sheria ya *Maritime Transport Act* ya mwaka 2006, ambapo jukumu kubwa la mamlaka litakuwa ni kusimamia utekelezaji wa sheria hiyo pamoja na mambo mengine yanayohusiana na biashara ya usafiri wa baharini.

Kwa hivyo, matumizi ya sheria hii yatakwenda sambamba. Ili kuyafahamu vizuri majukumu ya mamlaka inapendekezwa kuzipitisha sheria hizi kwa pamoja. Sheria inayopendekezwa inatoa muundo wa mamlaka, majukumu yake kwa ufupi na aina ya vianzio vya ukusanyaji wa mapato.

Sheria ya *Maritime Transport Act* ya mwaka 2006 inaelezea kwa urefu majukumu ya mamlaka na taratibu za utekelezaji wa majukumu hayo.

Mhe. Spika, madhumuni ya kuwasilishwa mswada wa sheria hii mbele ya Baraza lako tukufu la Wawakilishi ni kupata maoni na mapendekezo ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili. Kuhusu namna bora ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kusimamia Shughuli za Usafiri wa Baharini hapa Zanzibar na hatimaye kuupitisha mswada huu kuwa sheria ya kuanzisha mamlaka hiyo.

Mambo yanayopendekezwa katika mswada huu wa sheria ya *The Zanzibar Maritime Authority Act* ya mwaka 2009 imegawika katika sehemu kuu saba na ina jedwali moja na yaliyomo kwenye muhtasari ni kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza ni mambo ya utangulizi. Mhe. Spika, sehemu hii ina jina la sheria, taratibu za uwekaji wa tarehe ya kuanza kutumika sheria hii pamoja na ufafanuzi wa tafsiri ya maneno mbali mbali yaliyotumika kwenye mswada huo.
Sehemu ya pili ni uanzishaji wa kazi na nguvu za mamlaka. Sehemu hii inahusu uanzishwaji wa mamlaka, itakuwa na uwezo wa kushtaki na

kushtakiwa, kazi za mamlaka zitakuwa ni pamoja na kusimamia Sheria ya *Maritime Transport Act* ya mwaka 2006 kwa ujumla. Pia usajili wa meli, kusimamia shughuli zote za usafiri wa baharini Zanzibar, ukaguzi wa meli za kigeni zinapokuwa Zanzibar pamoja na kusimamia utekelezaji wa mikataba ya kimataifa katika meli zinazosajiliwa Zanzibar.

Aidha, mamlaka itakuwa na jukumu la kusimamia biashara ya usafirishaji habarini na kusimamia usalama wa bandari pamoja na kuishauri serikali juu ya mambo mbali mbali yanayohusu usafiri wa baharini na kadhalika.

Sehemu ya tatu inakuhusu utawala na uendeshaji wa mamlaka. Sehemu hii inaelezea utawala na uendeshaji wa mamlaka, ambapo bodi itasimamia uendeshaji wa mamlaka. Sehemu hii pia inaelezea taratibu za uteuzi wa bodi, taratibu za uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu ambaye ndiye Msimamizi na Mtendaji Mkuu wa kila siku wa Shughuli za Mamlaka pamoja na uteuzi wengine wa maafisi wa mamlaka.

Mambo mengine ni uwezo wa waziri kutoa maelekezo kwa bodi na mamlaka, uwezo wa bodi kutoa maelekezo kwa mamlaka na uwezo wa Mkurugenzi Mkuu kuamua mambo mbali mbali yanayohusu uendeshaji wa shughuli za mamlaka.

Sehemu ya nne ni utaratibu unaohusu utekelezaji wa majukumu ya mamlaka. Mhe. Spika, sehemu hii inahusu taratibu zitakazotumika katika masuala ya uchunguzi wa ajali za baharini, udhibiti wa mabaki ya meli yaliyoachwa baharini kutokana na ajali, udhibiti na uharibifu wa mazingira ya baharini kutokana na taka zinazozalishwa na meli.

Aidha, sehemu hii itatoa maelekezo kuhusu usalama wa safari za baharini, kusimamia meli za kigeni zinapoingia katika maeneo ya Zanzibar juu ya utekelezaji wa matakwa ya *International Ship and Port Facilities Security Court (ISPS Court).*

Vile vile inaelezea taratibu za kusimamia utekelezaji wa viwango vya usalama wa meli na uongozi wa kampuni za meli kwa mujibu wa viwango vitavyowekwa na mamlaka, kutoa taratibu za kufuatwa wakati shughuli za utafutaji na uokozi wa maisha ya watu baharini.

Sehemu ya tano mambo ya fedha. Mhe. Spika, sehemu hii inaelezea namna mamlaka itakavyoweza kukusanya fedha kwa ajili ya uendeshaji wake ambazo zinatokana na ada pamoja na huduma mbali mbali zitakazotolewa na mamlaka, kama vile usajili wa meli, utoaji wa leseni tofauti. Aidha, mamlaka itakuwa na uwezo wa kupokea msaada na kukopa fedha kutoka taasisi mbali mbali

zikiwemo za fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zake baada ya kukubaliwa na Mhe. Waziri.

Sehemu ya sita, makosa na adhabu. Sehemu hii inahusu makosa tofauti pamoja na adhabu zake kwa wale watakaokwenda kinyume na sheria, yakiwemo kuharibu mali za mamlaka, uendeshaji wa utoaji wa huduma zinazohusu isivyo halali au chini ya kiwango.

Mengine kuharibu au kwenda kinyume na taratibu za usalama wa bahari, kutoa taarifa za uongo na adhabu kwa makosa yanahusu usalama wa vyombo na kadhalika.

Sehemu ya saba, mambo mbali mbali. Mhe. Spika, sehemu hii inahusu mambo mbali mbali kwa ujumla kama vile uwezo wa mamlaka kuzuia meli kutoka na kutolipa ada zinazostahili, kutoa kinga ya kutoshtakiwa maafisa wa mamlaka kutokana na uharibifu utakaosababishwa na wao kuwa kazini.

Pia, kutoa uwezo wa mamlaka kwa waziri kutunga kanuni zitakazotumika kwa ajili ya kusimamia mambo mbali mbali na uwezo wa mamlaka yenyewe kutunga kanuni kwa baadhi ya shughuli zake.

Mhe. Spika, hitimisho. Sheria hii inakusudia kuweka mamlaka ambayo itakuwa na uwezo wa kisheria kusimamia utekelezaji wa sheria za usafiri wa baharini kwa ajili ya kuimarisha udhibiti wa usalama wa vyombo vya usafiri wa baharini kwa lengo la kupunguza majanga yanayotokana na safari za vyombo hivyo.

Vile vile kuiwezesha mamlaka iliyokusudiwa kuundwa kutambuliwa ndani na nje ya nchi yetu ya Tanzania.

Mhe. Spika, kupitishwa kwa sheria hii inayopendekezwa kutaisaidia Zanzibar kuwa chombo maalum ambacho kitatambulika duniani kama *Component Maritime Administration*.

Katika kufikia hatua hiyo wizara imeshakamilisha taratibu zote kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na *International Maritime Organization (IMO)*, kuanzisha *Maritime Administration* ya Zanzibar itatambulika kuwa *Maritime Administration* nyengine katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *Maritime Administration* hiyo ndio hii tunayoitungia sheria ya kuanzisha Mamlaka itakayoitwa *The Zanzibar Maritime Authority*.

Mhe. Spika, matarajio yangu ni kwamba kila mjumbe wa Baraza hili tukufu ameweza kupata mswada huu wa sheria. Hivyo, ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutushauri ipasavyo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako chini ya Kanuni ya 33 (1) na 28 (1) (d) naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Baharini Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na afya njema na kunipa nguvu za kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Mswada huu wa Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Baharini. Namshukuru Mwenyenzi Mungu pia kwa siku hii ya leo kuwajaalia na nyinyi wajumbe wenzangu kuendelea kuvuta pumzi za afya njema na uzima.

Mhe. Spika, wakati wengine wakiwa bado katika kufurahia mwaka huu mpya wa 2009, leo tukiwa na siku ishirini na saba (27) katika mwaka huu. Sisi wajumbe wako wa Baraza hili tukufu bado tumejawa na huzuni, majozi na simanzi kwa msiba mkubwa na mzito uliotupata kutokana na kifo cha mwenzetu ndugu yetu marehemu Mhe. Daud Hassan Daud aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Magogoni, kilichotokea tarehe 19 Disemba 2008 na kuzikwa tarehe 20 Disemba 2008, yaani ni mwezi mmoja tu uliopita.

Kifo chake kimetushtuwa wengi kwani kimetokea bila ya kutarajiwa kwa kweli kifo chake kimeacha pengo kubwa na lisiloweza kuzibika kirahisi, na ni msiba kwa taifa.

Mhe. Spika, **s**isi Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, kamati ambayo hadi alipokufa ndiyo kamati aliyokuwa akiifanyia kazi, tutamkumbuka milele, tunamkumbuka kwa mengi mazuri kutokana na mashirikiano makubwa aliyotupa katika utendaji wa kazi zetu za Kamati kwa muda wote. Michango yake iliyo hai iliisaidia sana kamati yetu katika kufikia ufanisi wa kazi zetu.

Tunakuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu "*Allah Subhana Wataallah*" uilaze roho ya marehemu mahali pema PEPONI Amin. Na uwape moyo wa subira ndugu, jamaa na familia yote ya marehemu katika wakati huu mgumu wa maisha ya upweke.

Mhe. Spika, kamati yangu vile vile inatoa mkono wa pole na rambi rambi kwa Mhe. Haji Omar Kheir kwa kufiliwa na mtoto wake mpendwa, na Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwa kufiliwa na mke wake mpendwa hivi karibuni. Tunamwomba Mwenyezi Mungu akupeni moyo wa subira pamoja na wafiwa wote, msiba wenu ni msiba wetu sote. Mwenyezi Mungu *Inshaallah* awape marehemu hao makaazi mema PEPONI AMIN!!

Mhe. Spika, kamati yangu imeundwa chini ya Kanuni ya 108 na kwa sasa ina wajumbe hai wafuatao:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Hamad Masoud Hamad | - | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Kamal Basha Pandu | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Ame Ussi Juma | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Subeit Khamis Faki | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Zakiya Omar Juma | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Omar Ali Jadi | - | Mjumbe |
| 9. | Ndg. Othman Ali Othman | - | Katibu |

Mhe. Spika, suala la kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Baharini hapa Zanzibar ni jambo moja muhimu sana ambalo serikali inaanzisha. Ingawa mswada huu umechelewa kuwasilishwa kutokana na umuhimu wake, lakini angalau serikali imeonesha nia nzuri kwa wananchi wake. Tunaipongeza sana serikali kwa wazo hilo la busara na kwa dhamira hiyo nzuri.

Mhe. Spika, kuanzishwa kwa Mamlaka hii ambayo itakuwa na jukumu, wajibu na uwezo wa Kusimamia Sheria ya Usafiri wa Baharini na matumizi ya vyombo vya usafiri wa baharini kutajenga imani na kuleta matumaini kwa wananchi juu ya usalama wao.

Mhe. Spika, Zanzibar kama kisiwa inategemea sana usafiri wa baharini na mnamo mwaka 2006 Baraza la Wawakilishi lilipitisha Sheria ya Kusimamia Usalama wa Baharini ambao inajulikana kama *The Maritine Transport Act* 2006.

Mhe. Spika, kazi za usajili na usimamizi wa meli hizo pamoja na usalama wa safari za baharini katika maeneo ya Zanzibar umetajwa katika kifungu cha 8 cha sheria hiyo, ambapo kutakuwa na usajili wa meli chini ya *Tanzania Zanzibar Register of Shipping* na *Tanzania Zanzibar International Register of Shipping* shughuli hizo zinasimamiwa na Mrajis wa Meli ambaye ameteuliwa chini ya kifungu cha 7 cha Sheria hiyo.

Hivi sasa kuna kitengo ambacho kilikabidhiwa rasmi majukumu hayo kutoka Shirika la Bandari mnamo mwezi wa Mei 2007, kabla ya hapo Shirika la Bandari lilikuwa likishughulikia masuala hayo kwa niaba ya wizara.

Mhe. Spika, kuanzishwa kwa Mamlaka itakayosimamia shughuli za usalama wa baharini katika maeneo ya Zanzibar, kutasaidia sana katika kuondosha tatizo la usalama wa abiria wanaopanda vyombo vya usafiri wa baharini katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Kitengo kimeanza kazi zake mwezi wa Februari, 2008 kwa usajili rasmi wa meli za kimataifa. Usajili huo umeanza kwa meli ndogo ndogo zenye ukubwa usiozidi tani 500 ambapo mikataba ya Kimataifa haitumiki kwa meli hizo. Wizara inaendelea kukamilisha taratibu za kuiwezesha Zanzibar kutekeleza majukumu katika Mikataba ya Kimatifa iliyoridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, lengo la kuwasilishwa mswada huu ni kutunga sheria itakayowezesha kuwepo na Mamlaka kamili itakayokuwa na uwezo kwa hali zote, kuhakikisha kwamba usafiri wa baharini unadhibitiwa vilivyo, ili kunusuru maisha ya wananchi na mizigo yao wanaotumia vyombo hivyo.

Katika Sheria hii kila uchunguzi wa ajali ya meli baharini utaanzia kwa hatua za awali kufanywa na Mamlaka na pale waziri atakapoona kuwa ajali inahitajika uchunguzi wa ziada, ataunda Tume kufanya uchunguzi kwa utaratibu kama ilivyoelezwa katika sehemu ya ishirini na nne ya Sheria ya Usalama wa Baharini Nam. 5 ya 2006.

Mhe. Spika, kamati inashauri Mamlaka kupatiwa miundo mbinu ya uhakika wakati wa kutekeleza sheria hii, ili iweze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa na kupatiwa nyenzo zitakazowezesha maeneo mbali mbali kufikika pindi ikitokea ajali na wananchi kuweza kuokolewa.

Suala la utaratibu wa usafirishaji wa abiria hivi sasa lina matatizo kutokana na upotevu wa mizigo ya abiria. Kamati inashauri ichukuliwe hatua ya kurekebisha hali hiyo pamoja na msongamano unaotokea wakati wa kuingia na kutoka melini.

Mhe. Spika, kamati inaunga mkono sheria hii kutokana na umuhimu wake utakaowezesha Mamlaka kuwa huru na kuweza kufanya mambo yake kwa ufanisi zaidi.

Suala la usafiri wa vyombo vidogo vidogo limetajwa katika sheria hii. Kamati inashauri kuwekwa mkazo zaidi kuvishughulikia vyombo hivi kwa kuhakikisha

kwamba kuna utaratibu unaoeleweka wa kuchukua abiria, ili itakapotokea ajali iweze kujulikana kwamba chombo kilikuwa na abiria wangapi.

Mhe. Spika, **s**uala la mazingira katika bahari ni la kupewa umuhimu mkubwa kutokana na kila kiumbe kuwa haki ya kuishi na katika mazingira yaliyo mazuri. Kamati inashauri mazingira ya baharini yapewe uzito unaostahiki kwa kutolewa elimu itakayowawezesha wananchi watakapoona dalili za kuharibiwa mazingira hayo waweze kutoa taarifa kunakohusika ili wahalifu waweze kukamatwa na walioathirika wapatiwe fidia kutokana na tatizo hilo.

Mhe. Spika,,suala la mabaharia lina umuhimu wake katika utaratibu mzima wa uendeshaji wa vyombo vya baharini, na pindi suala la mabaharia likishughulikiuwa ipasavyo nchi itaweza kunufaika kiuchumi kutokana na kupata asilimia fulani kutokana na kazi watakazofanya mabaharia hao na kupunguza tatizo la ukosefu wa kazi, na kutungwa kanuni zitakazosaidia Chama cha Mabaharia.

Mhe. Spika, Kamati inashauri zichukuliwe hatua madhubuti katika suala la uokoaji ili ajali ziweze kupungua kwa kuimarisha kitengo kitakachokuwa kinashughulikia suala hilo na kuwekwa kanuni ambazo atakayezikiuka atachukuliwa hatua ya kufikishwa katika vyombo vya Sheria.

Mhe. Spika, suala la chombo kusababisha moto katika katika bandari ni la kuangaliwa kwa uzito wake kwa kufanywa ukaguzi wa mara kwa mara kwani ajali ikitokea huwa kubwa na inaweza kusababisha maafa pindi ikiwa haikudhibitiwa, hasa kuonekana kwamba kesi nyingi za meli huwa hazipatikani ushahidi wake, na kamati inashauri wananchi waelekezwe sehemu ya kwenda pindi matatizo kama haya yanapotokea ili hatua za kufaa ziweze kuchukuliwa.

Mhe. Spika, baadhi ya marekebisho yaliyofanywa na kamati ni pamoja na kifungu cha 2 (i) cha Mswada ambacho kimefutwa kilichokuwa kinasomeka kama ifuatavyo:-

(a) ”Eneo la bahari la Zanzibar” maana yake ni ”eneo ambalo limo ndani ya mamlaka ya iliyokuwa Jamhuri ya Zanzibar kabla ya Muungano wa 1964 baina ya Zanzibar na Tanganyika”

Mhe. Spika, Kifungu cha 3 (1) mstari wa kwanza kinafanyiwa marekebisho kwa kuingizwa maneno ”yenye uwezo wa kurithi na kurithiwa”

Kifungu cha 3(1) mstari wa pili neno ”usalama” litasomeka ”usafiri”.

Mhe. Spika, Katika kifungu cha 4(1)(vi) neno ”kujifurahisha” lisomeke ”starehe”
Kifungu cha 5 (1)(z)(iii)(aa) kinaandikwa upya kama ifuatavyo:-

”Kutoa taarifa za usalama na taarifa nyenginezo baharini”

Mhe. Spika, Kifungu cha 8(2)(b) mstari wa pili neno ”Injinia” lisomeke ”mhandisi” kifungu cha 21(2) mstari wa pili neno ”msajili” lisomeke ”Mrajis” na sehemu yoyote iliyotajwa katika mswada huu ambayo vifungu vyake vinatoa adhabu ya fedha mbele ya neno ”fedha” isomeke ”cha thamani ya shilingi”.

Mhe. Spika, Kamati inaunga mkono utaratibu wa uundwaji wa Bodi ambao ndio mhimili wa Taasisi yoyote inayojitegemea ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi kwa kuendeleza mbele taasisi inayohusika na baada ya kupitishwa Sheria na baadae kuunda Bodi.

Mhe. Spika, hayo ni baadhi ya marekebisho ambayo kamati yangu imeyaona na kuyafanyia kazi kama nilivyokwisha kufafanua namna ya uchambuzi wa vifungu na maana iliyokusudiwa kwa kila kifungu cha Sheria hii, kupitishwa kwa Sheria hii kutasaidia kupatikana ufanisi katika uendeshaji wa usafiri wa baharini.

Mhe. Spika, katika Sheria hii ikiwa itapitishwa itasaidia kuweka taratibu zinazotumika katika masuala ya uchunguzi wa ajali baharini kutokana na ajali, udhibiti wa uharibifu wa mazingira ya baharini kutokana na taka taka zinazozalishwa melini.

Mhe. Spika, Ikiwa Sheria hii itapitishwa itasaidia nchi kuwa na chombo chake cha usimamizi wa masuala yote ya baharini na kuondoa tatizo la masikitiko kwa wananchi kuhusu huduma mbaya za usafiri.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaipongeza sana Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa kuleta Mswada huu unaokwenda na wakati kwa kuangalia mustakbali wa maendeleo ya nchi yetu ili tija iweze kupatikana na uchumi kukua.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii adhimu na maalum kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati yangu kwa nidhamu na mashirikiano yao makubwa waliyonipa wakati wa kuupitia Mswada huu na kuufanyia marekebisho kutokana na umuhimu wake.

Mhe. Spika, matumaini yangu ni kwamba waheshimiwa wajumbe watauchangia ipasavyo na kwa kadri ya uwezo wao kwa lengo la kuufanya uwe bora zaidi na hatimae kuupitisha kwa pamoja ili lengo na madhumuni ya kuanzishwa Sheria hii kufikiwa na kutupa matumaini mapya na yaweze kuwaondoa hovu na wasi wasi wananchi wakati wanaposafiri.

Mhe. Spika, Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Said Ali Mbarouk (Waziri Kivuli, Wizara Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi):** Mhe. Spika, ninashukuru Mwenyezi Mungu Subhana wa Taala kwa kunipa Uzima na uhai, na kunipa afya ya kusimama hapa kuelezea machache kuhusiana na hoja iliyoko mezani baada ya kupata ruhusa yako.

Kabla sijaendelea naomba nikupongeze wewe na wajumbe wengine wa Baraza lako waliobahatika kwenda na kurudi salama kwenye Ibada ya Hija mwaka huu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu azitakabalie Hija zenu, azifute dhambi zenu na azitakase nyoyo na nafsi kuepuka madhambi baada ya kurejea.

Mhe. Spika, muda mrefu Kambi ya Upinzani ya Baraza lako tukufu imekuwa ikiitaka Serikali kuanzisha na kuandaa utaratibu wa maana, ulio wa kitaalamu na uliowazi wa kusajili meli za kigeni ili kujipatia mapato na kukuza uchumi wetu. Katika jambo hili, kunahitajika maandalizi mazuri na makubwa, ili kuona tija katika nchi yetu inapatikana kutokana shughuli yenyewe na madhara yanaepukwa kutokana na athari ya shughuli hio.

Wakati Kambi yangu ya Upinzani haijaona wala kujulishwa na Waziri maandalizi aliyoyachukua katika kuanzisha jambo hili muhimu, tunashtukiwa tunaletewa mbele ya Baraza lako tukufu Mswada wa sheria ya kuanzisha mamlaka ya usafiri baharini.

Mhe. Spika, ingalikuwa sheria za kuanzisha Mamlaka ndio maendeleo, Zanzibar ingelikuwa miongoni mwa nchi zilizoendelea, maana mamlaka zishazoanzishwa ni nyingi, lakini ufanisi wake ni mtihani, mwaka juzi palianzishwa mamlaka ya Maji kwa matumaini mema, lakini hali ni kinyume chake, bado mamlaka iliyokuanzishwa haijasaidiwa ipasavyo na serikali kutimiza malengo yake ilipokuwa ni Idara ya Maji, mie kwangu japo wiki mara moja nilikuwa nikipata maji, sasa kwenye mamlaka, hufika mwezi napata mara moja na pengine usiku wa manane, ama bili ya maji huwa haichelewi!!. Jee Mhe. Waziri amefanya maandalizi gani ya kuanzisha mamlaka hii.

Mhe. Spika, kihistoria matumizi ya pwani, bahari na bahari kuu na mipaka ya maeneo ya bahari; yamekuwa yakisimamiwa na kuongozwa na Sheria za Kimataifa kama zinavyojulikana *"Freedom of the Sea's Doctrine'*.

Mwanzoni, sheria hizo zilitoa Mamlaka ya meli tatu tu kutoka ufukweni kwa nchi husika kuwa na uhuru na miliki nazo, lakini baadae mwanzoni mwa karne ya 20, *”Freedom of the sea Doctrine’* ilionekana na udhaifu mkubwa wakati wa kinyanganyiro cha raslimali za bahari, na ndipo mwaka 1982, nchi zilikubaliana kuanzisha mkataba unaoitwa *UNCLOS’82,* ambao ndio msingi wa Sheria nyingi za Kimataifa za matumizi ya Bahari.

Mhe. Spika, wakati tunajadili Mswada huu wa matumizi katika raslimali ya bahari yetu, ni vizuri Mhe. Waziri akalieleza baraza lako tukufu, faida na athari ya mikataba hio, na uwezo na mamlaka ya Zanzibar katika kunufaika nayo.

Mhe. Spika, Katika baadhi ya vipengele vya mkataba huo wa *UNCLOS’82,* nchi zilipewa mamlaka ya kuanzisha maeneo ya bahari zao *(maritine spaces)* na msingi iliyoongoza mipaka yao *(maritime boundaries)* na majirani zao. Serikali ya Tanzania imeridhia mktaba wa *UNCLOS’82* tokea mwaka 1984/85, na mwaka 1989/90 Bunge la Jamhuri ya Muungano ilitunga sheria inayoitwa *”Territorial sea and Exclusive Economic Zone”* iliyosema inafanyakazi hadi Zanzibar.

Jee Mhe. Waziri analihakishiaje Baraza hili kwamba Mamlaka itayotokana na Sheria tunayoijadili, haitakwamishwa na Sheria hiyo ya Bara, na au Mamlaka yenyewe ikawa wakala wa utekelezaji wa sheria hio ya Bunge?

Mhe. Spika,kabla sijaingia ndani ya Mswada wenyewe kupata ufafanuzi ninaomba kwa ruhusa yako Kambi ya Upinzani ielezwe mambo ya jumla ya matayarisho na sera kama ifuatavyo:

1) Nchi ya Panama ndio ya mwanzo iliyoanzisha utaratibu wa kusajili meli za kigeni mwaka 1919, ikafuatia nchi ya Liberia mwaka 1946 na baadae zikafuatia nchi nyingi nyengine, lakini, kwa sasa nchi ambazo zimepiga hatua ya kujivunia katika biashara ya kusajili meli ni PANAMA, LIBERIA NA BAHAMAS, Jee Mhe. Waziri kabla ya kuamua kuleta Mswada huu amewahi kupeleka wataalamu wake wangapi angalau katika moja ya nchi hizo kwenda kujifunza kwa matayarisho ya shughuli hii hapa Zanzibar.

Mhe. Spika,katika ulimwengu huu kuna watu wanapinga sana utaratibu wa kusajili meli za kigeni bada ya kupata uzoefu wa nchi zao, na sababu zao ni kwamba utaratibu huu.

- Unasababisha meli hizo kukwepa mfumo wa sheria za kazi

- Unasababisha meli hizo wafanyakazi wake kufanya kazi masaa mengi kwa malipo haba, bila ya matibabu stahiki

- Unasababisha meli hizo kuwepo ufanyajikazi usio salama

- Unasababisha meli hizo kusafirisha bidhaa haramu kama silaha na nyenginezo

- Unasababisha meli hizo kuharibu mazingira

- Unasababisha meli kunyima nafasi ya vyama vya wafanyakazi kama *sea farer's Trade Union* kuwatetea wafanyakazi wake kwa sababu meli zenyewe hazina uraia madhubuti

Jee Mheshimiwa Waziri anaweza kuliarifu Baraza lako tukufu amejiandaa vipi na mamlaka yake kudhibiti na kukabiliana na athari hizo kitaalamu, kivifaa na kisheria.

Mhe. Spika,katika utaratibu wa kutoa usajili wa meli, aghalabu uko wa namna mbili unaotambulikana (1) KWENYE NCHI YA BENDERA*(FLAG STATE)*na (2) kwenye nchi ya BANDARI *(PORT STATE)*

1. *FLAG STATE*, huu ni utaratibu unaotoa mamlaka kwa nchi kushughulikia udhibiti wa meli ambazo zinapewa usajili chini ya Bendera ya nchi husika.

**2.** *PORT STATE* (NCHI YA BANDARI)

Huu ni utaratbu unaotoa mamlaka kwa nchi kushughulikia udhibiti wa meli ambazo zinapewa usajili chini ya Bendera ya nchi nyengine, Mamlaka ya aina hii ni dhaifu na inafanyakazi tu katika eneo la pwani pwani

Jee Mheshimiwa Waziri anaweza kulieleza Baraza lako tukufu mamlaka yetu itafanyakazi kwa utaratibu wa *Flag State* chini ya Bendera ya Nchi ya Zanzibar au chini ya utaratibu dhaifu wa *PORT STATE* chini ya utaratibu wa Bendera ya Nchi nyengine.

Mhe. Spika, baada ya kuomba ufafanuzi kutoka kwa Mhe. Waziri wa maelezo ya jumla na sera kuhusiana na Mswada, sasa naomba uniruhusu niingie ndani ya Mswada kuomba ufafanuzi juu ya masuala machache na pia ushauri wangu juu ya baadhi ya vifungu vya Mswada huu.

1. Jina la Sheria ni Zanzibar *Maritime Authority au Zanzibar Maritime Regulator Authority?*

2. Katika kifungu cha 5 (1) (c) nakala ya Kiswahili – pametajwa "kusimamia meli zilizosajiliwa Zanzibar na kusimamia shughuli za meli na biashara ya usafiri wa BAHARINI ZANZIBAR", na katika nakala ya Kiengereza, pametaja kusimamia meli zilizosajiliwa Zanzibar na kusimamia shughuli za meli na biashara ya usafiri ndani ya *"ZANZIBAR MARITIME ZONE"*

   Naomba kujulishwa na kuelezwa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri *'Zanzibar Maritime Zone'* ni ipi, na kwa nini hakuiweka kwenye ukurasa wa ufafanuzi, Jee kuna sababu yeyote ya kikatiba inayotuzuia kuitaja na kuinasibu hio *"Zanzibar Maritime Zone"*.

3. Mhe. Spika, katika kifungu cha 5 (1)d imetaja moja ya jukumu la mamlaka ya usafiri wa Baharini Zanzibar ni "kusajili na kutoa leseni kwa meli za biashara, kwa ajili ya kutimiza malengo ya Kitaifa na Kimataifa, KUTOA URAIA, ushahidi wa umiliki na nyaraka za umiliki, kusajili rehani na kueka jina la chombo".

   Mhe. Spika,naomba kupata ufafanuzi tokea kwa Mhe. Waziri anamaana ipi anaposema KUTOA URAIA, kwani ninavyojua mie SMZ haina Mamlaka ya kutoa uraia hata kwa Wazanzibari wake, achilia mbali kwa watu wa kigeni.

4. Mhe. Spika, katika kifungu cha 5(1)(m) kuna tafauti kubwa ya maana baina ya Mswada wa Kiswahili na wa Kiengereza, wakati katika nakala ya Kiswahili, Mhe. Waziri anazungumzia pamoja na mambo mengine pia wenyeji kushajiishwa kufanya kazi za huduma, katika nakala ya Kiengereza Waziri anazungumza pamoja na mambo mengine pia ushajiishaji wa uundaji wa zana za usalama za baharini kwa wenyeji. Tofauti hio ni kubwa kimaana na na namuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi amekusudia nini hasa.

5. Mhe. Spika,katika kifungu cha 5(1)(o)(ii) Hoja ya Mheshimiwa Waziri inataja "mafao ya wafanyakazi wa melini yanatimizwa kwa mujibu wa viwango vya Kitaifa kwa meli za ndani, na viwango vya Kimataifa kwa meli zinazofanya safari za Kimataifa.

   Jee neno viwango vya Kitaifa vimekusudiwa TAIFA lipi? Naomba ufafanuzi.

6. Mhe. Spika,katika kifungu cha 5(1)p(iv) na (v), mswada unataja kupendekeza kwa ajili ya uteuzi, ninaomba kupata ufafanuzi mamlaka itakua inapendekeza kwa nani, na anayeteua atakua nani kwa muhibu wa sheria hii itayotokana na Mswada huu.

7. Mhe. Spika,katika kifungu cha 5(1)(u), hoja hii inataja "kuishauri Serikali masuala ya usajili wa baharini pamoja na URIDHIAJI na utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa, huduma za baharini, huduma za bandari na mambo mengine ya kiufundi" jee Mheshimiwa Waziri anataka kuliambia Baraza lako tukufu kwamba SMZ sasa imepewa mamlaka ya kuridhia mikataba ya Kimataifa? Kwangu mie hii ni habari njema na labda ndio mafanikio ya vikao vinavyoendelea vya kuondoa kero za Muungano.

8. Mhe. Spika,katika kifungu cha 7(2) Mswada umezungumzia uteuzi wa mwenyekiti wa Bodi ambaye atateuliwa na Rais, lakini Mheshimiwa Waziri ameshindwa kumsaidia Rais aina ya mtu, uzoefu, elimu, uraia wa mtu, na ukaazi wa Mwenyekiti wa Bodi, hii ni kasoro kubwa na ambayo haikubaliki, inayohitaji kurekebishwa

9. Mhe. Spika, Katika kifungu cha 8(1) kinazungumzia Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka kuteuliwa na Rais. Kwa kweli hili ndio tatizo linalopata uendeshaji wa mashirika mengi ya SMZ,nalo ni uteuzi wa watendaji / wataalamu kuhusishwa na siasa, huu ni utaratibu wa kizamani, unaolea uzembe na kuanguka kwa ufanisi.

   Nashauri Mkurugenzi Mkuu ateuliwe na Bodi baada ya kutangaza nafasi hio na Wazanzibar wakaomba kwa mujibu wa uwezo wao, uzoefu wao ujuzi na Elimu zao.

   Utaratibu huu utamfanya Mkurugenzi mkuu kuwajibika moja kwa moja kwa Bodi ambayo inaweza kumuondoa wakati wowote akifanya uzembe au ufisadi.

10. Mhe. Spika,katika kifungu cha 10 a, b MSwada umeipa Bodi uwezo wa kufanya <u>mabadiliko madogo</u>

    a) ya viwango vya Kodi
    b) vya Viwango vya mishahara

    Mheshimiwa Waziri anaweza kutueleza kufanya mabadiliko madogo maana yake nini? Hivi amesahau kwa wengine sh. Billioni nivijisenti, na wengine ni utajiri wa kupindukia?

Kwanini asitaje kiwango cha asilimia ambacho kingeweza kupimika vizuri kimahesabu na kitarakimu?

11. Mhe. Spika, katika kifungu cha 14(2) mswada unazungumzia masuala ya utupaji taka na umwagaji taka, ninaomba ufafanuzia kutoka kwa Mheshimiwa Waziri haoni kipengele hichi kinaweza kuipa mamlaka uwezo wa kutupa au kumwaga taka kutoka kwenye mameli ya nje, na hii jee haiwezi siku moja Zanzibar ikaja ikaruhusu umwagaji wa taka za mabaki ya *"Nuclear"* kutoka kwenye viwanda vya Silaha vinavyotafuta wapi pa kumwaga taka zao.

Nashauri kifungu hichi kirekebishwe ili kiwe ni kosa kubwa sana kutupa taka za aina yoyote baharini.

12. Mhe. Spika, kifungu cha 15(1) Mswada unataja kwamba mamlaka itaitaka meli inayosafiri ndani ya eneo la Zanzibar kufuata kanuni za Kimataifa za kuzuia mgongano baharini; Jee ndani ya eneo la Zanzibar kwa mujibu wa Mswada huu ni lipi

13. Mhe. Spika, kifungu cha 27(2) kinataja kwamba mtu yeyote anaweza kumkamata mtu mwengine yeyote ambae kwa maoni yake atakuwa ametenda kosa, hii nadhani ni utaratibu utaopelekea watu kukamatana ovyo, kusumbuana na pengine kusababisha ugomvi ndani ya raia, kwani kisheria mamlaka imetoa uwezo wa nani anauwezo wa kumkamata mwengine, nashauri hichi kifungu kitafutiwe utaratibu mzuri zaidi wa kisheria za kukamata *(Arrest procedures)* na vifungu 28 na 29 vinahitaji kuainishwa vizuri ili kuleta maana halisi iliyokusudiwa, vyenginevyo vinaweza kuja kuwapa adhabu wananchi ambao wanatoa huduma ya usafiri wa mitumbwi na ngalawa baina ya visiwa vidogo vidogo, ambapo taratibu za kuibiana pondo na kafi (kama vitu vinavyohatarisha usafiri vikikosekana) ni jambo la kawaida, hivyo kuja mtu kutoleshwa faini dola elfu ishirini kwa kuficha, kuiba au kuzuia kafi au pondo litakuwa jambo la ajabu sana, nashauri vipengele hivi viainishwe vizuri.

14. Mhe. Spika, kifungu cha 46 a kinahitaji kuangaliwa zaidi, ili mamlaka au wafanyakazi, waweze kuwajibika kwa hasara ya chombo itachokipata kutokana na upotoshwaji au maelezo yasio sahihi ya wafanyakazi wa mamlaka au wakala wake, kukiwacha kifungu kama kilivyo kunaweza kuleta uzembe ndani ya mamlaka na au wakala wake na hivyo kutia hasara meli zinazopewa huduma na mamlaka na hivyo kutia hasara huku mamlaka ikikwepa kuwajibika kisheria.

15. Mhe. Spika, katika Jadweli linaloshusiana na muundo wa Bodi, kifungu 1C kinataja Wajumbe wengine ambao watateuliwa na Waziri, lakini kifungu hakielezi idadi ya wajumbe, nashauri patajwe wajumbe kwa idadi, lakini pia kifungu hakitaji wajumbe wa Bodi hii watoka maeneo gani ya jamii yetu.

Mimi nashauri idadi yeyote isizidi saba na angalau wawili kati yao watoke sekta binafsi itayosimamiwa na Mamlaka hii.

16. Mhe. Spika, katika kifungu cha 4 cha Jadweli kinachohusu kuacha kwa mjumbe, kifungu kidogo 4c kuna maandiko yanayosema" Atashindwa kwa namna yoyote ile kupoteza sifa za mjumbe"

Tafsiri ya maneno hayo hayaelekei kutoa Taswira kwa mjumbe, ninaomba kupata ufafanuzi maana yaliokusudiwa.

17. Mhe. Spika,uanzishwaji wa Mamlaka ya aina hii umetafautiana baina ya nchi na nchi.

- Kuna nchi kubwa zenye uchumi unaokuwa vizuri, zinaanzisha mamlaka kwa mfumo kama ulivyopendekezwa na Mswada huu mfano nchi ya Australia.
- Kuna nchi kubwa zenye uchumi mdogo, zinaanzisha mamlaka ya usafiri baharini pamoja na usafiri nchi kafu, mfano wa *SUMATRA* Bara
- Kuna nchi ambazo ni ndogo zenye miundo mbinu ya bahari, huwa zinachanganya mamlaka ya Bandari na usafiri baharini mfano nchi ya Singapore.

Jee uamuzi wa kuanzisha mamlaka kwa utaratibu huu amezingatia kitu gani?

18. Mhe. Spika, kama nilivyoanza katika utangulizi wa maelezo haya, Nchi ya Zanzibar inaweza kufanikiwa sana kiuchumi ikiwa itafanya maandalizi mazuri katika kusimamia shughuli za usafiri baharini kitaifa na Kimataifa. Na hii itawezekana ikiwa Waziri atakuwa na Sera mzuri na madhubuti, itayokuwa na maandalizi na usimamizi mzuri wa kitaalamu.

Ikiwa leo tunaletewa Mswada, lakini Waziri ameshindwa hata kumiliki afisi ya maana ya msajili wa meli, pia hana wataalamu wa

kutosha, na wataalmu waliopo hawaelekei kutumiwa ipasavyo, hawalipwei vizuri na kushirikishwa vyema. Nimecheki na mamlaka ya *SUMATRA* Bara hadhi na maslahi ya wataalamu ya aina yao wenye taaluma na uzoefu sawa, nitafauti sana, Waziri asipofanya maandalizi wataalamu watamkimbia, hali itayosababisha vyombo viatavyoomba kusajiliwa Zanzibar kwenda kukaguliwa na kupewa baadhi ya vyeti bara, likitokea hilo, mamlaka itazorota na haitokuwa tofauti na utitiri wa mamlaka nyengine zilizoanzishwa ndani ya visiwa hivi, ikawa ni mamlaka jina tu lakini hakuna huduma inayopatikana, wala ufanisi wa maana.

Mhe. Spika, kabla sijamaliza katika kifungu cha 4(1) "Mamlaka itatekeleza majukumu yake" halafu (viii) "Vyombo vya kuchimbia mafutabaharini , vyombo vya uzalishaji na mitambo inayoambatana nayo".

Jukumu hili ni muhimu sana na namshukuru Mhe. Waziri kwa kuliingiza hapa, ni jambo ambalo angalau kwa mara ya mwanzo naona serikali ya Zanzibar inafanya maanadalizi japo machache katika rasilimali yetu ya mafuta ni jambo jema, angalau Mhe. Waziri katika taasisi zetu ziliomo katika Zanzibar kwamba kuna chombo ambacho kinafikiria kwamba kuna siku moja itakuwa na jukumu la kusimamia rasilimali yetu, ni jambo zuri mimi namshukuru sana kuliweka hili na kuipa mamlaka. Hii ni rasilimali yetu ni lazima tuiandalie mazingira ya kufaidika nayo, vyenginevyo tusipofanya mazingira mazuri na matayarisho mazuri wajanja wanaikodolea macho na wataichukua.

Sasa hili ni jambo zusi sana na mimi namshukuru Mhe. Waziri kwa kuliweka na nimalizie tu kwa kusema kwamba Mhe. Spika, uniruhusu kwa hili naomba nipongeze sana na nilisifu hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Amani Abeid Karume katika sherehe za Mapinduzi, ni hotuba nzuri yenye kuelekeza umoja wa nchi nashukuru sana.

Lakini Mhe. Spika, hivi juzi nimevunjwa moyo sana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba inaenda kinyume na yale ambayo Mhe. Amani Abeid Karume aliyaelekeza, inalenga kuwabagua Wazanzibar na vyenginevyo sasa hili naomba niseme hilo ili nisikike vizuri.

Mhe. Spika, nawashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza na nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi na kuweza kuchangia hayo machache. Ahsante sana.

**Mhe. Abubakar Khamis Bakary:** Mhe. Spika, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kufika hapa, lakini la pili nakushukuru wewe

kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo ambayo nilijitahidi kuiomba mapema kwa sababu maalum ambayo baadae utaifahamu.

Mhe. Spika, kwanza ningelipenda nimshukuru Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa maelezo yake mazuri, angalau ya kutaka Zanzibar yetu ionekane kwamba ni Zanzibar.

Pili namshukuru Mwenyekiti wa Kamati kwa maelezo yake, na tatu namshukuru Waziri Kivuli kwa maelezo yake. Maelezo yote haya yanasaidia sana Mswada huu. Nichukue nafasi hii kuishukuru serikali kwa kutaka kuonesha kwamba Zanzibar bado ni nchi.

Mhe. Spika, Mswada huu nimeupitia nilikuwa nikubaliane nao asilimia mia moja, lakini una matatizo. Lakini nashukuru sana kwamba serikali ipo na hasa Mhe. Waziri Kiongozi. Matatizo haya ndio madhumuni yangu ya kutaka kusema mwanzo. Matatizo yaliyomo katika mswada huu ni kwamba hata tukiupitisha leo na ukatiwa sahihi na Rais, basi bado utakuwa sio sheria halali kwa sababu ya matatizo ya kisheria yaliyokuwemo.

Mimi ningelipenda sana Mswada huu upitishwe na ninayo niya hasa ya kwamba Mswada huu ungelipita leo. Tatizo langu ni kwamba una matatizo ya kisheria ambayo hatuwezi kuupitisha. Naomba Mhe. Spika, nichukue nafasi yako kidogo kuelezea matatizo hayo ili baadaye si vibaya kama nikieleza maelezo yangu na serikali ikayaona, likaahirishwa Baraza wakenda wakajadili suala hili.

Mhe. Spika, nilikuwa naupitia Mswada huu kuanzia kifungu cha mwanzo mpaka cha mwisho cha 52. Kuna makosa madogo madogo ya kikawaida ambayo hayo nisingelipenda kuyaeleza hivi sasa kwa sababu baadaye huu Mswada utakuwa si halali. Nilipofika katika kifungu cha 52 hapa ndio kwenye matatizo makubwa na naomba kwa ruhusa yako Mhe. Spika, niitanabahishe serikali.

Kifungu cha 52 (1) *"Section five of the maritime transport act no 5 of 2006 is here by reppealed and replaced by the following"*

Sasa *maritime transport act no 5* ya 2006 ndio hii, ninayo hapa. Kifungu cha 5 Mhe.Spika, katika sheria hiyo ya nambari 5 ya 2006 inasema kwamba,

*"The Minister is exercising his powers under this act shall establish a statutary body to be known as*

*Zanzibar Maritime Safety Administration to oversee his matters of maritime safety and security. "*

Hichi ndio kifungu cha 5 cha sheria tuliyoipitisha mwaka 2006. Katika sheria hii ya mwaka 2006, inasema kwamba Waziri ataanzisha *statutary body* ndiyo sheria inayotoa ruhusa. *Statutary body* kisheria ni  Shirika, kwa hivyo waziri alipewa uwezo katika sheria kuanzisha shirika la mambo haya haya. Leo tunafanya sheria hii, tunakifuta kifungu hichi kilichomo katika sheria ya 2006. Kwanza katika *principle* za *drafting*, nasema hii *not authority.*

Mhe. Spika, katika *degree* yangu ya pili nilichukua *drafting*, kwa hivyo najua ninachokisema. Katika *principle* za *drafting* huruhusiwi kufuta sheria ukaitumia katika kikao kile kile unachoifuta, itakuwa si halali. Kwa sababu leo tunaifuta hii na hata kama tukikubali kwamba tunaifuta haiwezi kutumika hii sheria mpaka sahihi ipatikane *assent* ya Rais, kwa hivyo itakuwa bado si sheria hii.

Sasa tumekifuta kifungu hichi cha 5 katika sheria hii ambacho kilikuwa kinampa uwezo Waziri kuanzisha *statutory body*, tukaanzisha sheria kwa hii, *it means* kwamba tumefuta sheria kabla haijakubaliwa kwamba kweli imefutwa, tumeanzisha kitu kile ambacho tulikuwa tunakitaka, itakuwa sheria hiyo siyo halali. Nikasikitika sana na nikaona bora niseme mwanzo, ili tuone kwamba hapa pana makosa ya kisheria. Utaratibu ni kwamba tunapotaka kufuta kifungu hichi ndio kukawa na sheria zinazoitwa *Miscellaneous Amendment Act*. Tunafuta vile vifungu ambavyo tunavitaka, tukishakuvifuta Rais anatia sahihi. *It means* sasa kifungu cha 5 cha sheria hii, kinakuwa hakimo, kitakuwemo kile ambacho Rais ameshatia sahihi.

Kwa hivyo, kikao kinachofuata chengine ndiyo tungeliweza kutunga sheria hii kwa misingi hiyo kwamba kifungu kile sasa kimeshafutwa. Lakini, hivi sasa tukikifuta hichi ndani ya sheria hii ambayo hata tukiipitisha hivi sasa bado Rais hajatia sahihi, kwa hivyo bado itakuwa sio sheria, haiwezi ikawa ni sheria ambayo imetupa *authority* ya kufanya sheria ya mamlaka hii. Bado sheria itakuwa ni ile ile sheria Nam. 5 ya mwaka 2006 ya waziri kufanya *statutory cooperation* au *statutory authority*.

Mhe. Spika, huu ni Mswada mzuri na mimi naukubali sana, lakini hata tukiupitisha hapa hii sheria baadaye akaitia sahihi Rais. Utaratibu wa sheria ni kwamba ile sheria iliyotangulia ndiyo itakayokuwa ina nguvu kuliko ile iliyotungwa leo. Mfano hii imetungwa 2006, kwa hivyo hii ina nguvu zaidi kuliko hii itakayotungwa 2009. Kosa lolote litakalofanywa humo, mtu yeyote atakayefanya kosa humo, hata tukimshtaki hatuwezi kumtia hatiani kwa sababu

yeye atakuwa na sheria hii kifungu Nam. 5 kilisema kwamba kuundwe *statutory authority* sio mamlaka haya.

Mhe. Spika, tunafanya kitu kizuri, lakini sio halali kwa utaratibu huu. Ushauri wangu kwa serikali tuahirisheni hii sheria kuipitisha kwa sababu itakuwa sio halali, tufanye *Miscellaneous Amendment Acts* ya kifungu hichi Nam. 5. Tukisha kufanya hivyo, ndio itatupa uhalali wa kufanya sheria hii. Tukisha kupata uhalali wa sheria hii baada ya Rais kutia sahihi, sheria hii itakuja Barazani tutaipitisha na mimi nitaiunga mkono mia juu ya mia wakati huo, kwa sababu ni sheria nzuri na itatusaidia.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nina hayo ya kuishauri serikali kwa moyo safi kabisa na kwa dhati yangu kwamba hichi tunachofanya hivi sasa ni kitu ambacho tumekikosea kisheria na naomba tukirekebishe kiwe sawa.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru ahsante.

**Mhe. Spika:** Nadhani tuendelee na majadiliano halafu tuone serikali mwisho itazungumza nini kuhusiana na hichi kilichoshauriwa.

**Mhe. Ali Abdalla Ali:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia katika Mswada huu. Mimi si mwana sheria mimi ni mwana siasa niliyonayo nitayatoa na serikali kadri itakavyofanya uwamuzi tena itatizama na yangu kama yanafaa itayachukua.

Kwanza niipongeze serikali kupitia wizara yetu kwa kuleta Mswada huu ambao muda mwingi sana tulikuwa tunaupigia debe, lakini hivi sasa nadhani umefika wakati umewasilishwa petu ambao utapunguza matatizo mengi sana katika usafiri wa baharini. Mswada ambao umewasilishwa sasa hivi na Mwenyekiti wetu wa Kamati kwa ufasaha, kawasilisha uzuri na kwa kweli Mswada ni mzuri.

Mimi kabla sijaenda kwenye Mswada wenyewe nilikuwa nina maoni manne naomba niyatoe kwa wizara na kama ingewezekana, basi wangeongeza kwa njia yoyote kama kikanuni au kama kuna njia nyengine ya kuweza kuongezwa ingelisaidia katika kuuboresha Mswada wetu huu.

Mhe. Spika, kwa kweli sisi kama ni wananchi tuliokuwepo katika visiwa ni lazima tutatumia vyombo vya bahari kutoka eneo moja na kwenda katika eneo jengine, la si hivyo utatumia ndege. Lakini kwa wananchi wetu wengi uwezo wao ni kutumia vyombo vya baharini na vinatumika tangu enzi na enzi. Mimi napata fahamu yangu vitu hivi vipo, majahazi, ngalawa, mitumbwi, meli n.k.

Mhe. Spika, mchango wangu wa mwanzo katika huu Mswada wetu haya mambo ninayoyazungumza sikuona kuwekwa pahala na ni mambo ya msingi kidogo. Mfano  bandari yetu imejengwa uzuri, kule kwenye bandari kubwa tunashusha mizigo na huku tumetengeneza tishari wanashuka abiria na mizigo yao. Kwanza tumebagua, ili kuweza kuondosha hatari inayoweza kutokezea. Lakini bado kuna hatari ambayo inaonekana, lakini hatujaione athari yake kwa kipindi hichi cha sasa hivi labda kwa hapo baadaye.

Mhe. Spika, pale kuna meli nyingi ambazo huwa zinatia nanga. Meli zile zipo zinazofanya kazi na zipo ambazo kuwa zimeshakufa. Kwanza kimandhani ya bandari inatoa  haiba yake. Kwa sababu uingiaji wa meli pale anapotokezea mgeni huwa anapata misuko suko sana. Siku za nyuma ilikuwa meli zikija wanatoka watu wetu wanakwenda kuzichukua na kuzitia kwenye gati. Zile meli nyingi zilizokuwepo pale ambazo hazifanyi kazi pia huwa zinasababisha usumbufu.

Mhe. Spika, nilikuwa nataka nimwombe Mheshimiwa labda patungwe kanuni iongezwe kwenye Mswada au itiwe kipengele kwamba meli yoyote ambayo haina kazi ya msingi au imeshakufa, basi iondoshwe kwa kutupwa mbali au kuzamishwa kuliko kukaa pale ambako kwanza inakera na inaleta hatari inaweza ikasababisha meli nyengine zinazokuja kasi zikagonga, zikaleta athari kwa wananchi wetu. Nashauri hili kama litakuwa la msingi, basi litafutiwe pahali kuwekwa kwamba kisheria bandari ikae meli ambayo nzima wakati wote inafanya kazi ikirudi inasubiri tani yake nyengine.

Mhe. Spika, suala jengine hivi sasa kumezuka mtindo wa meli zetu hizi *speed boat* kufukuzana. Mimi najua hufukuzana ni gari barabarani, lakini sio meli baharini au ngarawa kwenye resi ndio huwa zinafukuzana, maana huwekewa zawadi atakae fika mwanzo huwa atapata kiasi fulani. Kuna meli zina mtindo sasa hivi ambazo zinaleta dhara nyingi kwanza upotevu wa mizigo. Mimi mwenyewe binafsi mkasa huo umeshanikuta. Tumekwenda Pemba wakati wa mwezi wa Ramadhani wa mwaka huu kufanya kazi za Kamati za Baraza, nashukuru tumefanya vizuri, tumemaliza. Tunafika Mkoani kuna meli ya Sepide  na Sea Bus. Bahati mimi nilikata tiketi ya meli ya Express, lakini kutokana na  kishindo kile na mvurugano ule nikasema mkoba wangu nimuachie mchukuzi mimi niwahi kiti maana watu ni wengi.

Kwa bahati nikapata ngazi nikaingia ndani, lakini bahati mbaya sana nashuka mzigo haumo. Kutokana na kufukuzana kwa meli hawa wanashuka hawa wanaingia, matokeo yake mizigo ya Dar-es-Salaam ikashushwa Pemba wangu miye wa Unguja ukashushwa Dar-es-Salaam pakawa na vurugu kubwa, ingawa rizki ya mtu haipotei. Baada ya mwezi mmoja mizigo yangu nikaletewa nyumbani. Nashukuru, lakini wengine huwa hawaupati sijui wangu ulikuwa na

kago gani mpaka ukachukuliwa Dar-es-Salaam, ukaletwa hapa na nikaletewa nyumbani. Nadhani ni utaratibu mzuri tu. Na hili kama hatukuliwekea mkakati katika sheria yetu litatusumbua.

Mhe. Spika, kubwa zaidi hivi sasa kuna tatizo la upandaji wa nauli na kushuka. Natoa mifano iliyokuwa imeshanikuta mimi mwenyewe, raia wa nje hawezi kuja hapa akatoa mfano, wao wanatutuma sisi, lakini na sisi wenyewe pia huwa yanatukuta. Juzi nilikuwa Dar-es-Salaam, nimepanda Sepide asubuhi kuja huku na pale kuna nyengine Express inakujia huku, yule mwenzake kauza tiketi Sh. 15,000/= na mwengine kaweka tiketi Sh. 12,000/= wengi wamekimbia kwenye tiketi ya Sh. 15,000/= wamekuja kwenye tiketi ya Sh. 12,000/= ikaondoka meli moja ina watu wachache sana, lakini moja imejaza.

Mhe. Spika, katika wale wahudumu wa meli nikamuuliza huu ni utaratibu gani mnaotumia juu ya nauli. Akasema haiwezekani kama yeye kaweka Sh. 15,000/= mimi nitakuwa sipati wateja, kwa hivyo ni lazima nishushe bei ili niweze kupata abiria. Kuna siku unaweza ukaambiwa leo bei Sh. 18,000/=, sasa inakuwa kwanza unatuhangaisha na hatujui utaratibu uko vipi.

Naomba na hili kama litatiwa kwenye kanuni au kama itakuwa pahali gani, lakini tungependekeza bei itulie pahali pamoja, isiwe mtu ana uwezo wa kusema tu kwamba leo nataka Sh. 12,000/= , kesho Sh. 13,000/= itakuwa hiyo sio biashara, abiria wana wanawatesa na wananchi vile vile. Hili huwa linatokezea, naiomba wizara kupitia na wataalamu wake nauli iwekwe ya kudumu. Pale mafuta yameshuka wakishusha na sisi tutakuwa pamoja na pale mafuta yakipanda, wakipandisha tutakuwa pamoja, lakini leo mtu kwa utashi wake tu binafsi mwenzangu kaweka Sh. 15,000/= mimi nataka abiria wengi, basi niweke Sh. 10,000/= wanakuwa wanatushughulisha sana. Nadhani na hili litatusaidia uwekaji mzuri katika hali kama hiyo.

Mhe. Spika, jengine meli zetu nyingi zinazokuja hapa inakuwa kama magari ni *recondition* ambazo zinakuwa zimeshatumika muda mrefu. Hivi sasa, baadhi ya meli zimeshakuwa taabani na hakuna anayezisimamia. Utakuta mtu anatoka Dar-es-Salaam kwa masaa sita, meli inazima njiani kama gari, wakati ilikuwa ichukue masaa matatu tu. Gari hufunguliwa *bonnet* watu wakatizama huwa unaingia imani, lakini meli fundi humjui anaendea wapi, mtakaa mle kama mvuta sigari atavuta 3, 4, meli bado haijenda. Hili vile vile ningeshauri likatizamwa, ingewekwa kanuni au sheria kuhusiana na hili.

Mhe. Spika, gari za kawaida hata iwe mpya, lakini unapasisha kila mwaka, ili kujulikana kama nzima au ina matatizo. Halafu pia silva kati kati ya mwaka anakuja barabarani ana *block,* anasema leo ni ukaguzi wa magari. Na huwa anatoa matatizo na kama gari mbovu zinasimamishwa kutembea barabarani.

Sasa na meli kama tunaosajili sisi basi tungeweka taratibu kama mwaka mzima tunaikagua meli, haifai ipelekwe kupasishwa hawezi basi ifutiwe kibali. Au kati kati ya mwaka wana *block* wanaziangalia meli ziko katika hali gani. Hivi sasa hali mbaya, tusingoje mpaka ikawa kama wenzetu wa Bukoba, meli imezama ndio wametanabahi, hatuombi hivyo na sisi.

Mhe. Spika, nashauri na hili kama litawekwa kwenye kanuni au tutaipenyeza humu humu itasaidia sana kutupa imani kwenye vyombo tunavyopanda ambapo kila mmoja haifiki mwezi keshapanda katika chombo hicho. Naomba na hili Waziri kama kutakuwa na uwezo huo, basi tuweze kulitizama ili liweza kutusaidia.

Mwisho katika ushauri wangu halafu niende katika Mswada nipate ufafanuzi wa baadhi ya vifungu ambavyo sikuvifahamu. Ukipanda ndege kuna utaratibu unaulizwa kwamba huu mzigo utakuwa wa mkononi au utiwe kwenye kago. Unasema nitachukua mkononi na huu nitilie kwenye kago. Unafungwa stika na stika nyengine inabandikwa kwenye mzigo wako, ili kumaanisha kwamba ule mzigo kadiri unavyokwenda kama utapotea shirika litalipa.

Sasa kwa kuwa na hizi meli zetu ni za kileo, ni speed boat na zina sehemu ya mizigo na sehemu ya kukaa, tungeshauri na wao wakafanya kama utaratibu wa ndege, ili mzigo wako ukawa na uhakika, pesa yako ukaikusanya vizuri na wewe ukapanda vizuri na ukashuka vizuri. Unatiliwa stika yako na moja unakaa nayo mwenyewe ukishuka unakabidhiwa bila ya tatizo na ikitokea mzigo kupotea basi meli ilipe. Lakini leo mzigo ukipotea unaambiwa uzembe wako mwenyewe bwana, wakati yeye keshakusanya pesa yako na hiyo ndiyo inayomwendesha katika shughuli zake.

Naomba na hilo litizamwe na lifanyiwe kazi kama tutaweza kugeuza tukenda kama wenzetu mashirika ya ndege, nadhani itatusaidia wenye mizigo na wasafiri ili kuweza kusafiri kiusalama na mizigo yetu.

Mhe. Waziri baada ya hayo maoni yangu kijumla sasa naomba niingie kwenye Mswada kifungu baada ya kifungu.

Nije kwenye ufafanuzi kwenye utangulizi sehemu ya kwanza, tafsiri. Tafsiri sikuwa na mambo makubwa kuna jambo dogo sana ambalo nataka maelezo. Sehemu inayosema chombo baada ya neno “Rais” pale chini pana neno linasema “Chombo”. Kinasema,

Kifungu cha 2 ““Chombo” inajumuisha kila aina ya chombo cha majini pamoja na vyombo vya bapa na ndege za baharini zinazotumika au vyenye uwezo wa kusafirisha baharini;”

Sasa hili neno bapa nilitaka nijue chombo cha bapa ni kipi hicho. Mimi najua ngarawa ina shimo, mtumbwi una shimo, nataka nipewe ufafanuzi kama tunapanda kutembelea au bapa watu wanafurahishia tu wenyewe au vipi.

Ukurasa wa 199 kuna sehemu inayosema “Eneo la udhibiti la Mamlaka”.

Kifungu cha 4(1) “Mamlaka itatekeleza majukumu yake”

Kuna (a), (b) na (c) halafu kuna na namba za kirumi ya (vii) na (viii) ndio penye suala langu. Vyombo vya kienyeji na vyombo vidogo vidogo na vyombo vya kujifurahisha. Vyombo vidogo vidogo navifahamu, lakini nataka nijue hivi vyombo vya kienyeji ni vipi. Wakati ni vitu viwili tofauti na vyombo vya kujifurahishia. Pia nataka nipate ufafanuzi wake kwa sababu ingekuwa ipo huku kwenye tafsiri nisingepata tatizo kubwa. Nilikuwa naomba nijue hivyo vyombo vya kienyeji ni vipi na vyombo vya kujifurahishia ni vipi.

Ukurasa wa 200 sehemu ya (2) Majukumu ya Mamlaka. Kuna mambo yameorodheshwa (a), (b), (c), (d) - (o) naomba nisome ili nipate ufafanuzi.

Kifungu cha 5(1)(d) “Kusajili na kutoa leseni kwa meli za biashara kwa ajili ya kutimiza malengo ya kitaifa na kimataifa, kutoa uraia.Ushahidi wa umiliki na nyaraka za umiliki, kusajiri rehani na kuweka jina la chombo.”

Hili ndio lililonipa matatizo ambalo na mwenzangu alilizungumza kwamba uraia pia utatolewa na mamlaka hii. Sijui ni uraia upi huo. Kusajili rehani pia nayo nilikuwa nataka nijue baina ya uraia na rehani, ili niweze kufahamu. Ingelikuwa ipo kwenye ufafanuzi pia nisingepata matatizo.

Kifungu 5(1)(g) “Kufanya ukaguzi wa meli za kigeni kwa ajili ya kuimarisha usalama wa watu baharini, kinga na uchafuzi wa mazingira ya bahari na kuhakikisha kuwa maisha yana hali ya utendaji kazi melini ni salama kwa viwango vinavyokubalika:”

Sasa nilitaka kujua hii kinga itafanywa vipi ya uchafuzi wa bahari, kwa sababu imechanganywa ingekuwa ni sentensi mbili tofauti pia ningezidi kuelewa, lakini hii kinga ya mazingira ya bahari itafanywa vipi na Mamlaka.

Ukurasa wa 204 Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji hapa pana uteuzi wa bodi, mwenzangu kazungumza, lakini mimi kidogo nitakuwa tofauti na yeye. Mwenyekiti atateuliwa na Rais na mkurugenzi pia atateuliwa na Rais.

Walichotofautiana hapa mkurugenzi kapewa sifa nyingi awe nazo ndipo aweze kuteuliwa, lakini mwenyekiti hatukuona sifa yoyote. Nitaka kujua inakuwaje mmoja anatakiwa awe na sifa na mwengine asiwe na sifa. Nilitaka nipewa sababu za msingi nikiridhika sina tatizo.

Halafu wajumbe wa bodi nao pia hawakuainishwa ni wangapi kama 8 au 9 naomba na hii pia ingekuwa ni vizuri ikatambulishwa, kwamba wajumbe wa bodi wote ni 9, lakini 6 watateuliwa na waziri, 2 watateuliwa na Rais, hiyo inakuwa rahisi kufahamu.

Sehemu ya adhabu namba 211 hapa imewekwa adhabu kwa pesa za kigeni na wenzetu wengi hapa Tanzania au hapa Zanzibar huwa tunafanya kazi, lakini tunalipana kwa pesa zetu za Kitanzania. Ningeshauri basi kama inawezekana ingewekwa zote mbili kwa sababu leo anafanya kosa mtu wa jahazi, pengine kagonga boya na kashtakiwa unamwambia toa dola 50 yeye atazipata wapi na pesa zetu ni za Kitanzania. Sasa naomba bora tungetumia pesa zetu za hapa hapa kwa kuwa hii sheria haiwalengi wageni tu ni yetu sote. La kama ni ya kimataifa, basi ni vyema tukaandika kwa thamani ya fedha za kigeni basi naomba nipatiwe jibu na Mhe. Waziri. Lakini mapendekezo yangu tungeweka pesa kwa thamani ya pesa zetu za Tanzania.

Mhe. Spika, baada ya hayo niliyokwisha kueleza na maoni yangu binafsi pamoja na hayo niliyouliza kwenye sehemu ya Mswada, nadhani nisichukue muda mrefu nimshukuru waziri pamoja na serikali kwa kuleta Mswada huu. Mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini, baada ya kuwekwa sawa kisheria naunga mkono mia kwa mia. Pia, nawashauri wenzangu tuujadili na kuupitisha ili kuweza kuondosha matatizo ya usafiri wa baharini. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Abass Juma Muhunzi:** Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Labda nianze kwa kutanguliza maneno yale yale ya Kiongozi wa Upinzani aliyoyazungumza ya kwamba Mswada huu ungebidi kurejeshwa na kufanyiwa kazi upya. Ni maneno ambayo nayaunga mkono moja kwa moja na zaidi katika mchango wangu. Lakini pia nitaongeza na mengine ambayo pengine yataboresha zaidi.

Mhe. Spika, Mimi sikupita katika mfumo wa kisheria, mambo ambayo ameyazungumza pamoja na lile zito ambalo ukiyajumlisha pamoja yanaupeleka Mswada huu moja kwa moja kwamba urudi na ufanyiwe kazi upya. Sio, urudi na ufanyiwe kazi upya kwa maana kwamba tunaukataa, tunaukubali na tunataka tuukubali Mswada na tupitishe sheria ambayo ikishapita sheria hiyo kweli inaweza ikafanya kazi.

Mhe. Spika, maana haitokuwa busara ndani ya Baraza lako iwapo tutakaa na tutapitisha sheria, lakini ikaonekana sheria ile baadaye haiwezi kufanya kazi. Tulikwisha kufanya kosa hilo hapo awali kwa hivyo nadhani tusilirejee tena. Tulipopitisha sheria ya Nam. 5 ya mwaka 2006 ilikuwa ni sheria inayozingatia usimamizi, lakini ni sheria ambayo haikuweza kufanya kazi kwa sababu chombo chenye mamlaya ya kuisimamia sheria hiyo Nam.5 ya mwaka 2006, kilikuwa hakijapitishwa katika Baraza lako. Tulifanya kazi nzuri ya kupitisha jambo zuri, jambo ambalo halikuweza kufanya kazi hadi leo ambapo tunapitisha sheria ya kuitia nguvu.

Mhe. Spika, mambo mengine ambayo ni ya msingi na yanaongezea ule uzito wa hoja ya kwamba ipo haja ya Mswada huu wenzetu waufanyie tena kazi zaidi. Kwa mfano nikija katika Mswada huu kwenye utangulizi. Hapa kuna tafsiri ya maneno kwa mfano meli ya serikali, maana yake ni meli inayomilikiwa na inayotumiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini serikali katika tafsiri ya miswada yote miwili ni ile sheria Nam. 5 pamoja na hii sheria ambayo tunaizungumzia leo. Serikali iliyozungumziwa ilikuwa ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hivyo, sheria ilijikita kwa vyombo ambavyo vinaweza kumilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hapa leo pameingia na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Ni vyema kwetu sisi tukataka kuelewa zaidi uwezo wa sheria yetu tunaweza tukaitunga na tukawanayo na kuweza ku-*accommodate* mpaka vyombo vya meli vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Hilo la kwanza.

Mhe. Spika, kuna maelezo ya ukurasa huo huo wa 198 mwisho kabisa chini kuna neno ‘eneo la bahari la Zanzibar’. Maana yake ni eneo ambalo limo ndani ya mamlaka yaliyokuwa Jamhuri ya Zanzibar kabla ya Muungano mwaka 1964 baina ya Zanzibar na Tanganyika. Tulisikia kwenye hotuba ya mwenyekiti kwamba maneno haya sasa hivi yanafutwa ya eneo la bahari ya Zanzibar.

Mimi nimepigwa na mshangao kwa nini maneno haya yanafutwa? Yakifutwa maneno haya kifungu cha tano cha sheria hii ambacho ni 5(1)(c) “*to administer ships registered in Zanzibar and generally Superintend merchant shipping within Zanzibar maritime zone”*. Hapa imetajwa tena, maana tukifuta maneno haya hata na kifungu hiki hakina maana katika maelezo haya. Sioni sababu ya kufuta kifungu hiki kinachoelezea *maritime zone* kwa sababu hata katiba yetu sehemu ya kwanza eneo la Zanzibar ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba na visiwa vidogo vidogo vilivyozungukwa na bahari yake ambayo kabla ya Muungano ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

Ndani ya katiba tunayo maneno haya mazuri. Lakini ndani ya sheria yetu ambayo tunataka itupe nguvu ifanye kazi maneno haya yanafutwa. Mimi

nimeshindwa kufahamu ni kwa nini tunafuta maneno muhimu kama haya na kama tutayafuta haya, maana yake kwa kweli sheria yetu itakuwa haiwezi kufanya kazi.

Mhe. Spika, katika utangulizi hicho kilikuwa ni kifungu cha 2(1) lakini kifungu cha 2(2) kwa kuongeza maelezo ya kijifungu cha kwanza cha kitabu hiki kuna maelezo pale. Ukiangalia sheria hii kwa lugha ya Kiingereza inasema: "*in addition to the provision of subsection (1) of this section.* Narejea tena, *in addition to the provision of subsection (1) of this section.* Mimi nilipoiona tafsiri hii na huku anasema kwa kuongeza maelezo ya kifungu cha kwanza cha kifungu hiki kwa kweli tafsiri hapa imechafuliwa. Hapa inatoa sharti kwa kuongeza lakini huku *in addition* inatoa maelezo pamoja na kifungu cha kwanza ambacho kile tulichokizungumza. Kwa hivyo, nadhani hii ni *conflict* kubwa ya tafsiri kitu ambacho huwezi kusema maana yake si kwa kuondoshwa neno ni kwa kugeuzwa maneno *all together*. Mimi nafikiri *literal* tu labda ingelikuwa *by adding provision of subsection (1) of this section* ndio ingekuwa tafsiri ya maneno haya, kwa kuongeza maelezo ya kijifungu cha kwanza cha kifungu hiki na hiyo *by adding* isingekuwa na maana moja *in addition to*.

Mhe. Spika, kwa hivyo, lililozungumzwa na Mhe. Abubakar Khamis Bakary ni moja lakini inaonekana kwamba yako mengi ambayo wenzetu hawa wangeyafanyia kazi tungekuwa na jambo zuri zaidi.

Mhe. Spika, nikija katika kifungu cha 4 cha mswada huu na hii nadhani ni madhumuni. Uanzishwaji majukumu, uwezo na mamlaka. Madhumuni ya mswada sisi tumeyafahamu na hata sababu zake pia tumezifahamu, kwa kweli ni madhumuni yaliyo na maana kabisa na sababu zilizo nzuri lakini kwa sababu hata ukiutunga, madhumuni haya huwezi kuyafikia hapo ndipo tunapopata matatizo.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 4 mamlaka itatekeleza majukumu yake katika eneo la Zanzibar. Hapa kuna mambo yaliyotajwa kwa mfano 4(b)(iv) meli zinazoingia katika bandari yoyote ya Zanzibar, meli zinazopita katika maeneo ya Zanzibar, vyombo vya kujifurahishia na mambo kama hayo. Haya ni mambo mengi sana, hata kifungu cha 4 na 5 kwenye majukumu. Kifungu cha 5(1)(b) kuna masuala ambayo yamezungumzwa ya kuhusisha masuala ya kimataifa. Wenzangu wamesema kutoa uraia lakini hata haya malengo ya kitaifa na kimataifa. Sasa wasi wasi wangu ni ule ule kama wa wenzangu.

Mhe. Spika, hapa sisi tungependa sana nchi yetu iwe ni taifa. Kwa sababu ukiwa na taifa ndio unaweza ukajengeka hasa na ukatambulikana katika masuala haya ya kimataifa. Lakini kwa bahati mbaya utakapokuwa utaifa wako haupo, unalega lega au ni nusu nusu sisi unatutia hofu sana namna gani

tunaweza kujengeka katika masuala ya kimataifa na sheria zetu zikafanya kazi. Hapa mimi sitaki nitoneshe madonda, lakini bado suala la Zanzibar ambalo lilikuja likazungumzwa kuwa taifa au si taifa, Wazanzibari walinyamaza baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano kusema kwamba ndani ni taifa lakini nje si taifa. Wako watu ambao walipiga kofi wakaona ehee, leo Rais keshaweka sawa, Rais hakuweka sawa, Rais ndio alichafua zaidi. Kwa maana unapokuwa sasa hivi unaingia katika biashara hizi za meli na biashara za uchafuzi wa mazingira hizi ni shughuli ambazo zina nguvu zaidi katika sheria za kimataifa. Lakini vile vile tufikirie kwamba ndani ya utekelezaji wa shughuli hizi kutatokea migongano.

Kwa hivyo, wakati utakapokwenda kupeleka madai yako mara nyengine katika mahakama za kimataifa na kwa mambo ya meli nadhani mahakama za kimataifa ambazo zinashughulika na masuala ya meli ni lazima moja katika mambo ambayo yatazingatiwa ili uwe *competent* na kuweza kushughulikia masuala yako kimataifa ni kwamba wewe mwenyewe ni taifa? Ndio swali hilo. Meli tutakazoziruhusu zikapita ni meli ambazo zinamilikiwa na watu mbali mbali kwenye utaifa wao. Kuna siku sisi tutawafikiria wao ndio watafanya makosa na pia nafsi zetu hizi zitawabana. Lakini kuna siku sisi wenyewe tutafanya makosa kuzifanyia meli hizo. Tutakapokuwa tumepelekwa katika mashauri ya kisheria ya kimataifa tutayasimamia vipi masuala haya?

Mhe. Spika, hii haituzuii uwezo wa kupanga sheria zetu za ndani lakini inatufanya tutafakari zaidi namna sheria zetu tunavyoziunda zitakavyoweza kufanya kazi hasa kwa vile ndio Zanzibar tunaambiwa si taifa.

Mhe. Spika, mimi si mwanasheria lakini nilipokuwa nafanya *research* hii ya kuelezea nilikuta kesi na wenzangu watakaokuwa na *interest* nitawaambia ilipo. Kesi hii ilikuwa inahusu meli ya MV. Saiga, nimeipata katika mtandao www.it.los.oc. MV. Saiga ilikuwa imekuwa *registered* katika visiwa vya Saint Vincent na Grandies, meli hii ilikuwa inauza mafuta katika *coast* ya Guinea. Sasa siku ya tarehe 27 Oktoba, 1997 meli hii ilikuwa iko Guinea na siku ya pili yake ilikuwa imeruhusiwa kufanya kazi ya kuuza lakini katika *Guinea's Exclusive Economic Zones* basi, lakini kwa bahati mbaya siku ya pili yake ikaingia katika maji hasa ya Guinea. Kwa hivyo, *navy* wa Guinea wakaikamata meli hii na walipoikamata wakaizuia meli hii. Suala lililokuwepo katika meli hii wafanyakazi wake walikuwa ni Warusi, meli imesajiliwa Saint Vincent. Wamiliki wa meli hii walikuwa ni Kampuni moja wanaoitwa *Gabona Shipping Company* ya Nicosia Cyprus. *Management* ya meli hii ilikuwa inafanywa na kampuni moja inaitwa *See Cot Ship Management Limited* ya Glassgo na ilikuwa *under charter*. *Tullemania Shipping Group* ya Geneva.

Mhe. Spika, nilitaka nizungumze kesi hii ili wenzangu wafahamu namna ambavyo tutakapokuwa tuta-*deal* na meli, tusiichukulie tu kwamba ni meli hii imekuja kutoka Kenya ni meli ya Kenya. Lakini ina-*involve* mambo mengi sana, ina-*involve* mataifa mengi. Sasa Grenada walipeleka kesi *International Court of Justice,* wao hawakuwa na matatizo kwa sababu ni visiwa ambavyo vina utaifa wao. Kwa hivyo, *their competence* mwisho kesi hii namna ilivyohukumiwa kwa ufupi, kwa sababu kuna mambo mengi yalipita hapa ya *remedies* na sitaki nichukue muda kwa sababu nimekwishawambia wenzangu wapi nimeipata na wao watachukua *interest*. Lakini tarehe 13 Novemba, 1997 baada ya shauri hili kupelekwa katika *International Court of Justice* ya *Law of the Sea*, ili Guinea waiachie meli hiyo mara moja korti hiyo walitoa *order* tarehe 4 Disemba kuitaka Guinea iiachie meli hiyo. Lakini kulikuwa na *remedies* ambazo visiwa hivi dola laki nne itoe na kuna mambo mengi mengineyo.

Mhe. Spika, hapa kitu cha kuzingatia ni kwamba sio tu kuwa biashara ya meli ina-*involve* mataifa mengi, lakini pia biashara hii kuna pesa nyingi ambazo zinahitajika kuzilipa *in terms of remedies* wakati ambapo unaweza ukapatikana na matatizo. Kwa hivyo, sheria yetu hii ya Zanzibar tukiwa kama si taifa nje bila shaka tutakuwa tunaitegemea Tanzania iwe ndio *principal* wa kutusemea. Ni *mechanism* gani humu ya kifungu cha kisheria ambacho kinatoa uwezo moja kwa moja kwa masuala haya kuweza kushughulikiwa katika sheria hii. Kiko kifungu kilichozungumza hapa kutakuwa na mashirikiano nilikiona hapa lakini hakijitoshelezi, mashirikiano na vyombo vya Muungano katika masuala haya lakini imetaja katika mambo ya mafunzo peke yake hakuna jambo jengine. Jambo ninalolizungumzia hapa ni jambo lililo zito linalohusu uendeshaji, linalohusu mtafaruku wa makesi, linalohusu pesa nyingi ambazo unaweza ukashtakiwa na ukaambiwa mara moja uzilipe.

Mimi nilikuwa nasema sheria hii pamoja na uzuri wake tunaihitaji lakini tunaihitaji iweze kufanya kazi na tungeomba sana serikali wakaangalia tena ni sheria ipi au ni namna gani vyombo vya sheria vya kule vinavyohusiana na sheria hii moja kwa moja vinavyoweza kutoa nguvu au kuipa uwezo sheria hii ikawa katika utekelezaji wake. Hatupati matatizo hasa tunapokumbwa na masuala ya *peril of the sea* tukahitaji kwenda katika mahakama za kimataifa. Nilikuwa nasema hilo nililiona kama ni jambo muhimu ambalo kwa kweli hapa lilikuwa limekosekana.

Mhe. Spika, mimi napenda nimalizie kwa kusema hapa ndipo ninapokuja nikasema kwamba sasa hivi haya mambo tunayoyaona ni muhimu yanahitaji sana kutatuliwa kwa kuweka tafsiri bayana, mipaka yetu na Jamhuri ya Muungano ya Tanzania katika masuala haya ya kimataifa. Kwa kweli haitoshi tu pekee kusema Zanzibar ni taifa ndani lakini nje si taifa na sisi Wazanzibari

tukabakia tunapiga kofi, hata kidogo hatunufaiki. Kwa sababu nje sasa hivi ndio kwenye *opportunities* zinazohitajika kila nchi inakumba kuingia ndani.

Kuna jambo limetajwa hapa ni zito ambalo linahusu Baraza hili namna ambavyo tunaweza ku *ratify* miswada ya nje namna ambavyo imezungumzwa kusimamia usafiri, limenipotea lakini ndio hiyo ku *ratify*. Je, tayari tunao uwezo sisi kama Baraza? Kwa sababu *ratification* inafanyika ndani ya Mabunge na ndani ya Baraza haifanyiki kwenye serikali tu, lazima liwe *involve*. Ni kifungu kipi na wapi tutapata nguvu hizo, tutatunga sheria hii lakini tukawasubiri Bunge liende lika-*ratify* lichukue katika *process* zake au Bunge linaweza likakaa likasema Zanzibar kuna suala hili la msingi la muhimu na kuzingatia Bunge likae sasa kwenda kuingia katika mambo hayo. Kwa kweli tunaogelea katika bahari ambayo kina chake kitatuzamisha tu kuliko kuweza kuvuka.

Mhe. Spika, najua ipo nia nzuri sana ya kuifanya Zanzibar ijitegemee hasa katika masuala haya ya meli, lakini nia nzuri peke yake haifanyi kazi. Mhe. Spika, ni lazima tuelezwe ni kwa kiasi gani masuala ya Muungano ambayo yanaitwa kero mimi naita ni matatizo kwa sababu jambo la kuzuia kuwa huwezi kutunga sheria yako hilo si kero, hilo ni tatizo kubwa, ni kwa kiasi gani? Hili tu mimi sisemi hayo mengi, hayo yana muda wake tuyaachie lakini angalau hili la kuifanya sheria yetu tunayoitunga iweze kufanya kazi.

Mhe. Spika, mimi nilisoma tena kifungu kimoja nikaona kunazungumzwa mambo ya majanga. KMKM wana nafasi yao katika masuala haya ya kukamata kama ni vyombo, kuna *police marine* hapa, kuna tume ya majanga pia katika Afisi ya Waziri Kiongozi, na hapa vile vile ndani ya sheria hii kuna uwezo wa kushughulikia majanga. Tunataka tuone uhusiano mzuri sana uliopo na sehemu hizo lisitokee janga, tunataka tumkamate nani ikiwa kila mmoja anamrushia mwenzake mpira, ni KMKM, ilikuwa ni polisi, au ni nani. Kimo kifungu chengine humu cha sheria kinachosema kwamba sheria hii haiingilii sheria ya KMKM wala ya polisi wala vyombo gani vitu kama hivyo, haina uwezo huo wa kushughulikia vitu vya kiulinzi. Kwa hivyo, ni kwa kiasi gani sheria hii inaweza ikatupa uwezo wa kuitekeleza.

Mwisho kabisa ni suala la utaalamu. Mhe. Spika, jambo tunalolizungumza hapa ni jambo zito, ni fani nzito inayohitaji utaalamu mkubwa sana. Jana tulipokuwa tukizungumza Mswada wa kuanzisha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali alitupa *data* hapa akatwambia watu alionao wenye *master*, sijui wawili wana *PhD* akatutoa ule wasi wasi. Mimi napenda niulize sana katika wizara hii ni maofisa wangapi walio na shahada za *International Marine Laws* mbali ya wale wenye *shipping administration perse*. Hao ni watendaji lakini wale tunaoweza kuwapeleka wakenda

wakasimamia iwapo pametokea kesi ni wangapi tulionao Zanzibar na mawasiliano wanao wangapi? Kama hakuna, serikali imejitayarisha vipi au tunasubiri tupate tatizo twende tukamsumbue Mzee wetu Joseph Sinde Warioba kwa sababu nasikia yeye ndiye aliyebobea katika hayo mambo ya *marine.* Nadhani hatokuwa na nafasi.

Serikali inaweza ikaingia katika gharama kubwa sana ya kuwapata wanasheria hao wa kusimamia masuala hayo iwapo haikuchukua juhudi ya kuwa na watu hawa ndani ya wizara yake au ndani ya serikali. Ni jambo muhimu ambalo hilo nalo tungeelezwa angalau tukaweza kujua wamejitayarisha vipi au tunataka sheria ipelekwe tu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa sababu haya niliyoyazungumza wala sikwenda katika mswada wote mzima huko mbele sikwenda. Mswada huu umeletwa una nia nzuri na kitu kinachotaka kufanywa kizuri lakini naweza kusema kwa lugha ambayo wengine hawatoipenda ni *sub standard*. Kwa maana hiyo, mimi naunga mkono moja kwa moja yale maoni ya mwanzo ya Kiongozi wa Upinzani kwamba wenzetu wakae tena sisi tupo, Baraza lipo kuwafanyia kazi na tutaipitisha vile vile kama alivyosema ahadi ya mia kwa mia hata mia mbili kwa mia moja tutaweza kufika hapo. Baada ya kusema hayo nakushukuru sana Mhe. Spika.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi angalau nikapata kusema mawili matatu juu ya mswada huu. Kwanza Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru *Allah (SW)* kwa kutujaalia kuwa wazima kutuwezesha kukutana hapa leo katika Baraza lako tukufu kwa lengo la kuendeleza shughuli zetu za kila siku.

Pili nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliaono na Uchukuzi pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Maofisa mbali mbali kwa kuandaa mswada huu muhimu sana katika nchi yetu ya Zanzibar ambao tumekuwa tukiusubiri kwa hamu sana na kwa muda mrefu na zaidi ukitilia maanani kwamba visiwa vyetu hivi vya Zanzibar vimezungukwa na bahari na kuna matatizo mengi ambayo yanatokana na jambo hilo.

Mhe. Spika, kabla ya kuanza kuchangia nizungumzie hoja ambayo Mhe. Abubakar Khamis Bakary amewasilisha kwetu. Pamoja na kwamba mimi si mwanasheria lakini nimejaribu kuangalia angalia na kuona kwamba kuna tofauti juu ya maelezo yaliyokuwemo katika sheria hii na hii sheria ambayo imefutwa. Mimi tatizo langu halipo kama alivyoeleza yeye kitaalamu, lakini tatizo langu liko kwenye kifungu cha 5 cha Sheria ya Usafiri wa Baharini ya Mwaka 2006 kwa nini kikafutwa? Mimi ndiko niliko. Kwa sababu sijaona mantiki ya kufutwa kifungu hiki, kifungu cha 5 cha sheria hii kimempa Mhe.

Waziri anayeshughulika na masuala haya kuunda chombo ambacho kitasimamia usalama wa baharini. Hiyo sheria nambari 5 ambayo inafutwa ya mwaka 2006 imempa uwezo wa kuunda chombo, hapajaundwa chombo hapa isipokuwa imempa uwezo wa kuunda chombo. Sasa kwa mawazo yangu chombo kilichompa waziri kuunda ndio hii mamlaka ambayo sasa tunataka kuiunda kwa mawazo yangu ya kwamba si mwanasheria.

Kifungu cha 5 cha sheria ya mwaka 2006 kimempa uwezo Mhe. Waziri kuunda chombo cha kusimamia usalama baharini lakini chombo hakipo hakijaundwa, sasa tuko katika kuunda hicho chombo. Kwa hivyo, kifungu hiki hakikuwa na mantiki ya kufutwa kibakie kwa sababu ndicho kilichompa Mhe. Waziri uwezo wa kuunda chombo ambayo ni mamlaka hii tunayotaka kuipitisha sasa hivi. Mimi kwa mawazo yangu bado tunakwenda sawa lakini kifungu hiki kisiondoke kibakie. Baada ya maelezo hayo sasa niendelee na mchango wangu. Mhe. Spika, kama nilivyotangulia awali kwamba asilimia kubwa ya wananchi wa visiwa hivi vilivyozungukwa na bahari hutumia usafiri wa baharini. Kwa kweli, Mhe. Spika, kumekuwa na matatizo mengi, pamoja na kwamba matatizo haya yameweza kuchukuliwa hatua mbali mbali, lakini inaonekana bado yanakuwepo na yanakuwepo kutokana na kukosekana kwa taasisi kama hii au chombo kama hiki au mamlaka kama haya ambayo yanasimamia mambo hayo.

Mhe. Spika, kwa mfano kupanda kwa bei za nauli za abiria pamoja na mizigo. Mhe. Spika, kwa kweli hili ni tatizo la wananchi. Tumekuwa tukishuhudia uholela wa bei za vyombo vya baharini ama kutoka hapa kwenda Dar-es Salam au kutoka hapa kwenda Pemba. Wenye vyombo vya bahari wamekuwa wakijipangia bei wanavyotaka wenyewe. Leo utakwenda bei hii, na kesho utakwenda utakuta bei hii pamoja na kusema kwamba tuko katika biashara huria. Jambo hili kwa kweli linawapa usumbufu sana wananchi. Mwananchi anaweza kutoka na pesa yake akijua kwamba nauli ya usafiri kutoka hapa mpaka Pemba au Dar –es Salam ni kiasi gani, anapofika pahala pa kukatia tiketi anakuta pengine mara mbili zaidi ya ile bei iliyokuwepo. Mhe. Spika, kwa kweli hili limekuwa tatizo, lakini hata mizigo nayo imekuwa haina utaratibu maalum wa bei.

Mhe. Spika, kifungu cha 4, 1.6 cha sheria hii au cha mswada huu kimetaka mambo ambayo mamlaka hii ya usafiri wa baharini idhibiti ikiwepo nauli za abiria na mizigo. Lakini, pia itadhibiti ada na huduma za bandarini pamoja na kudhibiti nauli ya huduma za usafiri za bahari. Kwa hivyo, kama sheria hii itasimamiwa vizuri, kwa sababu kwa kweli tumekuwa na udhaifu wa kuzisimamia sheria zetu. Tumekuwa mahodari wa kutunga sheria, lakini tumekuwa na udhaifu wa kuzisimamia sheria zetu.

Sasa tunasema sheria hii itakuwa ipo, lakini kama ikipita na ikisimamiwa vizuri basi sisi tunaamini kwamba matatzio madogo madogo hasa ya nauli kwa wasafiri wetu yatapata kudhibitiwa. Hili lipo hata katika usafiri wa magari ya daladala na magari ya shamba, nako kumekuwa na matatizo kama hayo ambayo inaonekana nako hakuna udhibiti uliokuwa makini. Sasa hivi wananchi wetu wanalalamika bei ya mafuta imeshuka kutoka kule ilikokuwa. Lakini, bado bei za nauli za magari zinaonekana bado ziko pale pale. Sasa unafuu kwa wananchi wetu uko wapi?

Mhe. Spika, mafuta hapa sote tunashuhudia yalikuwa kwenye bei ya shilingi elfu moja mia nane na ushee kwa lita. Sasa hivi yamefika mpaka elfu moja na mia nne. Lakini bado bei za magari ziko pale pale. Inaonekana kwamba hakuna chombo ambacho kinasimamia kwa mujibu wa sheria. Lakini, leo ni faraja kuona kwamba Mhe. Waziri katuletea mswada huu ambao kutakuwa na chombo cha kusimamia mambo ya aina hii ya nauli na mambo mengine. Mhe. Waziri tunakushukuru kwa mswada huu.

Jengine Mhe. Spika, nilipokuwa naupitia mswada huu sehemu kwa sehemu nikaja katika sehemu ya ufafanuzi, kifungu cha 2 kuna maelezo kwa ruhusa yako naomba kunukuu:

> "Kwa kuongezea maelezo ya kijifungu cha (1) cha kifungu hichi. Endapo neno au maelezo yoyote yaliyotumika katika sheria hii yametafsiriwa katika Sheria ya Usafiri wa Baharini ya mwaka 2006 maneno au maelezo hayo, isipokuwa kama yataelezwa vyengine, yatakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usafiri wa Baharini ya mwaka 2006".

Sasa mimi kidogo hapa naona wenzetu wanafika pahala wanatuzonga, sijui wanatujua kuwa sisi si wanasheria. Kwa sababu sheria hii ya kuanzishwa kwa mamlaka ya kusimamia usafiri wa baharini kwa mujibu wa maelezo yaliokuwemo humu kwamba itasimamia utekelezaji wa sheria ile namba 5 ya mwaka 2006. Sheria hii ndio itakayosimamia ule utekelezaji wake.

Sasa kama kuna maneno yamekuwa yanapingana tafsiri zinapingana kwa nini kuwe na mpingano huo wakati sheria hizi zote zipo. Kwa nini tuyaweke sawa kabisa tukaongezewa kifungu kama hiki ambacho hakina msingi na sheria tunaweza kusema karibu yote ni sawa. Sheria hii imekuwa kwa kutekeleza ile pale.

Mhe. Spika, kwa mfano kama Mhe. Abass Juma Muhunzi alivyotoa maelezo nae kaona katika eneo hilo ambalo nimeliona linalozungumzia serikali. Serikali maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa mujibu wa sheria hii,

lakini meli ya Serikali maana yake ni Meli ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa kwa nini hapa tusiseme kwamba maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?. Sasa humu kwa kweli tunaona kidogo mnahitaji masawazisho.

Eneo jengine na mimi nilipenda kulitolea ufafanuzi hili eneo ambalo wenzetu wa kamati wamelitoa. Eneo la bahari la Zanzibar ambalo linasema maana yake ni:

> "Eneo ambalo limo ndani ya Mamlaka iliyokuwa ya Jamhuri ya Zanzibar kabla ya Muungano wa mwaka 1964 baina ya Zanzibar na Tangayika".

Mimi sijaona mantiki ya kutoa eneo hili. Kwa sababu sheria hii ina maeneo inayoyatawala ambayo itafanyiwa kazi. Sasa iwekwe kwa sababu humu mna sehemu imeelezewa kuwa kuna eneo inayoyatawala ambayo itafanyiwa kazi. Humu kuna ibara ambayo imeelezea hili eneo la Bahari za Zanzibar ambapo sheria hii itatumika kwa nini tuitoe.

Mhe. Spika, mimi wasi wasi wangu ambapo nahisi labda imepelekea kutolewa eneo hili kutokana na tafsiri ya Katiba iliyotoa tafsiri ya eneo la Tanzania ikamaanisha kwamba pamoja na visiwa vya Zanzibar na bahari yake labda ipo. Lakini ukiangalia bahari kwa mujibu wa katiba ni kitu cha Muungano, bahari si jambo la Muungano kabisa. Kwa hivyo, mimi sijaona mantiki ya kutolewa eneo hili ambalo linaonesha kwamba ni eneo ambalo litatumika na sheria hii itatawala. Mhe. Spika, bahari si kitu cha Muungano.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa sababu jambo hili limetolewa na Mwenyekiti wa Kamati. Sasa pengine labda atakuja kutupa nafasi kwa nini akafikia pahala akalitoa neno hili zuri tu ambalo linaainisha maeneo yetu ya kujidai ambapo sheria hii itatumika.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo ningependa nilizungumzie ni katika kifungu cha 3 cha mswada kifungu cha 3 (1) kinaelezea:

> " Kuanzishwa kwa mamlaka itakayojulikana kama Mamlaka ya Kusimamia Usalama Baharini Zanzibar kwa kifupi "*ZMA*".

Lakini katika kifungu kidogo cha 5 cha mswada huu kinazungumzia makujumu ya mamlaka. Majukumu hayo ya mamlaka katika kifungu cha 5 (1) (a) kwa jumla:

> “ Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usafiri wa Baharini. Nam. 5 ya mwaka 2006”

Katika kifungu cha 5 katika sheria namba 5 ya mwaka 2006 kilimpa Mhe. Waziri uwezo wa kuunda chombo kama cha kusimamia usafiri wa baharini kama maelezo yangu ya mwanzo ambayo yametangulia. Sasa kuna mambo mazuri humu kwa kweli katika sheria ile ya namba 5 ya mwaka 2006. Yamo mengi ambayo kwa kweli Mhe. Spika kama yatasimamiwa vizuri, basi wananchi watapata faraja sana na kwa sababu inaonekana kwamba haijaanza kufanyiwa kazi.

Katika sheria hiyo kifungu cha 57 (1,2) cha sheria namba 5 ya mwaka 2006, kinazungumzia masharti ya kukata Bima ambapo kila meli ya Tanzania Zanzibar itakuwa na Bima zidi ya hatari ya upoteaji au maafa. Lakini pia kila meli itakuwa na Bima kuhusiana na kila abiria aliepakiwa.

Mhe. Spika, kwa kweli hapa ni mahala pa maana sana tuwaombe sana wenzetu baada ya sheria hii kupita wasimamie sana jambo hili kwa sababu linaonekana halipo kabisa na utekelezaji wake unaonekana ni mzito. Sasa kama sheria hii itapita na mambo haya yatapitishwa, basi kwa upande wa wananchi wetu itakuwa ni faraja kwa sababu tutakuwa tunajua tunapanda vyombo tukiwa na usalama wa kutosha. Kutakuwa na ulinzi wa kutosha wa Bima na pale pahala ambapo patatokea masuala ya maafa, basi tunajua kuwa kutakuwa juu ya fidia ya mambo haya. Usimamizi wake ni mgumu mzito, lakini kwa kweli yatatusaidia sana.

Lakini, si masuala ya Bima tu, kuna masuala mbali mbali yanayohusu mabaharia na vyombo. Sheria hii namba 5 ya mwaka 2006, imebeba mambo mengi sana. Na mimi mara nyingi nilikuwa najiuliza huwa naipitia sana sheria hii. Nilikuwa sioni utekelezaji wake, kumbe mambo mazuri kama haya yanakuja ambayo kitaundwa chombo ambacho kitasimamia utekelezaji wa sheria hii. Kwa hivyo, tuwaombe tu wenzentu ambao watakuwa wamepewa mamlaka haya kwa mujibu wa sheria, basi watekeleze vizuri sheria hii. Lakini, wasi wasi wangu ni juu ya hao watalaamu ambao hata wenzetu wamekuwa na matatizo kama haya hata Mhe. Abass Juma Muhunzi alivyosema hao watu wenye utaalamu wa mambo ya bahari wapo? Kwa sababu kuna mambo ambayo yanahitaji wataalamu wa hali ya juu katika kusimamia. Kuna masuala ya ndani ya kimataifa. Kwa hivyo, yanahitaji utaalamu wa hali ya juu kuona kwamba yanasimamiwa ipasavyo.

Mhe. Spika, pia Mhe. Waziri ametuletea Sheria ya kusimamia chombo kama hiki. lakini bado kuna matatizo ya usafiri katika masuala ya Anga. Chombo cha aina hii inaonekana kuwa hakipo. Kwa hivyo, bado tunahitaji chombo cha

kusimamia usalama wa Anga kwa sababu nalo ni eneo muhimu ambalo wananchi tunasafiria, hasa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa taratibu zetu, tunakuwa tunatumia sana usafiri wa Anga. Tumekuwa na malalamiko mengi sana tumethubutu kukiondosha chombo kile ambacho tumekihisi si cha Muungano sijui kinaitwa *SUMATRA*. Huku tukitarajia tunasubiri chombo kama kile ambacho kitatusimamia na wao pia wamekuwa hawana utaratibu wa kuendesha shughuli zao.

Sisi kama Wajumbe tungetegemea chombo kama kile basi kiweze kuendeshwa kwa msingi ile ya kimataifa. Lakini kinaendeshwa kiholela, leo wewe umekwenda kukata tiketi ya ndege kwamba unasafiri saa 8 kwenda Dae –es Salaamu. Kwa bahati kukatokewa na dharura ya hafla unaahirisha, basi tiketi yako ile ukiipeleka siku nyengine kuitumia unaambiwa kuwa haifai unaambiwa kuwa imekwisha. Kweli ndio utaratibu wa kimataifa vitu kama vile.

Kwa hivyo, ni mambo ambayo kwa wenzetu kwenye usafiri wa ndege tunapambana nayo. Kwa hivyo, kwa kweli Mhe. Waziri tungemwomba sana baada ya kuunda chombo kama hiki cha kusimamia usafiri wa baharini, basi atuundie na chombo ambacho kitasimamia usafiri wa Anga ambacho kitaweza kusimamia na kudhibiti mambo mbali mbali, ikiwemo ubovu wa ndege. Kwa sababu ndege zetu mbovu tunazosafiria hasa zile tunazotoka nazo Unguja kwend Pemba hazifai, lakini tunapanda. Kwa hivyo, udhibiti ni lazima uwepo, sheria ni lazima itungwe ili kuona ndege zile tunazidhibiti.

Mhe. Spika, katika sheria hii nimeipitia nimeona Mkurugenzi Mkuu hakupewa kazi, isipokuwa katika kifungu cha 8 (4) cha mswada huu kimemtaja tu Mkurugenzi. Kinasema Mkurugenzi Mkuu awajibike kutekeleza masharti kama yatakavyoelezwa katika barua yake ya uteuzi. Mimi hiki hakijaniridhisha. Kama kazi zake zitajwe kwenye barua ya uteuzi. Mkurugenzi atateuliwa kwa mujibu wa sheria hii atateuliwa na Mhe. Rais. Sasa wakati anapomteuwa atamwelekeza na kazi zake.

Mimi nadhani si utaratibu nzuri na uzoefu unaonesha kwamba hapa tumekuwa tukipitisha miswada mingi. Utaratibu hauoneshi hivyo, udhoefu unaonesha kwamba Mkurugenzi anaeteuliwa katika ama Bodi ama Mamlaka au kitu chengine anakuwa anapangiwa kazi zake kwa mujibu wa sheria, na atakuwa anatekeleze kazi zake kwa mujibu wa sheria, sio atekeleze kazi kwa mujibu wa mtu aliemteua au maelekezo ya mtu aliemteua. Kwa hivyo, Mhe. Waziri pahali hapa panahitaji kuangaliwa, kuondosha matatizo, basi Mkurgenzi Mkuu huyu apewe kazi kwa mujibu wa sheria humu haioneshi. Ibara ya 11 imeeleza uwezo wake. Lakini hakuna eneo ambalo limeeleza kwamba Mkurugenzi atakuwa na kazi hii na hii katika mamlaka yetu. Kwa hivyo, nalo pia ningeomba Mhe. Waziri aliangalie na tupate ufafanuzi juu ya jambo hilo.

Eneo jengine Mhe. Spika, ni sehemu ya 3 ambayo inazungumzia Utawala na Uendeshaji wa Mamlaka. Ambapo kifungu cha 7 (1) cha sheria hii kinatueleza kwamba kutakuwa na Bodi wa Mkurugenzi wa Mamlaka ambayo kwa mujibu wa sheria hii itasimamia shughuli na maslahi ya mamlaka ambapo Mwenyekiti wa Bodi atateuliwa na Mhe. Rais.

Mimi sina mashaka juu ya eneo hili. Lakini mashaka yangu yapo katika kifungu cha 5 naomba kukinukuu:

> " Waziri kwa kushauriana na Bodi anaweza kwa kutoa tangazo katika gazeti rasmi la Serikali Kurekebisha, Kubadili, kuongeza na Kufuta au kuweka masharti mengine katika jaduweli la sheria hii".

Hapa mimi kidogo ndipo ninapo wasi wasi napo. Mimi naona kifungu hiki kimempa uwezo mkubwa sana Mhe. Waziri. Kwa sababu eneo la Jaduweli la Sheria hii ni sehemu ya sheria. Sasa kama sheria itampa uwezo Mhe. Waziri wa kubadilisha mambo ambayo yamepitishwa na Baraza hili nadhani tutakuwa tumempa uwezo mkubwa sana Mhe. Waziri, yeye mwenyewe tu akiamua kubadikisha jeduweli ilikuwemo mle ambayo tayari imeshapitishwa kwenye Baraza la Wawakilishi hapa, basi anatoa Gazeti la Serikali kumbe kurekebisha tu au sijui Gazeti hili litawasilishwa hapa Barazani sijaelewa. Kwa hivyo, nilikuwa nahitaji ufafanuzi juu ya jambo hili. Kwa vyovyote vile, ni lazima kuwe na mijadala juu ya jambo ambalo linahitaji kurekebishwa.

Jengine Mhe. Spika, kulikuwa kunahitaji mabadiliko tu ya vifungu viliomo kwenye mswada huu vimekuwa vimechanganywa mno. Kwa mfano kifungu cha 8 cha mswada kinazungumzia kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka atakaeteuliwa na Rais. Lakini kwa mtiririko mzima kifungu cha 11 baada ya kumalizika kifungu cha 8 kimeruka kimekuja kifungu cha 11 kuelezea uwezo wa Mkurugenzi Mkuu.

Sasa mimi kwa maoni yangu Mhe. Waziri baada ya kumaliza kifungu cha 7 kuelezea muundo wa Bodi, basi hiki kifungu cha 10 ambacho kinaelezea uwezo wa Bodi kifatie kiwe na kifungu cha 8 cha sheria hii ambapo baada ya kuunda Bodi inaelezwa uwezo wa Bodi. Lakini baada ya uwezo wa Bodi, basi kuwe na kifungu cha 10 kiwe kinazungumzia kuteuliwa kwa Mkurugenzi ambapo kifungu cha 11 kitazungumzia juu ya uwezo wa Mkurugenzi.

Nadhani hapo tutakuwa tumekwenda vizuri, kuliko kushika huku na kurudisha huku katika sheria hiyo hiyo, baada ya kuzungumzia jambo moja tukamaliza tumechukuwa hili na tunashika hili, tunaliacha kidogo itakuwa inatuletea mgongano. Tumeanza na Bodi tumalize Bodi, tuingie suala la Mkurugenzi, basi tukisha tunaendelea na sheria yetu.

Mhe. Spika, kifungu cha 17 cha sheria kifungu kidogo cha 2, kinachoelezea ambapo taratibu za uendeshaji wa shughuli za usalama. Sasa mamlaka wakati ikipitisha utaratibu wa endeshaji wa shughuli za Usalama kwa ajili ya meli za kampuni za ndani itazingatia kanuni za kimataifa za taratibu za uendeshaji wa shughuli za usalama.

Haya ni baadhi ya hofu ambazo mimi mwenyewe na baadhi ya wenzangu juu ya uwezo tuliokuwa nao katika masuala ya kimataifa katika sheria zetu. Kwa kweli, tunahitaji tuwe waangalifu sana na tuwe waangalifu kama walivyotangulia wenzengu kwamba nia yetu ni kuona kwamba tunaiweka nchi yetu katika hali nzuri ya kusimamia masuala mazima ya Bahari na mambo mengine.

Lakini kuna mambo kidogo yamenichanganya, kwa hivyo haya mambo yanahitaji kuangaliwa kwa umakini sana. Ili kuona kwamba sheria hii inatekelezwa ipasavyo. Lakini vyenginevyo Mhe. Spika, tutakuwa tunaunda sheria na hatimae tutakuwa sheria hazifanyi kazi hasa katika yale maeneo muhimu.

Mwisho Mhe. Spika, juu ya Muundo wa Bodi kwenye hii jaduweli ambapo kuna kitu kikubwa kimekosekana. Kitu hiki ambacho mara nyingi huwa tunakizungumzia juu ya ushirikishwaji wa Sekta binafsi ambapo mara nyingi tunakuwa tunasema kwamba tunawashirikisha.

Kwa hivyo, ningeomba sana na kwa kuwa mimi kamati yangu ndio inashughulika na Sekta hii ambayo inashughulikia masuala mengi wamekuwa na malalamiko mengi, kila tukikutana nao wamekuwa na malalamiko juu ya ushirikishwaji katika Bodi hizi mbali mbali na wao kuweza kutoa michango yao.

Sasa ningeomba sana Mhe. Waziri kwa hawa Wajumbe wako 5 ambao umepewa kisheria, basi umege wawili ili uzipe nafasi hizi sekta binafsi angalau nafasi mbili na wao wawemo katika huu muundo wa Bodi. Hawa watatusaidia kwa sababu hawa ndio wanao meli, wenye vyombo mbali mbali. Kwa hivyo, kuwaingia mle katika masuala mbali mbali yanayohusu uamuzi wa vyombo hivi itatusaidia, kwa sababu watakuwa na wao wenyewe wamo.

Mhe. Spika, juzi Mhe. Waziri wa Utalii alitualika kwenye semina fulani ambayo nadhani anataka kututayarishia mswada huko mbele, mambo ya utalii, lakini yuko katika utaratibu wa kuandaa mambo mazuri ambayo hatimae yatakuja hapa Barazani ili tuweze kuyapitisha kwa urahisi. Alivialika vyombo hivi wakati wa utayarishaji na kwa bahati nzuri nilipokutana na watu wa *Chamber of Commerce* walipokuwa wanalalamika juu ya ushirikishwaji,

nilipata nafasi ya kuwaambia kwamba tumekuwa na semina na watu wa *Chamber of Commerce* wanaoshughulika na mambo ya sekta ya utalii wameshirikishwa. Kwa bahati katika ule mkutano wa *chamber* walikuwemo ambao walishiriki katika semina ile. Kwa hivyo, wakawa hawana maneno kwa kuwa tayari ile taasisi ambayo wenyewe wanakuwa wanapiga kelele ilishirikishwa katika kuandaa. Kwa hivyo, hata watakapokuja kulalamika wakati wa utekelezaji wa sheria ile, basi wanakuwa hawana nguvu. Kwa hivyo, tuwashirikishe wenzetu hawa, ili kuona kwamba na wao wanakwenda vizuri.

Kwa sababu taasisi hizi za binafsi ni taasisi ambazo nazo ni wadau wa masuala ya uchumi katika nchi yetu, ni sehemu ya utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo. Kwa hivyo, namwomba Mhe. Waziri awaweke wajumbe wawili, ili wawemo katika bodi waweze kutusaidia katika mambo na ushauri mbali mbali kwa sababu wao ndio watekelezaji zaidi. Wao ndio wasimamizi, na wao ndio watakaokutana na kupanga katika utekelezaji mzuri wa sheria hii.

Mhe. Spika, kwa hayo machache, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni tunaunga mkono mswada huu upite kwa asilimia mia moja na hatimae kuwa ni sheria nzuri itakayoweza kutusaidia katika kuendeleza mbele suala zima la usafiri wa baharini. Ahsante.

**Mhe. Ame Ussi Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuchangia ingawa machache kwenye mswada huu. Nasema machache kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Spika, kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pili nakushukuru wewe na wajumbe waliochangia pia nawashukuru kwa maelezo yao ya kina. Mhe. Spika, pia nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuona suala hili muhimu kwamba na sisi nchi yetu inaweza ikafaidika hapo mbele baada ya mswada huu kupitishwa.

Mhe. Spika, moja kwa moja nije katika mswada. Mswada ni mzuri na umeletwa kipindi ambacho utatusaidia hapo mbele. Sisi wajumbe wa kamati tuliyaona haya na mengi katika mswada huu tulifanya marekebisho kama inavyoonekana kwenye *paper* ile, lakini kuna baadhi ya wajumbe hawakuipata ile *paper* ya marekebisho.

Mhe. Spika, Sehemu ya Pili kifungu cha 4 “Eneo la Udhibiti la Mamlaka”. Pamoja na kazi zote ambazo mamlaka itakuwa na majukumu kama yalivyotajwa kwenye sehemu mbali mbali za mswada ule, kuhusiana na vyombo vitakavyosajiliwa kwa sehemu mbali mbali, vyombo hivi vitakuwa vya mashirika na vyengine vya wananchi ambao wanaomiliki. Sasa hapa kwa kuangalia, basi mamlaka ya wananchi hawa wenye vyombo hivi, basi wapewe

elimu ya kutosha, kwani wao ndio watakuwa wamiliki wa vyombo hivi ili kuona nini kasoro au faida.
Mhe. Spika, nikiendelea pia katika kusimamia usalama wa vyombo vya uvuvi pamoja na vile ambavyo vilivyokuwa vinashughulika na biashara, basi mimi nashauri kwamba usimamizi uwe mzuri, ili kuona mamlaka inafanya kazi zake kama ni mamlaka.

Mhe. Spika, suala jengine ni meli zinazoingia bandarini kutoka nchi jirani au nje ya nchi. Kuwe na udhibiti mzuri ili kuona serikali jinsi inavyopata mapato yake kupitia sehemu ya bandari na usafiri. Pia, kuna meli ambazo zinapita maeneo ya Zanzibar ambapo kwa kawaida kila nchi ina maeneo yake kwa taratibu za kimataifa. Kwa hivyo, zile zinazopitia maeneo ya Zanzibar, basi nazo ziangaliwe. Kuwe na doria ambayo itasaidia ufanisi mkubwa wa uingiaji hata ule wa utokaji. Kwa sababu kuna meli nyengine zinaweza zikaja eneo la Zanzibar, zikaanza kufanya mambo maovu ya utupaji wa taka taka za kemikali au kuja kuvua eneo letu ambalo kwa hivi sasa ni ukanda mzuri tu kiutalii, na wananchi wetu wanafaidika na mazingira hayo. Kwa hivyo, kuwe na uangalifu mzuri wa doria hizo kuangalia jinsi meli zinavyoingia na zinavyofanya shughuli zake.

Mhe. Spika, Sehemu ya Tatu ya mswada huu kifungu cha 8 (3) naomba kunukuu:

Kifungu cha 8 (3):

> "Mkurugenzi Mkuu atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Mamlaka na atawajibika kwa bodi katika utekelezaji wa shughuli za kila siku za mamlaka, ikiwa ni pamoja na kutekeleza maagizo na maelekezo ya bodi."

Kwa kuwa ndiye mtendaji, kitu muhimu kinachotakiwa hapa huyu mtendaji pamoja na sifa zote zilizotajwa awe ni mkweli kwa sababu tayari anasimamia kazi za mamlaka. Kwa hivyo, huyu mtu awe mwaminifu, mwadilifu, akileta uzembe au vyenginevyo hiyo mamlaka itakuwa haitambuliki, itakuwa ni jina tu mamlaka, lakini taratibu zenyewe zitakuwa haziendi vizuri.

Pia, kuhusu kuzingatia huduma za biashara na usafiri wa baharini, mimi msisitizo wangu ni usimamizi mzuri, udhibiti mzuri wa mamlaka yote, itakuwa tayari imeweza kusimamia kazi hizo kwa ufanisi mzuri sana.

Mhe. Spika, kwa sababu nilisema sina mengi ila ni kutia nyama kidogo na kuboresha kwa kuwa ni Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Mimi

pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Nungwi tunaunga mkono mswada huu mia kwa mia. Ahsante sana.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Ahsante Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutuweka hapa tukajadili mambo yetu na mipango yetu ya kiuchumi. Pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii, ili kutoa mchango wangu ambao unaweza ukasaidia sana kuboresha katika kuunda mamlaka hii.

Mhe. Spika, ni siku nyingi tulikuwa tunataka baadhi ya mashirika yawe na mamlaka ili yapate kujiendesha. Mhe. Spika, kwa uzoefu kwanza tuone kwamba yapo mashirika ambayo kabla hayajawa mamlaka yakifanya kazi vizuri na tunayasifu. Kwa mfano, Shirika la Bandari ni katika mashirika ambayo yalionesha sura nzuri ya kuongezea uchumi wa nchi. Sasa inaundwa mamlaka sina wasi wasi, kwa mimi najua tu kwamba mamlaka itafanya kazi vizuri. Kwanza itakuwa na nafasi ya kuamua mambo yake wenyewe.

Lakini Mhe. Spika, katika hali ya usalama wa vyombo vya baharini yapo mambo mengi ambayo yanahitaji yaangaliwe vizuri. Ni mambo madogo madogo, lakini kwa mataifa yanakuwa kama ni sababu kubwa za kulalamika. Kwa mfano, minara. Minara ni njia ambazo zinaongozea vyombo na kuvipeleka salama vinakokwenda. Lakini mpaka mwaka juzi ilikuwa minara mingi sana taa haziwaki, sasa ni kosa kubwa kwa usalama wa vyombo vya bahari kuwa minara haifanyi kazi.

Lakini hata hivyo, tunaunda chombo sisi Wazanzibari kama chombo ambacho chetu na kitatoa wataalam na washiriki katika nchi yetu. Lakini nakumbuka kama minara ni sehemu ya Muungano, sisemi kwamba ni chombo cha Muungano. Kwa ile tafsiri yake siku niliyoipata nilihisi kama minara ni mambo ya pamoja. Kwa sababu minara matengenezo yake wanashiriki sana Shirika la Bandari na Mamlaka ya Bandari kule Bara. Mapato yake yanagaiwa nusu Tanzania Bara, nusu Tanzania Visiwani kwa utaratibu waliojiwekea.

Mhe. Spika, namwomba Mhe. Waziri atakapokuja anifafanulie. Baada ya kukamilika kupitisha mamlaka hii. Je, bado tutakuwa na utaratibu ule ule wa kutegemeana katika kutengeneza minara au tutakuwa na utaratibu mwengine. Kama bado tutakuwa na utaratibu ule ule na tunataka kusema kwamba eneo la bahari ya Zanzibar linataka kufutwa. Je, sisi tutahusika na mambo yepi ambayo yatakuwa ni matengenezo kama mamlaka ya Zanzibar itahusika. Naomba nije nipatiwe ufafanuzi.

Mhe. Spika, jengine tunataka kufanya usajili wa vyombo vya baharini. Unapofanya usajili unatakiwa uwe na utaalam wa kuona kwamba njia zipi

zinamhalalisha mwenye chombo, ili kisajiliwe na kiwe hakina matatizo. Kwa sababu katika usajili yapo mambo mengi yanahitajika ili unapopeleka kwenye usajili kuwe hakuna matatizo. Lakini si usajili tu, hata kupasisha vyombo kuna taratibu zake. Kwa mfano, huwezi kupasisha gari mpaka uipeleke gereji ikaangaliwe kila kitu, ukishakamilisha hayo ndipo hapo gari yako mpasishaji anaweza akaikubali. Sasa kwa vyombo ambavyo vimetajwa humu wapi wamiliki wanaweza wakapasisha vyombo vyao kabisa, kabla hawajapeleka kwenye usajili mpya.

Haidhuru tunacho chelezo hapa kwa sababu tunazungumzia zaidi mambo ya vyombo kama meli. Nilipokomea mwaka juzi chelezo kinaweza kinapandisha vyombo hata *size* ya kati. Kwa wakati ule Mkurugenzi wa Bandari alikuwa na mawazo ya kukiongeza chelezo kile kiwe kikubwa zaidi, ili kiwe kinakidhi haja kwa meli zote hasa za Zanzibar. Sijui kile chelezo kimeongezwa au bado kiko vile vile. Kama hakijaongezwa kutakuwa na utaratibu gani wa kuona kwamba kwa zile meli zinazohitaji kupandishwa na kufanyiwa marekebisho zinaweza zikashughulikiwa.

Mhe. Spika, jengine ukurasa wa 217 ambapo nimeshtushwa kidogo kwa Muundo wa Bodi. Katika bodi za kawaida hakuna sifa ambazo kubwa kama hizi zilizotajwa hapa. Labda kwa ruhusa yako Mhe. Spika, ninukuu katika jadweli Muundo na Mwenendo wa Bodi [Chini ya kifungu cha 7 (3)] naomba kunukuu:

Kifungu cha 1 (3):

"Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa mjumbe, isipokuwa awe na sifa zifuatazo:-

(a) awe mhitimu wa Chuo Kikuu kinachotambulika.

(b) awe na uzoefu usiopungua miaka mitano katika moja kati ya fani ya:

(i) sheria; au
(ii) mambo ya bahari; au
(iii) usimamizi wa usalama wa usafiri baharini."

Mhe. Spika, kwa bodi za hapa Zanzibar sijawahi kuiona bodi ambayo ina sifa zenye uzito kama hii. Pia, sifa hii inaweza kuwaweka watu wengi sana wa Zanzibar wasiwe wajumbe wa bodi. Sijui kitu gani kilichovutia mpaka wawe na sifa hizi. Kwa sababu nakumbuka kwenye Shirika la Bandari hawakutajwa watu wenye sifa hizi, lakini walifanya kazi vizuri sana na hata Mhe. Rais amesifu kwamba hakuna shirika lililofanya vizuri kama Shirika la Bandari.

Maana kwa wakati ule tuna Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Ali Suleiman Ali, wakati huo Mhe. Hamza hajawa waziri alikuwa mjumbe na mambo yalikwenda vizuri. Mhe. Ali Suleiman hana sifa hizi, lakini mjumbe. Sasa hapa Mhe. Spika, sijui kwa uzito gani uliopelekea kwamba lazima awe na sifa hizi.

Mhe. Spika, kifungu (b) bado nahisi masharti ya Mjumbe wa Bodi ni makubwa sana. Kwa hivyo, kwa kifungu hiki na hoja hizi ipo haja ya Mhe. Waziri kubadili maamuzi katika kifungu hiki kabla mswada haujapitishwa. Ni masharti makubwa sana na kwa Baraza hili nahisi sio wengi wanaoweza kufaa kuwa wajumbe. Kwa sababu wengi wao sifa hizi hawana. Sina hakika na sijui kitu gani hasa ambacho kinaweza kikalazimisha kwamba mjumbe awe na sifa hizi.

Mhe. Spika, jengine ni mambo ya usajili wa vyombo vidogo. Mhe. Spika, unapoweka taratibu za kituo kimoja tu katika usajili, basi unaweza ukawaletea usumbufu sana wenye vyombo, na Zanzibar tuna vyombo vingi. Ningependekeza kwamba kila penye bandari pakawa na utaratibu wa kukusanya maombi ya vyombo ambavyo vinataka kufanyiwa usajili. Lakini, kama tutataka usajili wa vyombo vyote viwe hapa mjini, basi tunaweza kuwasumbua sana wananchi. Zanzibar kuna vyombo vya bahari vingi sana vinafanana sana na gari. Sasa tunaona katika upasishaji wa gari watu wanapata tabu kweli, maana ukiwa Nungwi, Matemwe uje *ZRB*, ukiwa Michenzani haijambo utakwenda kwa miguu. Ukifika huko kuna usumbufu mkubwa kwa sababu utakuta foleni si ya kawaida. Kwa hivyo, lazima wakati mwengine tuone kwamba tunapotunga sheria tutoe maeneo ya kukasimu madaraka, ili watu wapate kufanya shughuli zao bila ya usumbufu.

Mhe. Spika, jengine katika mswada huu ni kifungu cha 23 (1) “Mwaka wa Fedha”. Kikawaida miaka ya fedha sisi tulivyoizoea ni ile ile kati ya mwezi wa 6 na mwezi wa 7. Lakini kwa utaratibu huu ambao umewekwa na bodi kwamba bajeti yao inaweza ikapitishwa wakati wowote kuwa mwaka wa fedha, inaweza kuwa tatizo. Kwa sababu mamlaka hii itakuwa ni sehemu ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Wizara hii kama zilivyo wizara nyengine inatakiwa mwaka wa fedha uwe mmoja, ili ripoti zipate kuripotiwa kwenye Baraza, lakini pia mkaguzi na mdhibiti wa mahesabu ya serikali awe na nafasi nzuri ya kuandika ripoti yake ambayo inaweza ikafaa kugawiwa katika Baraza. Sasa ningeomba wajitahidi sana kuona kwamba wanaharakisha katika mwaka huu wa fedha, ili uende sambamba na bajeti ya serikali.

Mhe. Spika, jengine katika mswada huu ni baadhi ya tafsiri. Katika tafsiri niliyoiona yapo maneno kama alivyozungumza Mhe. Ali Abdalla Ali kwamba Wazanzibari wengi na kwa vyombo vingi ambavyo vimetajwa, basi haiwezekani katika ufafanuzi tukatumia neno dola na hasa kwa vile dola hivi sasa inavyotishia. Juzi ilikuwa dola moja sawa sawa na shilingi elfu moja na

mia mbili, leo sijatazama soko, lakini inakaribia sawa sawa na elfu moja na mia nne na kitu.

Sasa Mhe. Spika, lazima tunapotunga sheria tuwe tunatafsiri kabisa kwamba yote yale thamani za pesa hasa ziwe kwa shilingi ya Tanzania kuliko kuitaja kwa dola, inapatisha tabu sana watumiaji hasa hawa ambao hawana miradi ya kupata dola ambao tunatumia shilingi za Tanzania.

Halafu pia jengine wanapata tabu sana watu wanapofika Mahakamani na kutafuta ile hesabu ya dola kwa shilingi. Kwa hivyo, naomba hii tuirekebishe mapema badala ya dola itumike shilingi.

Mhe. Spika, katika mswada huu mambo niliyotaka kuyachangia mengine yameshazungumzwa. Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Matemwe tunaunga mkono mswada huu mia juu ya mia. Ahsante.

*(Saa 6:50 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Waziri anayehusika yuko wapi. Mhe. Waziri Kiongozi teuwa mtu haraka afanye hiyo kazi kwa niaba yake. Kama hayupo tuondoke. *Chief* kama hayupo huyo mtu tuondoke. Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry atafanya hiyo kazi eeh! *ok.* Majadiliano yanaendelea.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk**: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii jioni ya leo kuweza kusaidia kuchangia mswada huu wa mamlaka. Mhe. Spika, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri, kwa kutuletea mswada huu kwa wakati muafaka sana.

Mhe. Spika, mimi nianze huko nyuma kwenye ukurasa wa 217. Kwanza Mhe. Waziri katika hii sehemu ya kifungu kinachoeleza habari ya kumpa mamlaka Mkurugenzi wa Mamlaka, halafu wajumbe wenyewe wa bodi. Kidogo hapa Mhe. Waziri apaangalie zaidi, kwa sababu historia yetu huko nyuma, bodi nyingi sana tumeshaziona, hazikuwa na sifa kama hizi zinazotakiwa humu ndani. Hii ni moja katika kumnyima fursa yule ambaye hana elimu ya kuweza kuingia katika bodi kwa mtazamo huu kama inavyoelezwa hapa kwenye mswada huu.

Mhe. Spika, kama utawaweka mafahari wawili, na wote wakawa na shahada za juu kama inavyoelezwa humu, basi wasi wasi wangu hapa kila mmoja atajiona

yeye anajua zaidi. Sasa kile ambacho kinataka kutekelezwa kwa jamii kitakosekana. Lakini wakiwepo baadhi ya watu wengine ambao hawana elimu kama hii, basi nafikiria hapa Mhe. Spika, patapatikana mambo mazuri sana, kwa sababu kuna wengine Mwenyezi Mungu kawajaalia hawana taaluma, lakini kawapa upeo wa kuzaliwa.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri pamoja na kuwa mswada huu ni mzito sana, basi akiangalie sana kifungu hiki, ili kuweza kusaidia wale ambao hawana taaluma na kuweza kuchaguliwa na wao wawe wajumbe wa bodi halali, kuweza kusaidia na kuunda sheria ambazo zitaweza kuwalinda hawa watu wetu wa mambo ya maboti na kadhalika.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Spika, kuundwa kwa mamlaka hii ambayo hivi sasa sote tunaiongelea vizuri sana, nina wasi wasi kwa baadhi ya mambo yasijeyakaharibika. Kwa sababu kama tulivyosema kuwa hapa kuna kifungu katika ukurasa wa 202, kwenye kifungu cha (bb) kwa ruhusa yako naomba kukisoma kidogo.

Kifungu cha 5(1)(z)(bb)

> " Kuhakikisha utekelezaji wa usimamizi wa mikataba yote iliyoridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania".

Mhe. Spika, hapa katika kifungu hiki, kidogo pananitia mashaka. Mhe. Abass Juma Muhunzi alieleza maneno mengi sana, tahadhari zilivyo. Sasa na mimi wasi wasi wangu uko hivi. Kwa sababu tunapounda chombo hiki, basi tukiangalie, mimi si mwanasheria, lakini wasi wasi wangu huko mbele huenda kukatokea jambo ambalo linaweza likanitetea mimi katika utaifa wangu, lakini hatimaye ikakuta mimi napata hasara. Chombo hiki tumeshasema tumeshakiunda Baraza la Wawakilishi limeshapitisha na Rais keshatia saini, hatimaye hizi haki tukaja tukakosa.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa utaratibu wa sheria kuwa bado tumo katika udhibiti wa Jamhuri ya Muungano, huo ndio wasi wasi wangu. Sasa labda Mhe. Waziri anisaidie zaidi tafsiri, kwa sababu kama tafsiri ni kila mtu anavyoifahamu hivyo, ndio maana mimi nikawa na wasi wasi mkubwa.

Kuna wasi wasi mwengine ambao naweza nikautoa Mhe. Spika, hivi karibuni kuna meli ilizama, mabaharia wetu Wazanzibari wakapoteza maisha. Kwa bahati nzuri meli ile nilisikia hivi karibuni ilizuiliwa kwa mujibu wa Mahakama, lakini sikufahamu imeishia vipi. Mawazo yangu yalinijia hivi, labda ile sheria ya ule utaifa wenyewe hatuna ndio maana ile ikaachiwa tu hivi hivi na haki za watu wetu hazijulikani zimekwenda wapi. Kwa hivyo,

tunapoamua jambo kama hili, basi tuangalie pande zote mbili zinaweza zikatusaidia.

Vile vile tunasema kuwa tutatoa leseni. Leseni hii nayo inanitia wasi wasi, kidogo Mhe. Waziri utanisaidia, kuwa hii leseni italingana na ule utaifa wenyewe au leseni hii itakuwa na mpaka maalum, tukivuka pale Chumbe ndio imekwisha leseni yetu tunaitia ndani ya mfuko. Pia, hili ningemuomba Mhe. Waziri hebu tuone ni jinsi gani tunaweza kusaidia hili.

Mhe. Spika, hivi karibuni kuna kampuni ambayo jina lake limenitoka kidogo, Mhe. Waziri atanisaidia kama hili suala kalifuatilia la kampuni ya kukusanya hawa mabaharia. Kwa kweli, hii kampuni inafanya kazi vizuri sana, lakini ndani yake sasa sielewi kama kuna taratibu ambazo zimekamilika kwa mujibu wa sheria. Kwa sababu wanatafuta wafanyakazi wa Kizanzibari na wa Kizalendo na kuwajaribu kama kweli wanawajaribu, au wanawafundisha yale mafunzo ya kibaharia ambayo yanatakiwa kwa mujibu wa taratibu za sheria hizo za kibaharia.

Vile vile huwakusanya hao na kuwapatia kazi huko nje, wengine hawarudi. Sasa sijui nayo hii sheria itawasaidia vipi kwenye mamlaka hii ambayo tunataka kuipitisha.

Mhe. Spika, hivi karibuni kuna meli moja, alikuwepo Mzanzibari ambaye alipata maradhi ya kifafa, akatumbukia baharini. Sasa, kwa kuwa labda Mhe. Waziri aliona umuhimu wa chombo kama hiki, ambacho kinaweza kikatafuta taarifa na kikaweza kueneza kwa mujibu wa utaratibu hata kwa wale wahusika ambao wanapata matatizo, ili waweze kujua haki zao zitapatikana vipi. Kama ni hivyo Mhe. Spika, basi tuwe waangalifu wazuri. Kwa sababu majanga tayari katika bahari yanatokea mengi sana na yanakuwa hayana usimamizi mzuri kama tunavyosema.

Halafu Mhe. Spika, kutokana na hali ya vyombo vidogo vidogo hivi, humu vimo, vyombo vya wavuvi. Mhe. Spika, hawa ni sawa sawa na samaki wadogo na papa kule baharini. Papa samaki. Sasa hawa mara nyingi sana wanagongwa hawa wenye ngarawa na hizi boti au meli, lakini utakuta mwisho wake hautambulikani, hawa watu kupewa fidia zao au kupatikana taarifa ambazo zinakubalika, watu wakafahamu kuwa sehemu fulani kuna ajali imetokezea ya boti kugonga ngarawa au hivi vimashua vyetu, na hii inatokezea mara nyingi sana.

Narudia tena, lakini kutokana na hali hii mamlaka yetu Mhe. Spika, itaweza kutusaidia na kuweza kuwaokoa hawa watu wetu, ili na wao wajisikie kuwa na wao katika hizi bahari wana sheria. Kama tulivyosema, kuwa watasajiliwa kwa

mujibu wa utaratibu. Huu usajili tangu zamani ulikuwepo, lakini labda kulikuwa na baadhi ya mambo hayasimamiwi vizuri, kwa sababu ngarawa ilikuwa ina usajili wake, ina jina lake na unapewa mpaka namba ya ngarawa na kituo chake kinachohusika. Lakini labda ni kutokana na usimamizi, kwa sababu tunaunda mambo mazuri usimamizi wake unakuwa mbovu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, suala hili mimi nalikubali moja kwa moja, lakini sasa usimamizi ukoje. Baada ya kuwa tumeikubali, tumeiridhia na tumeiunga mkono, basi naomba kabisa chombo husika kiwe madhubuti zaidi. Sio ijikumbe tu na kujisifia kina washauri wazuri, kina wasomi wazuri, lakini hatimaye ikaishia kwenye *briefcase*.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka niwe mchokozi tu kwa leo hii. Mhe. Spika, mimi naunga mkono, pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika. Kwanza kabisa kabla sijasema lolote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuchangia mswada huu muhimu, unaohusu juu ya kusimamia vyombo vya usafiri wa baharini Zanzibar na mambo mengineyo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, katika nchi yetu ya Zanzibar tumebahatika kwamba Zanzibar ni kisiwa ambacho kimezungukwa na bahari, kwa asilimia kubwa wananchi wake ni lazima watumie vyombo hivi vya usafiri wa baharini ili wafike kutoka sehemu moja na kwenda nyengine. Pia Mhe. Spika, nafasi kama hii huwa ni kama nyota kwa nchi kama hii kwa kuwa na vitu ambavyo ni vya uhakika na kusimamiwa vizuri, kwa ajili ya kuleta manusura kwa wananchi wetu wanaotumia vyombo hivyo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote, kwa kuleta mswada huu muhimu ambao naamini kwamba ukipita vizuri mswada huu na *Inshaallah* utapita, basi utafanya kazi zake vizuri na waliopewa mamlaka ya kusimamia shughuli hii watafanyakazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, mimi nafikiri tuwe wa wazi kabisa. Leo asubuhi katika Baraza hili katika swali la vyombo vya usafiri hasa magari, kwamba katika nchi zetu za Afrika Mashariki na Kati au nchi za SADC zimeweka utaratibu wa kuwa na namba za nchi yao. Kwa mfano Zanzibar tunatumia Z, ukenda Tanzania Bara wanatumia T, Ukenda Uganda wanatumia U, ukenda Rwanda wanatumia R na ukenda Burundi wanatumia B. Huo ni mwelekeo mmoja wapo wa kuhakikisha kwamba hili suala ni la halali kabisa na kuwa nalo katika nchi yetu ni haki yetu.

Mhe. Spika, Tanzania sisi tuna sehemu yetu na utaratibu wetu katika nchi yetu ya Zanzibar. Tukiangalia kwa hali halisi ilivyo, basi Zanzibar tunakuwa na jukumu kubwa zaidi kwa mamlaka hii kufanya kazi vizuri kuliko sehemu ya pili ya wenzetu. Pia kwa wenzetu Tanzania Bara, nao wana sehemu yao na ukenda nchi jirani ya Kenya, wana sehemu yao, ukenda Uganda, Ziwa Victoria wana sehemu yao.

Mhe. Spika, mimi nasema huu mswada ulioletwa, basi tuuwezeshe kuupa nguvu na tuuchangie vizuri, ili kuhakikisha kwamba mamlaka iliyoidhinishwa kufanya kazi zake, basi ifanyakazi zake kwa usalama wa wananchi wetu wa nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi nimeupitia mswada huu na una mambo mengi sana. Lakini mambo makubwa ambayo yanataka kushughulikiwa, ama kupewa nguvu zaidi ni mamlaka kupewa uwezo wa kuhakikisha kwamba inafanyakazi zake kwa mujibu wa sheria iliyowekwa nchini.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naamini Mhe. Waziri au wizara yetu nzima kwa kupitia kwa wataalamu wake aliokuwa nao Mhe. Waziri katika mamlaka hii na vyombo vyengine vya sheria, wamepitia sehemu mbali mbali na wamefuatilia taratibu mbali mbali, ili mswada utakapokuja hapa uwe hauna tatizo.

Mhe. Spika, katika kipindi kilichopita kama miaka miwili na nusu, mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, lakini pia nilikuwa Mwenyekiti kwa muda wote na mwaka wa nyuma yake pia nilikuwa Mwenyekiti, tulikuwa tunabadilishana mwaka hadi mwaka. Lakini niseme tu Mhe. Spika, hili suala la kero ni la muda mrefu.

Mhe. Spika, leo kuna vyombo vinafanyakazi hapa kwetu, yaani vimesajiliwa hapa Zanzibar au vilikuwa vinafanyakazi hapa Zanzibar au vinaishi hapa. Lakini utaratibu wake wote wa uangalizi wa vyombo vile ulikuwa haufanywi hapa, ulikuwa unafanywa kwa wenzetu Tanzania Bara. Hii yote ilitokana na kwamba hatuna mamlaka ambayo inahusika na kuhakikisha kwamba vyombo hivi vinaweza kufanyiwa ukaguzi hapa na kupata leseni halali ambayo inakubalika kitaifa na kimataifa, ili chombo kile kifanyekazi zake kwa maslahi ya watu wetu wanaosafiria vyombo vile.

Mhe. Spika, mswada huu umeeleza mambo mengi ambayo yanahusiana na vyombo mbali mbali. Kwa mfano meli zetu za serikali, meli za binafsi, kuna boti za kawaida, kuna ngarawa, kuna majahazi na hata ndege zetu ambazo wenzetu hawa wa utalii husafiria, yaani wanazifanya kama ndege halafu wanazifanya kama boti. Sijui wanaita jina gani, anajua yeye Mhe. Waziri na watendaji wake. Hili ni suala ambalo litatusaidia sana kuingiza mapato katika

nchi yetu na kuhakikisha kwamba mamlaka hii itakapofanya kazi zake, basi mapato yatakuwepo.

Mhe. Spika, mimi namshauri Mhe. Waziri, hili ni jukumu kubwa sana kwetu na tutakuwa na jukumu ambalo ni la kutunza usalama wa watu wetu. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri, tuwe na vitendea kazi ambavyo vitatusaidia katika utekelezaji wa kazi zetu.

Mhe. Spika, sheria ni sheria na mamlaka ikishakabidhiwa sheria ile, basi panatakiwa nyenzo za kufanyiakazi na nyenzo zinaanzia mambo mengi tu. Siku nyengine watendaji wa kazi zile wawe na vyombo vya usafiri. Kwa sababu inaweza kutokea haja wakati wowote, wakaambiwa waelekee Nungwi, majahazi ya Nungwi yanatakiwa yakakaguliwe huko huko. Mfano tu huo au waende Uroa, au Makunduchi, au Muyuni, au Mtambwe kwetu kwa babamkwe. Kwa hivyo, haya yote Mhe. Spika, ni lazima wenzetu hawa wawe na nyenzo ambazo wataweza kufanyia kazi zao kwa uangalifu na uadilifu mkubwa sana.

Mhe. Spika, naamini kutokana na shughuli hii muhimu na serikali kwa kuwa imeleta mswada huu, basi naamini itakuwa iko tayari. Lakini Mhe. Waziri atakuja kunijibu baadae kwa faida ya Baraza hili na wananchi wetu ambao wanaungojea kwa hamu mswada huu, ili kuhakikisha kwamba wanafanyakazi zao kama ilivyopangwa.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ni muhimu, ni kwamba tuhakikishe hawa wataalamu wetu kuanzia Mkurugenzi na watendaji wake wanapata mafunzo mbali mbali, au wanakwenda kujifunza kwa wenzetu japo kwa ujanja wowote waliokuwa nao, ili waone kwamba kumbe jambo hili ukifanya hivi na hivi unapata hiki.

Unajua Mhe. Spika, hakuna jambo zuri kama kuiga zuri, maana ukiona fulani kafanya jambo zuri ukasema na mimi nataka niliige lile zuri na nimshinde yeye, basi hapo ufanisi ndio unapatikana.

Mhe. Spika, nitowe mfano mwengine. Mhe. Spika, bandari yetu ya Zanzibar, pamoja na kuwa kwa muda mrefu bandari hii ilikuwa katika matengenezo, lakini wafanyabiashara wengi sana wanapenda kutumia bandari ya Zanzibar na watazidi kuipenda, kwa sababu Mwenyezi Mungu akipenda baada ya muda mfupi vitaingia vyombo vya kufanyia kazi, basi wafanyabiashara huko waliko watarudi hapa na wataleta mizigo yao iteremshwe hapa kwa usalama na kufanyakazi zao vizuri bila ya taathira yoyote.

Mhe. Spika, naweza kusema ninalolijua katika Baraza hili. Tanzania Bara pamoja na mtiririko mkubwa wa makontena yaliyokuwepo na vyombo vingi vilivyokuwepo pale vya kuteremsha mizigo, lakini bado kuna adha kubwa sana ukilinganisha na hapa kwetu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hivi vyombo vya usafiri baharini kwa kuwa vitakuwa na uwezo wa mamlaka hii kufanyakazi zake vizuri hapa Zanzibar, basi naamini Mhe. Spika, wenye vyombo wengi wataleta mizigo yao hapa, ili kupunguza urasimu uliokuwepo kwa wenzetu.

Mhe. Spika, namwambia Mhe. Waziri jambo zuri halitaki urasimu, jambo zuri linataka hapo kwa hapo lifanyiwe kazi, "linalowezekana leo lisingoje kesho" hapo ndio sifa itakuja ya utekelezaji mzuri katika kuhakikisha kwamba mamlaka inapata sifa na inafanyakazi zake na waliokuwepo Tanzania Bara, Tanga, Mtwara na kwengineko, basi wataomba waje hapa, ili wafanye kazi zao vizuri na kuondoa urasimu ambao wanaupata huko.

Mhe. Spika, tunatembea sehemu mbali mbali, tunawaona wenzetu, uaminifu ni jambo la mwanzo na uaminifu ni dhamana. Kwa hivyo, mimi naomba Mhe. Waziri uwe mkali sana kwa hawa wataalamu wetu. Nisije kwenda mimi kwa mlango wa pembeni nikasema aah! chombo changu wacha kiende kwa siku mbili au tatu, lakini baadae nitatengeneza. Huo si uadilifu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri uwe mkali sana, pakiwepo na usimamizi mzuri yaani chombo kikipasishwa kwa sheria na kukubalika kisheria, basi nakuhakikishia na wafanyabiashara wengine wataleta vyombo vyao hapa.

Mhe. Spika, naomba nitowe mfano mzuri tena wa uhai, katika wasafiri wetu ambao wanatumia vyombo vyetu. Hivi karibuni Mhe. Spika, palikuwa na patashika kubwa sana ya Shirika la Ndege la Tanzania (ATC) kusimamishwa. Limesimamishwa shirika, sio kwa sababu ndege mbovu, lilisimamishwa kwa kukosa sifa ambapo kulikuwa na shahada fulani hawajatimiza. Mimi niliipongeza sana serikali kwa kuona kwamba pamoja na kuwa shirika hili ni la serikali, lakini linasaidia wananchi wote wa Tanzania na wengineo, ili waende salama na zile sifa zao zinakubalika zikisomeka. Kwa hivyo, na sisi tuwe kama hivyo, nakuomba sana Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, naamini katika masuala mbali mbali tuliyokuwanayo, basi naamini mamlaka itakuwa na uwezo wa kuongoza kiutaratibu, hasa tukizingatia bodi ndio kitu cha mwanzo ambacho kinasimamia na kinashughulikia kwa uhakika kazi zake na taarifa zake zote hutakiwa Mhe. Waziri azipate ili kufanikisha shughuli zao.

Mhe. Spika, nadhani wenzangu wengi walizungumzia suala la Mwenyekiti wa Bodi. Mimi naomba tu kwamba tuna watu wengi wataalamu, tuna watu wengi wenye fani za ubaharia na tuna watu wengi wenye fani za vyombo vyetu vya

usafiri baharini. Kwa hivyo, mimi nafikiri ridhaa hiyo isilazimishe kuwa lazima awe na kitu fulani kikubwa. Kwa sababu Mhe. Spika, tunaweza kuwa na mtu *professor* hapa, au *doctor*, lakini siku nyengine kwa bahati mbaya akaja mtaalamu wa kawaida tu akam-*challenge professor or doctor*.

Mimi naomba Mhe. Spika, tuangalie uwezo wa mtu, tuangalie sifa za mtu na tuangalie uhodari au kwa Kiswahili fasaha utundu. Kwa sababu Mhe. Spika, kuna watu wabunifu sana humu. Mimi kuna kitu kimoja Mhe. Spika, labda nikitolee ufafanuzi, hii ni ya kweli hasa mheshimiwa. Palitokea shughuli, kwenye shughuli hiyo taa zikaleta matatizo katika sehemu ile pakawa na patashika kubwa sana. Wataalamu wa pale walikuwa ni wageni kutoka nje ya Tanzania wazungu. Unajua mzungu Mhe. Spika, ndiye anayeaminika sana, sijui kwa nini, kuna kitu ambacho hatukifahamu katika nafsi zetu, kumbe mzungu yule yule unaweza kumfanyia jambo akakushangaa.

Mhe. Spika, taa zile zikazimika, ikabidi aitwe mtaalamu, akashughulika pale huku jasho linamtoka mzungu. Palikuwa na jamaa mmoja kakaa pembeni anamuangalia tu yule mzungu. Baadae yule jamaa alipomuona yule mzungu taabani anafuta jasho, akamwendea akamwambia pumzika. Kenda kukichukua ki-*switch*, maana hata sijui ni cha aina gani, sekunde tu umeme unawaka, basi yule mzungu aliondoka kidogo kidogo akenda zake pembeni kutafuta vitabu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, utaalamu wa watu wetu nao unasaidia. Mimi naamini elimu ni jambo la msingi kabisa, lakini na utaalamu wa mtu binafsi pia uangaliwe. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hapa paangaliwe, ili kuhakikisha kwamba mtu yeyote anaweza kuwa mtaalamu kutokana na shughuli ambayo ana fani nayo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka kulizungumza ni kwamba, hapa kwetu kama nilivyozungumza mapema tu, tuna bandari nyingi. Kama tutakuwa na jambo la urahisi kwa kazi zetu, kama nilivyotangulia kusema mwanzo, basi tusing'ang'anie tu kuwa na bandari ya makao makuu tu hapa. Vyombo vyote vile japo hata vidogo, basi viletwe hapa. Ndio nikasema Mhe. Waziri ajitahidi sana, ili kuhakikisha kwamba anapata nyenzo kama usafiri na mambo mengineo, ili zile bandari ndogo kule Nungwi, Mkokotoni, kule nilikosema kwa babamkwe Mtambwe na Wesha na kila pahala palipokuwa na bandari zetu ndogo ndogo, basi tuzithamini. Kama tutafuatilia kikamilifu, basi mapato yatakuwa makubwa sana katika nchi yetu. Lakini tukiwapa mwanya, tukasema tungojee waje hapa, hawaji.

Marehemu Mzee Karume alisema neno moja silisahau wakati huo bado nasoma. Alisema Zanzibar nataka kuifanya nchi ya maendeleo ya kileo, hata aliyekuweko kijijini, basi ajione yuko mjini. Kweli kajitahidi sana

mheshimiwa, maana tunaona mambo mengi tu. Kubwa alisema neno moja ambalo sitalisahau maisha yangu, pamoja na juhudi zote tutakazozifanya, mfano umeme na majumba yafike kila mwahala Bambi na kwengineko, lakini biashara itakufuateni huku huku badala ya wewe kuifuatia mjini.

Waheshimiwa Wajumbe nafikiri sote ni mashuhuda sasa hivi, huo ni ukweli uliokuwa wazi. Honda kwa honda zinabeba mizigo zinapeleka vijijini. Ukenda Mkanyageni kwa Mhe. Haji Faki Shaali, ukenda Nungwi, ukenda Uroa na Pujini, mote unakuta watu wanahangaika. Hayo ndio maisha mheshimiwa. Ndio maana nikasema kwamba lazima na sisi wataalamu wetu wawe wanafuatilia kule kule, ili kuhakikisha kwamba wanawafanyia vitisho, lakini ni vitisho kwa ajili ya usalama wa watu wetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache. Nasema kwamba mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani, mswada huu nimeukubali kwa asilimia mia moja. Nawaomba na wenzangu tuuchangie kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake, ili wananchi wetu wajuwe kwamba vyombo vyetu vinapokaguliwa na wanapopata usafiri wa usalama, basi hiyo ndio hatima ya watu wetu juu ya maisha yao kuwa mazuri na ya uhakika. Baada ya hayo nasema ahsante na naunga mkono.

**Mhe. Ali Denge Makame:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Baharini hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuchangia mswada huu ambapo umekuja kwa wakati muafaka, ambao hata wadau wetu huko nje tokea kuanza kwa mswada huu wamejumuika kutusikiliza tunavyouchangia. Kwa hivyo, nawapongeza Mhe. Waziri pamoja na kamati yake iliyoandaa mswada huu na kutuletea hapa ili kupata kuujadili.

Mhe. Spika, kwa kweli tumekuwa na matatizo kwa kipindi kirefu kulingana na masuala mbali mbali ya baharini na vyombo vyetu hivi vya usafiri. Mhe. Spika, mara nyingi kumekuwa na masikitiko kwa wananchi wetu wengi, pindi wanaposafiri kwenye vyombo hivi vinakuwa havina msimamo wa kutosha kwenye bei ya nauli, mambo ya utunzaji wa mizigo yao. Kwa hivyo, kama itaundwa mamlaka hii kwa ajili ya kusimamia shughuli zote za upakizi wa abiria pamoja na mizigo yao, suala hili litaleta faraja kwa wananchi wetu. Kwa hivyo, ninampongeza Mhe. Waziri kwa kuuleta mswada huu ambao tutaweza kupiga hatua nyengine mbele kwa masuala ya bandari pamoja na usafiri wa baharini kwa ujumla.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 205 kifungu cha 12, kinachozungumzia kuhusu kuunda tume ya kufanya uchunguzi wa ajali. Suala hili kama hapo nyuma lilikuwepo basi liendelezwe na liekewe mikakati ya nguvu. Kwa sababu masuala ya ajali katika vyombo vyetu vya baharini mara nyingi zinatokezea.

Kwa mfano, mtu ameanguka kwenye bahari katoka kwenye meli au jahazi imezama, meli imetoboka. Kwa maana hiyo, akiunda tume hii ya uchunguzi wa ajali, itasaidia na kuweza kuepusha masuala haya ya ajali yanayotokezea katika visiwa vyetu. Kama tunavyofahamu wakaazi wengi wa visiwa hivi shughuli zao nyingi ni za baharini, kama vile uvuvi na hata safari zao nyingi huwa wanatumia meli, boti kwa ajili ya kutoka sehemu moja kwenda nyengine.

Mhe. Spika, wizara hii itakapoanzisha mamlaka haya kwa ajili ya kusimamia masuala ya ajali, hali hii itasaidia sana kwa sababu tumepoteza watu wetu wengi sana. Kwa mfano, haifiki miezi miwili au mitatu tunaweza kusikia watu wamezama na boti za uvuvi, wakati mwengine meli imegonga majahazi.

Kwa hivyo, kuna mambo mengi ambayo yanatokea baharini kwa ukosefu wa kuwepo mamlaka hii. Kwa maana hiyo, kama itakuwepo Mamlaka itaweza kusaidia kupunguza pamoja na kuliondosha tatizo hili ambalo linatokezea mara kwa mara.

Mhe. Spika, ninaiomba Mamlaka itakapoundwa kwa baadhi ya vifaa itakuwa vichache kwa ajili ya kufanyia doria ya usalama pamoja na kuangalia matokeo mbali mbali yanayotokea baharini, ni vyema kushirikiana na vikosi vyetu. Kwa sababu tuna baadhi ya vikosi vyetu wana vifaa vya kutosha. Kwa mfano, Jeshi la Wananchi wa Tanzani, Jeshi la Polisi na vyengine wana vifaa vingi kama vile *helicopter*, boti kubwa za kuweza kutafutia baadhi matukio kama haya ya ajali kwa ajili ya kuwaokoa wale waliopata ajali.
Kwa hivyo, ninaiomba Mamlaka ikashirikiana na vikosi hivyo pindipo itakuwa na upungufu wa vifaa ili kuweza kufanya doria ya kutafuta yale matokeo ya ajali yaliyotokezea. Mara nyingi ajali hapa kwetu kama inavyoeleweka huwa zinatokea sana kwa kipindi cha Kaskazi au kipindi cha Kusi na hata wakati mwengine kipindi cha mvua za Masika huwa zinatokea ajali kama hizi.

Kwa hivyo, pindipo ikiundwa Mamlaka na ikiwa imeshajiweka tayari na vifaa vyao hivyo. Napenda kutoa maoni yangu kuwa kila inapofika misimu kama ile ya upepo mkali wa Kaskazi wakawa tayari kwa ajili ya kufanya doria ya kupita kwenye maeneo ya bahari, ili kuangalia nani kazidiwa na chombo chake au kumetokea maafa gani ili kuweze kufanya uokozi.

Mhe. Spika, suala hili naliomba pindipo litakapoanza, Mamlaka wajiweke tayari kwa masuala kama hayo ili kukinga ajali mbali mbali zinazotokezea. Kama inavyoeleweka baadhi ya ajali zinapotokea huwa zinaathiri watu wengi na kusababisha kuleta ukali wa maisha. Kwa maana hiyo, tukijiandaa kwa kuunda vyombo kama hivyo na kuvitayarisha utapunguza ule ukali wa maisha kwa wananchi wetu. Leo katika familia kuondokewa na mtu mmoja tu ni pengo kubwa. Kwa hivyo, pindipotukijiweka tayari kwa masuala haya tutawapa faraja wananchi wetu.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nizungumzie kwenye ukurasa wa 206 kifungu cha 14 kuhusu umwagaji wa taka baharini Zanzibar. Suala hili kwa kweli linatokezea sana na mara nyingi huwa linatokezea katika ukanda wa Magharibi kuanzia Nungwi mpaka kufikia Makunduchi, kesi hizo ndio nyingi za kutupwa *chemicals* za sumu au taka nyengine mbali mbali.

Taka hizo mara nyingi baada ya maji kuja ufukweni huwa zinakumbwa mpaka kwenye maeneo yanayokaa watu na baadhi ya watu wengi huwa wanaathirika na taka hizo. Kwa mfano, huwa vinatupwa vitu vingi kwa sababu wakati mwengine huwa zinapita meli nyengine za kubeba silaha wakizidiwa na mkondo wa maji huwa baadhi ya mizigo wanaipunguza.

Kwa hivyo, katika kupunguza ile inaelea mpaka inakuja mpaka kwenye vijiji vyetu. Kwa maana hiyo, kwa makusudi watoto au watu wasiojua watakuwa wakichezea vitu vile na kusababisha hasara pamoja na hatari kwa wale wakaazi wa maeneo yale.

Kwa mfano, taka zile zinazotupwa nyingi wakati maji yanapokupwa huwa zinaishia vijijini wanakoishi watu. Mhe. Spika, kama itakuwepo Mamlaka hii na kupewa nyenzo pamoja na vifaa mbali mbali vya kufanya doria, ili kuangalia masuala haya yasitokezee, tunaweza kuepusha maafa kutokana na ajali zinazotokezea.

Kama nilivyozungumza mwanzo kwamba washirikiane kuomba au kuazima vifaa pale inapotokezea haja kubwa, ili kuweza kufanya doria na kuziangalia meli zinazofanya uchafuzi wa mazingira kama vile kutupa vifaa visivyostahili na kuweza kuchukuliwa hatua zinazostahili.

Mhe. Spika, kama tunavyofahamu kwamba maeneo mengi ya visiwa vyetu hivi vina milango au bandari za kuegesha meli ama vyombo vidogo ambavyo havijasajiliwa, ili kukimbiza mapato yanayostahili ya kuipatia Mamlaka au serikali kwa jumla ili kufanikisha mipango yake ya maendeleo.

Kwa hivyo, kama nilivyoshauri ikiwa itapata ushirikiano na taasisi nyengine ili kuweza kupata vyombo vya kufanyia doria kwa ajili ya kuzuia kwenye milango hii kwa wale waliokuwa wakipita kwa njia ya kienyeji na kuweza kuwafichua, ili kupata mapato na kuyapeleka taasisi husika na nia ya kuleta maendeleo katika serikali yetu.

Nikiondoka hapo sasa niende kwenye ukurasa wa 207 kifungu cha 18 kinachozungumzia mtu yeyote ikijumuisha chombo binafsi atalazimika kufanya shughuli ya utafutaji na uokozi. Mhe. Spika, suala hili kwa kweli naliona ni gumu kidogo kwa sababu kumwambia mtu binafsi afanye shughuli ya uokozi au utafutaji wa matokeo mbali mbali yanayotokea katika bahari. Labda mtu ajue kuwa ni katika familia au mtu wake ndio ametokezewa na ajali kwenye chombo fulani, kwa hivyo si rahisi kwa mtu binafsi kumwambia akatafute.

Mhe. Spika, ninaiomba Mamlaka hii ikajipanga kama ilivyokusudia kujipanga, pindipo yanapotokezea matatizo hayo na wakipewa taarifa basi watangaze ili watu binafsi pamoja na wanaohusika washirikiane katika suala la utafutaji na uokozi kwenye ajali hiyo iliyotokezea.

Vile vile iwaelimishe zaidi wananchi wetu katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu, ili pale inapotokezea ajali waweze kutoa taarifa kwa Mamlaka hii na mamlaka iweze kuwasiliana na vyombo vinavyohusika, kwa ajili ya kufanya kazi ya utafutaji na uokozi wa majanga yale yaliyotokezea.
Mhe. Spika, ukurasa wa 303 kifungu cha 6 (4) kinachozungumzia kuhusu suala la udhibiti wa ajira ya mabaharia na kuweka kanuni za ustawi wa mabaharia. Katika kifungu hiki sijafahamu uzuri, udhibiti wa ajira ya mabaharia, kwa maana mabaharia waliopo ndio basi wasiajiriwe wengine au kudhibiti kwa namna gani.

Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anieleze vizuri ili nipate kufahamu. Kwa sababu kama kudhibiti kwa mabaharia kwa wale waliokuwepo wasiajiriwe wengine, suala hili litaleta athari kwa vijana wetu au wananchi wetu wa Zanzibar. Kama tunavyofahamu kwamba vijana wetu wengi kazi hizi za ubaharia wanazipenda sana. Kwa hivyo, kama zitakuwepo ajira za ubaharia na ikiwa kuna taasisi au chuo cha kuwasomesha, wanakuwa tayari wakati wote kujitokeza kwa ajili ya kujiunga na masuala haya ya ubaharia.

Mhe. Waziri ikiwa utaanzisha mamlaka hii, ninaomba uangalie zaidi kama kuna taasisi au chuo maalum cha mabaharia, ili vijana wetu waweze kusomea shughuli hizi za ubaharia na kuweza kufanya kazi yao kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu sasa niingie kwenye ukurasa wa 203 kuhusu kifungu kinachozungumzia uwezo wa mamlaka. Naomba kununukuu kifungu 6 (b).

Kifungu 6 (b) kinachosema hivi:

> "Kuweka viwango vya usalama na kanuni za kufuatwa kwa watoa huduma na watumiaji wa bahari na huduma za bandari pamoja na mitambo inayohusiana na hukumu hizo."

Kifungu hiki kinanitia mashaka. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anifafanulie vizuri zaidi, ili nikielewe pindipo nitakapokuja kukaa na wananchi wangu, basi nijue vipi vya kuwafahamisha ili na wao waweze kufahamu yale makusudio yaliyokusudiwa katika Mamlaka hii ya Kusimamia Usafiri wa Baharini Zanzibar.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa niende kwenye ukurasa wa 210 kifungu kinachozungumzia uwezo wa kukopa fedha. Naomba kununukuu kifungu cha 22.

Kifungu cha 22 kinachosema hivi:-

> "Mamlaka inaweza kukopa fedha kwa idhini ya Bodi kwa njia ya mkopo au kuomba fedha benki bila ya kuwa na salio la kutosha na kwa namna ya kutoa dhamana kwa masharti yanayolingana na ulipaji wa deni la riba kwa masharti kama wizara itakavyoelekeza na Bodi kuona inafaa."

Hapa kuna *section* mbili kwa tatu, yaani kuna mamlaka, bodi na shirika. Kwa hivyo, hapa sijafahamu ipi itakuwa na nguvu pamoja na mamlaka zaidi, ninachokiona ni muingiliano. Kwa maana hiyo, ninaomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anifafanulie yenye uamuzi wa mwisho ni ipi, mamlaka, bodi ama shirika kwa ajili ya kupata kutoa ufafanuzi zaidi wa utekelezaji wa masuala kama haya ambayo yameorodheshwa humu.

Mhe. Spika, kwa wingi wa maelezo yote yaliyoelezwa kwenye waraka huu ni sahihi na yote ninayaunga mkono, ambapo tukifikia hatua hii Inshaallah masuala yetu ya kufufua uchumi pamoja na kuimarisha maendeleo kwa wananchi wetu yatafanikiwa.

Baada ya maelezo hayo na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Amani ninaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. *(Makofi).*

**Mhe. Ali Mzee Ali:** Mhe. Spika, ninashukuru kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia kidogo. Wakati tulipokuwa Pemba tulifanyiwa Semina ya *Shipping Merchant Act* ili tuipitishe ndani ya Baraza letu. Katika semina ile tulikataa na Mhe. Waziri alikuwa Mhe. Zuberi Ali Maulid.

Vile vile ninakumbuka Gazeti la Dira likatoa picha za watu wa tano wakiwemo Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Mhe. Ali Juma Shamhuna, Mhe. Ali Mzee Ali na Mhe. Hafidh Ali Tahir ndio miongoni mwa Wazanzibari waliochangia. Kwa hivyo, tulimpa muongozo Mhe. Zuberi Ali Maulid na hatimaye ikashindikana kwa yale ambayo sisi tunayoyataka katika sheria ile, ili iweze kutumika kwa Zanzibar. Kutokana na hali ile sheria ikapelekwa Bungeni bila ya sisi kukubali. Kwa hivyo, tulifuzu kutokana na msimamo wetu ule.

Baadaye mwaka 2006 ikaja Sheria ya Zanzibar *Maritime Transport Act* Nam. 6 na tuliipitisha hapa Barazani. Kwa kweli sheria ile ilipigwa mabuti mara 35, siku hiyo mimi ndiye nilikuwa Mwenyekiti wa Baraza hili. Ninakumbuka Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi Mhe. Adam Mwakanjuki alimwambia Mhe. Abubakar Khamis Bakary Wallahi, Billahi, Tallahi. Basi nilimwambia Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwamba aridhie kwa sababu ya kuambiwa masuala hayo yote na aliridhia.

Suala la mzozo lilikuwa juu ya *International Maritime Organization (IMO)* pamoja na suala la *SUMATRA*. Mhe. Spika, zilitoka *statements* hapa za kuwafukuza na baadaye tulisema sivyo. Lakini Mhe. Waziri alisema kwa vyovyote Zanzibar itakuwa *member* wa *IMO*, bado hatujawa. Isipokuwa tumeingia katika kuridhia na kuendelea mbele Kwa hivyo, sheria hii ambayo Barazani tuliipitisha kuna kifungu ndani ya sheria hii kinachomtaka waziri aweze kutunga kanuni, kifungu hicho kinachozungumzia masuala ya *administration*. Mhe. Spika, naomba kunukuu. *(Makofi)*.

> *"The Minister in addition to other powers conferred to him under this act shall be responsible for the General Administration of this act."*

*Number five:-*

> *"The Minister in exercises his power under this act shall established a Statutory Board to be known The Zanzibar Maritime Safety Administration to overseas matter on Maritime Safety Security …*"

Mhe. Spika, kipengele hiki cha sheria kinamruhusu waziri kutengeneza *Statutory Board* ndogo tu ya kusimamia. Sasa wao ndio wametengeneza sheria hii ambayo tunaijadili, lakini imekuwa pana sana. Suala langu ni kwamba sheria hii haijafutwa, isipokuwa sheria hii inafuta kifungu cha tano cha Sheria ya Usafiri wa Baharini Nam. 5 ya mwaka 2006 na kuweka kifungu kipya, ndio hii sheria yenyewe.

Sasa kama kile kinafutwa nani ata-*administer administration* ya sheria hii kama sheria yenyewe imeshafutwa na imekuja huku. Mhe. Mwanasheria Mkuu sijui yupo hapa kidogo ninaona kuna mashaka.

Wakati tunapochangia kwa kusema kama haya haina maana kuwa sisi sio upande wa serikali na wala sote ndio Rais. Isipokuwa tunachangia kwa sababu sisi ndio Wawakilishi na tunayo haki ya kuchangia na kueleza. Kwa hivyo, kusije kuwa na tafsiri za ajabu.

Mhe. Spika, sheria yote hii nzima imekuja kutokana na agizo ya sheria ile tuliyoipitisha mwaka 2006 ya *Maritime Transport Act*. Vile vile kuna Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Juu, lakini sheria ile ya inayo sheria ndogo ya mfuko. Isipokuwa sheria mama ni ile Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Juu ya Mikopo. Kwa hivyo, sheria hii kidogo sisemi kama irejeshwe lakini ina mashaka.

Kwa hivyo, haya yote yametoka kwenye agizo la sheria mama lakini hili limefutwa na wala haina *administration* na sheria hii ni kubwa sana. Mhe. Spika, hii sheria ambayo inafutwa *administration* yake ina sehemu 25, ambapo sehemu zote hizo ni muhimu kwa faida ya Zanzibar. Kwa sababu sheria hii tumeitunga sisi wenyewe kwa vishindo pamoja na ugomvi.

Mhe. Spika, sheria mama sehemu ya kwanza inazungumzia kuhusu *registration of the ship and certificate of register;* pia *restriction of training and national character of flag property*. Vile vile inazungumzia masuala ya *sea fearers, prevention of collision*. Kwa kweli mambo yanayozungumzwa ni makubwa yakiwemo ya abiria, yaani masuala 27.

Lakini tukiondoa mambo yote hayo ambayo yanataka yasimamiwe kifungu chenyewe Nam. 5 kimeondoshwa na wala hakuna chengine kilichowekwa. Kwa hivyo, sheria hii itakuwa sijui tumeipata wapi, suala hili nimeliona nilizungumzie.

Mhe. Spika, suala jengine ni kwamba Zanzibar ni nchi ambayo mazingira yake ni visiwa. Kwa hivyo, lazima meli zilikuwewepo tokea mwaka 1905 serikali imekuwa na meli mbili, na kufikia miaka ya 1948 Al-Said, Al-hadhari, Said Khalifa imekuja meli Salama. Baada ya mapinduzi tukawa na meli za MV. Mapinduzi, MV. Maendeleo na hizi Aziza ni meli za Washihiri.

Kwa maana hiyo, lazima serikali tuwe na meli zetu kwa sababu juzi tumesafirisha vikosi vyetu kwa kutumia boti ya Burak ni hatari. Zamani meli zote zikiwemo Khalifa, Al-hadhari pamoja na MV. Mapinduzi madhumuni yake ni kusafirisha watu kutoka na kwenda Unguja na Pemba kwa ajili ya kupeleka abiria na mizigo yao na biashara *by the way*.

Mhe. Spika, nimeona nichukue fursa hii kwa sababu mimi ndiye Mwenyekiti wa Shirika la Meli. Kwa maana hiyo, kuna haja ya kupata meli zetu na tu-*replace* hizi meli mbili za MV. Mapinduzi na MV. Maendeleo *(Makofi)*.

Kwa taarifa ya Baraza hili Mhe. Spika, mimi ndiye Mwenyekiti wa Shirika la Meli na Baraza hili kila miaka yote tunayozungumza masuala ya meli, mara inaambiwa na Tume inauzwa au haiuzwi. Lakini nimeingia mimi kwa msaada wa Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, tumekaa pamoja na tumekwenda serikalini na serikali tumeieleza na imekubali kuiuza meli ya MV. Mapinduzi. Waliokabidhiwa kuuza ni Wizara ya Fedha na Uchumi na wameshatoa *tender* na mpaka hivi sasa sijui matokeo yake. Lakini kwa upande wetu tumemaliza, yaani ipigwe mnada iuzwe. Isipokuwa kilichokwama hivi sasa ni kuhusu *tender* na hayo tutazungumza baadaye. *(Makofi)*.

Mhe. Spika, ninampongeza sana Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi kwa kuuleta mswada huu na kuzitoa hoja hizi. Lakini Mhe. Ali Suleiman Ali nilimwambia na ninamuunga mkono kuhusu watendaji ndio wenye matatizo. Kwa sababu Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi amewahi kuwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi Mhe. Adam Mwakanjuki, ambapo Mhe. Waziri Mwakanjuki akipata buti 60 na Mhe. Naibu wakati huo Mhe. Machano Othman Said akimsaidia na kupata buti 40. Safari hii Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi Mhe. Machano amepata buti 32, si hapa Mhe. Machano hongera *(Makofi)*.

Kwa sababu wakati ule Mhe. Ali Juma Shamhuna anazungumzia kuhusu barabara ya Donge bado hajawa waziri, Mhe. Mzee Ali Ussi pamoja na Mhe. Said Khelef Ali. Kwa maana hiyo bajeti ya mwaka huu itakuwa ni shamra shamra tu, lakini barabara nyingi zimeshatengenezwa na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi hongera sana. Safari hii bajeti utapata buti moja mbili za kawaida tu amefanya kazi kubwa.

Katika jambo hili lililozungumzwa katika kifungu kile kinachozungumzia bodi ya Wakurugenzi wa mamlaka, Mwenyekiti, Mkurugenzi Mkuu, na wajumbe wengine ambao watateuliwa na Waziri sasa umemfunga Waziri. Wanasema mtu hataweza kuteuliwa kuwa mjumbe isipokuwa awe na sifa zifuatazo:-

Awe na elimu ya Chuo kikuu kinachotambulika, sasa hapo umesema nini na kwa shahada gani, haisemi kitu, vyuo viko chungu nzima. Halafu awe na uwezo usiopungua miaka mitano katika fani ya sheria kwani mahakamani kule, mambo ya bahari ni yepi. Kuna usimamizi wa usalama, hiki ni kitu kipya, juzi

tulikuwa na sheria ya sensa, kukawa na sifa ya mjumbe wa bodi awe mahiri. Mhe. Said Ali Mbarouk akauliza nani mtu mahiri ? Lakini baada ya michango iliyokwenda, michango ya P*rofessor* Moh'd Ali (Mulla), michango ya Mhe. Haji Faki Shaali, michango ya P*rofessor* Mhe. Ali Juma Shamhuna ana M*asters,* kachukua juzi zaidi amesema hapa kwamba nitamshauri Mhe. Rais Mheshimiwa awe mjumbe wa bodi.

Jana hapa ilisemwa si muhimu ma- *degree*, ni uzoefu na umahiri, kwa hivyo Mhe. Waziri futa hii *(Kicheko).* Kwa sababu hivi ni vipengele vya watu tu vilivyokuwa havina msingi. Mimi mwaka 1996 nilichaguliwa mjumbe bodi ya bandari nilikuwa si mwakilishi, si NEC, si chochote hata uheshimiwa nilikuwa siujui hata siku niliyopigiwa simu nimeteuliwa, ulinambia mimi hapa Kificho, nikawa najiuliza Kificho ndio nani na mshamba gani ninaeletewa tena. Akaniambia mimi Spika, akaniambia umechaguliwa na Rais. Kwa hivyo kesho saa 2.00 Asubuhi ufike nikamwambia mimi niko Morogoro, akaniambia lazima ufike nikauliza nije na mke wangu nikaambiwa uje peke yako leo ni rafiki yangu.

Lakini mimi nilichaguliwa kabla mwaka 1996 lakini bodi ile Waziri alikuwa Mhe. Amani Abeid Amani Karume. Katika Baraza lako hili akamchagua Mhe. Haji Omar Kheir, huyu ninamjua zamani. Lakini kwenye bodi tulikutana bodi ya bandari ya mwanzo, juzi miaka kumi. Rais anasema anaipongeza na bodi hiyo alikuwa Mhe. Haji Omar Kheir, Hilika, Moh'd Said, Ramadhan Saleh, Moh'd Said, Dk. Bilali, Ali Mzee, Haroun Shaib na Meza tukamaliza ikaingia mwaka 2000.

Mwaka 2000 mimi bado si mwakilishi Rais akaunda bodi nyengine nikachaguliwa tena kwenye bodi ile. Akaja mtu mahiri mtaalam mwenye ujuzi, hana shahada Mhe. Hamza Hassan Juma. Tumekuwa naye kwenye bodi kama mara mbili mpaka sita, anachangia na sio mzaha. Kipindi kile tumezungumza sisi gati hii kama sio bodi ile miaka kumi iliyokaa gati isingejengwa. Tumepigania meli imegongwa tumeleta $ 1.5 milion hakuna mtu mwenye *degree,* wala nini ndio hao hao Mhe. Hamza safari ndio bodi imemaliza. Mimi kanipeleka shirika la meli kaniteua nashukuru, Mhe. Machano kaniweka shirika la meli nashukuru Mungu.

Mhe. Hamza Hassan Juma kawa Waziri hajaweza kurudi, Dk. Jidawi kawa Katibu Mkuu Mhe. Waziri kapeleka watu wazito kutoka Baraza lako, kampeleka Mhe. Haji Omar Kheri shahada yake siijui hana anakwendea bahati mpaka aache dunia rafiki yangu huyo, Ali Suleiman Ali (Shihata). Sasa hili Shirika kubwa ndio linaloongoza hakuna mradi mkubwa Unguja kuliko gati imeongozwa na hawa niliowataja sasa unaweka kitu kidogo sana kama hiki, mimi nasema hii Mhe. Waziri ondosha na uchague watu watano, sita Mhe.

Salmin Awadh kasema wapatiwe bonas kidogo wewe mwenyewe utaogolea, utie wajumbe wawili wanaotoka humu ndani na hao ndio wenzako na huyo Rais aliyekuchagua wewe kafanya hayo hayo. Kwa hivyo futa sifa hizi za watendaji si za wajumbe wa bodi, sasa watendaji hawana sifa na ukiwa unamtaka mjumbe wa bodi awe na *degree* sasa mwenyekiti awe na nini basi tuseme mwanyekiti awe na *masters* na waziri awe *degree* hapo italingana, sasa Mhe. Waziri hii kitu ondosha kabisa na wenyewe wameshasema hapa.

Mhe. Spika, haya mambo tunayozungumza haya ya masavee Mhe. Abass Juma Mhunzi amezungumza leo hapa umemsikia, amefanya *research* tangu asubuhi. Mhe. Haji Faki Shaali anaipitia sheria ile na sijui atakapoibuka itakuwaje, na hivyo ndivyo inavyotakiwa uchangie kwa sheria. Mhe. Ame Mati Wadi kila ukiwa nae anasoma kanuni au katiba kusoma si lazima *degree* ni hamu, Mhe. Ame Mati Wadi huyu anawashinda watu wengi wenye karatasi, kwa kanuni na katiba akizungumza kifungu hiki na kanuni hii. Mhe. Ame Mati na Mhe. Haji Faki Shaali wamehifadhi kanuni na katiba kama nini, lakini wanasoma, wana hamu, wanajua mimi nimeona niseme hayo.

Sasa Mhe. Spika, hii sheria ni nzuri tumsaidie tufanye marekebisho lakini wanaopasisha hizo meli anasema ile sheria inafutwa, wale waliotolewa kule wanafutwa na wanaingia huku, hawa Kwanza hawana mtu leo kasema Mhe. Abass Juma Mhunzi. Katika fani hii kuna elimu yake hayo mambo ya meli hayo, Unguja nzima hakuna mtu mwenye *first class marine engineer*, Unguja nzima Wizara ya Mawasiliano hamna. Na kuna nyengine inaitwa *first class first mariner* sasa hizi ni shahada za mambo ya kuendesha meli na usimamizi wa meli, hawa na yule *server* hana shahada kubwa sana yule anayefanya mambo hayo ana *marine logistic* inasaidia hivo hivo wanakodi watu nje hizi meli kuzipasisha.

Sheria inaruhusu kwa upande mmoja lakini kwenye kitengo chao hakuna mimi mpaka nimeingia Shirika la Meli bado sheria hii kanuni zake hazijatungwa lakini sasa hivi tayari, sijui sisi wenyewe Baraza au Mhe. Waziri wa katiba au Waziri Kiongozi sheria nyingi tunazotunga zinafungwa na vitabu, kanuni hatutungi na sheria inasimama kwa kanuni.

Mhe. Spika, Bwana Mtume Muhammad (S.A. W) ndiye aliyeanzisha nafasi za ubalozi na balozi wa kwanza wa kiislam walifanyiwa *enter view* hawajapelekwa tu Irak wakati ule sio Irak, walivyokwenda *enter view* wamekwenda pale kuna watu ukiwakuta kwenye *inter view* anakwenda, rafiki yangu hapo akusaidie pale unaona huyo kapita tu. Sasa na mtu kama Omar Maruni a!, sasa walipokwenda wale watu wa mwanzo wakaulizwa kama utachaguliwa kuwa balozi utaendeshaje mambo akasema nitatumia Qur-ani, akaambiwa kama Qur-ani haikupi ufafanuzi akasema nitatumia hadithi za

Bwana Mtume kama hazikupi akasema basi akaambiwa nenda katika wale watu watano.

Akenda mtu wa pili akaulizwa akasema nitatumia Qur-ani kama Qur-ani haikupi akasema nitatumia hadithi na watatu vile vile, na wale ndio walitegemewa kuwa watu wa juu. Sasa kuna mmoja akaingia akaulizwa unasemaje sasa mtu anaingia *enter view* Mhe. Spika, unamuuliza unasemaje akasema nimekuja *enter view* akaambiwa hata wewe.

Mhe. Spika, akaulizwa haya wewe unataka nini, akasema mimi nimesikia kuna nafasi ya ubalozi akaulizwa, sasa wewe ukichaguliwa kufanya kazi ya ubalozi utayaendeshaje mambo akasema nitatumia Qur-ani, akaambiwa kama Qur-ani haijakupa ufafanuzi akasema nitatumia hadithi akaambiwa wewe wale jamaa waliotoka uliwaona wale, akasema mimi sijawaona kwa sababu wao wametoka mlango huu na sisi tuko huku. Akaambiwa kama hiyo hadithi haijakupa akasema nitatumia akili.

Qur-ani imeundwa kwa watu wenye akili, bwana Mtume kupelekewa akasema huyu anafaa na wale waliosoma kwa hivyo elimu ni muhimu, busara ni muhimu na hekima na akili ni muhimu. Kwa hivyo narudia tena elimu ni kitu muhimu sana kwa hivyo sifa bado ni ndogo lakini hawa jamaa wa hicho kitengo kinachopasisha mimi nimeandika sasa hivi *the do the job but the are not qualified* nini maana yake. Lakini ikitokea mambo ya Mahakama na kesi kina Mhe. Abubakari wakivaa makoti yao yale yanayotisha basi ndio *the do the job but the are not qualified* wewe ni jaji Mhe. Spika, unajua.

Kwa hivyo, haya nimeona niyazungumze ili mswada huu tuweze kuupa nguvu na haya tuyarekebishe, katika sheria hii yote mambo haya yapo jadweli No. 92 kifungu cha tano ambacho nacho kimebeba hii bodi, sasa Mheshimiwa Spika, tunatakiwa hizi sheria kwa maslahi ya hali za baharini sio nzuri na kwa wizara peke yake haiwezi labda serikali isaidie, kuna mambo mengi mimi leo Meli yangu ya MV Maendeleo wakati mmoja paliulizwa maswali hapa Mhe. Waziri ikawa hajui akasema tayari ni nzima matokezeo yake leo zimeganda zote mbili zimekufa Maendeleo na Mapinduzi, sasa serikali imsaidie tupate pesa tununue meli.

Lakini sio hayo tu hii meli watu wanapanda tu inazidi inapakia inavyotaka tu ni hatari hii tunaweza kuwa tunaudhi lakini ndio ukweli ulivyo. Mhe. Salmin Awadh leo kazungumza haimo humu lakini hapa ndio pahali pake tutapenyeza *sect* ya anga tunapanda chata, alikuwa akijibu Mhe. Mwakanjuki aa sijui kitu gani. Ndege inapakia na inakwenda na *pilot* mmoja tu kila siku Pemba na Zanzibar sio salama ile, lakini tunangojea mpaka siku *pilot* asinzie au apate maradhi sasa sijui itakuwaje ikiwa yuko mbele Mhe. Hamza anaweza kuitua

hivyo hivyo, lakini mtu kama Bimkongwe yeye mambo ya ndege hajui wala meli sasa akijaalia akiwa pale ni hatari, hili limesemwa tokea zamani humu ndani.

Mhe. Machano Othman Said mambo haya yako chini yako hili suala wala usisikilize hadithi. Hawa wawe wawili, jamani sio gari ile, tuliambiwa gari. Kapakiwa mtu mbele hajapanda gari maisha yake, yule anatia gia kasimamisha gari njiani, kwenda chooni anarudi hamna gia, sasa yule mtu anamwambia nimeitoa kwa nini. Kwa sababu naona unapata tabu , yeye kaitoa kaitupilia mbali iende hivyo hivyo, sasa usiku gari haitembei tunacheka lakini mimi nasema ndani ya kalbi yangu lolote nililosema la meli na ndege ndani ya moyo wangu ni hatari na sisi ndio watu wazima, sisi ni wawakilishi hili jambo lina hatari.

Lakini nitakuja kusema kwamba nilisema, Mhe. Salmin Awadh kasema, na wengine wameshasema, mimi huu mswada nauunga mkono mia kwa mia niliona hayo niseme kama mtu mzima kama kiongozi na nataka kumwambia Mhe. Waziri Machano wewe umebahatika, umeteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, Waziri wa Mawasilano. Safari hii sherehe ya Mapinduzi imependeza sana yanafunguliwa mabarabara, gati mpaka tukasema mbona hamumtaji Mwakanjuki, umeshapiga matai yako Mwenyezi Mungu akulinde na jicho la hasidi na jicho la maadui uendelee Baraza la Wawakilishi ndio wenzako utakapounda bodi zako sawa sawa.

Nakushukuru sana Mhe. Spika, mimi nimeshamaliza. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora:** Ahsante Mhe. Spika, nami napenda kuchukua nafasi hii kutoa mchango wangu kidogo tu katika Mswada huu wa kuanzisha Mamlaka ya kusimamia Usafiri wa Baharini Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, mswada huu kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa wakati huu kuamua kuuleta kwenye Baraza baada ya kupitisha ile sheria ya *maritime law* ambayo kusema kweli ni wakati wake sasa hivi, mimi ninachotaka kuzungumza. Katika suala hili ni hii sheria yenyewe na nguvu zake na sura yake ilivyo namna nilivyoisoma na kuitizama na kuifahamu, naanza kuizungumza sheria hii kwenye kifungu cha 4.

Kifungu cha 4 kinazungumzia mamlaka itatekeleza majukumu yake, yaani eneo la udhibiti la mamlaka. Katika kifungu hiki ukisoma eneo la udhibiti wa mamlaka utakuta kwamba mamlaka hii inayoundwa, kwanza kuna kifungu kinachoshughulikia usalama wa vyombo vya wavuvi baharini. Pia kuna kifungu kinachozungumzia kudhibiti, ulinzi wa bandari, kwa mujibu wa

kanuni na masharti ya usalama kitaifa. Vile vile kuna kifungu kinachozungumzia udhibiti usalama wakati wa utoaji wa huduma za bandari.

Mhe. Spika, nikiendelea kusoma mswada huu kuna majukumu ya mamlaka ambayo nayo yameorodheshwa, nikiyasoma machache ni kwamba kuna jukumu (a) katika kifungu cha tano kinasema.

"*Kifungu cha 5 (a) Kwa ujumla kusimamia utekelezaji wa sheria ya usafiri baharini Na. 5 ya mwaka 2006".*

Kuna kifungu (h) kinasema.

"Kifungu (h) kukagua na kuzuia meli ambazo zitaonekana ni salama au si salama"

Kifungu (j) nacho kinasema.

"Kuthibitisha michoro ya Meli zinazoundwa tena na kuweka kumbukumbu za kiufundi wa meli".

Kuna kifungu (l) kinasema.

*"Kutoa vitambulisho vya mabaharia na kitabu cha kumbukumbu za mabaharia, kuthibitisha vifaa vya usalama na kutoa huduma za upasishaji, kuratibu kazi za taasisi za ukaguzi".*

Hayo yametajwa kama ni majukumu ya mamlaka hii, yamendelea yamefika mpaka kwenye kifungu cha (aa) kinasema.

Kifungu (aa) kinasema.

"Kutekeleza majukumu yake kulingana na wajibu wa Serikali".

Halafu kuna uwezo wa Mamlaka Mhe. Spika, nao umetajwa kuweka viwango vya usalama na kanuni na kufutwa kwa watoa huduma na watunzi wa baharini, huduma za bandari pamoja na mitambo inayohusiana na huduma hizo. Kwa ujumla kusimamia mambo yote ya usalama wa meli na usalama baharini.

Kifungu cha 6 (h) Kinasema.

"Kudhibiti mabaharia na kuweka kanuni za ustawi wa mabaharia".

Mhe. Spika, ukienda kwenye kifungu cha 9 kinazungumza Waziri anaweza.

"Kutoa maelekezo ya jumla kwa Bodi yanayohusiana na shughuli zake kwa mamlaka".

Pamoja na mengineyo, mpaka tunafika kifungu (a) sasa ninachotaka kukisema hili jukumu la kushughulikia lililotajwa katika kifungu cha 52(1) limechukuliwa kwa sehemu kubwa kabisa, yaani kifungu cha 5 cha Sheria ile ya baharini ya mwaka 2006 yameingizwa katika Sheria hii karibu yote. Nadhani hapa ndipo ilipoonekana dhamiri ya kwamba si vizuri kuwa huku Bodi ya Mamlaka tunaipa uwezo wa kufanya kazi hizi zote halafu bodi hii hii, tunamwachia tena Waziri katika sheria ile ya zamani suala la kutunga ile mamlaka ya baharini. Nadhani hili ndilo walilolizingatia wanasheria wetu na wakaona kweli kifungu kile ipo haja ya kufutwa, kwa sababu kazi zote za administration ya bahari zimeshatajwa katika sheria hii na uwezo wa waziri pia umeshatajwa. Ndio ilipokuja suala la sheria Na. 5 ya kifungu cha baharini ya mwaka 2006 ifutwe ndio maana yake iliyokuwa hapa.

Sasa nini mwenyewe atakifanya nafikiri mwenyewe Waziri atakaposimama atakuja kutueleza niliona nilizungumza hili, kwa sababu ile sheria ya Bahari ni kwamba itakuwa inaning'inia. Hii hapana uwezo wake mkubwa itakuwa umeingia katika sheria hii, ndio maana utakuta kuna *authority* mbili zinafanya kazi ya namna moja.

Mhe. Spika, huo ulikuwa ni mchango wangu mfupi tu mwenyewe, Waziri atakapokuja ku- *wind up* atatengeza mengine zaidi. Ahsante sana.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuhudhuria kikao hiki jioni hii. Baada ya hapo, nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii na mimi kutoa maelezo mafupi na baadhi ya ufafanuzi kwa maneno machache ya wajumbe, pia kuunga mkono hoja hii ya mswada wetu.

Mhe. Spika, mchangiaji wa mwanzo ni Mhe. Mwenyekiti, na baadaye Waziri Kivuli, baada ya hapo alifuata Mhe. Abubakar Khamis Bakary, mategemeo yangu ni kwamba wale wote waliochangia mswada huu walikuwa na azma moja tu ni kuchangia mswada na kuboresha pale panapoonekana pana matatizo. Lakini baadaye uweze kupitishwa baada ya kutiwa saini na Mhe. Rais kuwa sheria.
Kwa sababu Waheshimiwa Wajumbe karibu wote wamekuwa wakituhimiza sana kuwepo kwa mswada huu, basi tegemeo letu ni kwamba wataunga mkono ili uweze kufanya kazi zake sawa sawa.

Mhe. Spika, mimi nitazungumzia kiujumla jumla katika baadhi ya maelezo ambayo yametolewa, kwanza nianze na kumshukuru Mhe. Ali Mzee Ali ambaye amezungumza jioni hii. Ametoa ufafanuzi wa mambo mbali mbali, lakini na mimi pia nataka niseme kwamba huo ndio utaratibu halisi. Pengine karibu serikali nyingi duniani, kwamba shughuli zote zinazohusu mambo ya utendaji basi zinahitaji kupata wataalam wa kutosha kwa sababu zinahitaji mambo mengi ya *technical*. Lakini zile shughuli ambazo za kisiasa basi huwa zinahitaji watu ambao ni wanasiasa wenyewe pamoja na elimu ya kuweza kuendesha jambo hilo. Lakini hailazimishwi sana kuwa na elimu ya kutosha kwa sababu yeye pale ni msimamizi na mwanasiasa ambaye anatakiwa kutekeleza ilani ya chama chake kinachoongoza nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba nimpongeze Mhe. Ali Mzee na naungana na yeye kwa hilo, lakini vile vile niungane naye mkono kwa yale masharti ambayo na sio yeye tu na wale wote walioleza kwamba lile eneo linaloonekana kwamba lina masharti mazito ya wajumbe, kwenye bodi basi tutaangalia uwezekano wa kuchanganya watu wenye elimu ya juu kwa ajili ya kupata ufanisi zaidi. Lakini na wale ambao watakuwa na elimu ambazo zitasaidia na maarifa mazuri basi nao vile vile kama walivyotoa ushauri wizara italichukua hilo na kulifanyia kazi.

Mhe. Spika, jengine ambalo limezungumzwa katika Mswada huu Mhe. Ame Mati asubuhi alizungumzia suala la kuhusu minara na akasema kwamba minara haifanyi kazi. Ni kweli kulikuwa na baadhi ya minara ilikuwa ina matatizo lakini hivi sasa minara karibu mingi inafanya kazi vizuri na imefanyiwa ukarabati wa kutosha na inafanya kazi. Kwa kujua hilo kwamba wizara yetu kwa kupitia Shirika la Bandari imeweka mkazo madhubuti wa kuona kwamba zinawekwa taa zile sola badala ya kutumia zile taa za zamani.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningelizungumza katika Mswada huu ni kuhusu usajili pengine uwezekano wa kwamba je, sisi Zanzibar tunaweza kusajili wakati kuna muelekeo kuonekana labda sheria hii pengine ingezidi kuwa na nguvu zaidi kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Spika, kabla ya Mswada huu kuletwa mbele yetu tayari tumekuwa tukifanya kazi pamoja na wenzetu wa Jamhuri ya Muungano na wao ndio ambao tumeshirikiana nao moja kwa moja kuweza kwenda nje kwa ajili ya kupata ile ithibiti ya kuwa na ruhusa ya kuanzisha hichi chombo. Kwa hivyo hatukuanza tu kwa kukurupuka lakini tulikuwa na mawasiliano ya kutosha kuona kwamba kile tunachokifanya kitakuwa na nguvu ya kisheria.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kulizungumza kuhusu lile tatizo ambalo limezungumzwa na wengi kuhusu meli zetu na uwiyano wa abiria

wanaochukuliwa. Mhe. Spika, ni kwamba wizara yangu kupitia kitengo hiki imekuwa ikifanya mazungumzo ya mara kwa mara na wenye meli na pale ambapo linapotokea kosa linafanywa na hawa wenye meli basi juhudi zinachukuliwa kwa kupewa adhabu ikiwa na faini. Tumewaza kutoza faini mara kadhaa kwa wahusika kutokana na vitendo ambavyo vinakiuka maagizo ambayo yanatolewa na wizara yetu kwa kupitia usajili wa meli. Sio kama wengine wanavyosema wengine kuona kwamba labda tumekaa na hatuna chochote ambacho tunakifanya kuona kwamba tunadhibiti uingiaji wa watu katika meli.

Mhe. Spika, suala la kusajili vyombo kuna wengine waliuliza kuna vyombo vyengine visivyo rasmin. Vyombo vilivyokusudiwa kwamba visivyo rasmi ni vile vinavyoundwa kwa kutumia vyuma pamoja na mabati lakini pia kuna vyombo ambavyo tunavitengeneza sisi wenyewe kama majahazi na mashua hivi ndio vyombo tunavyoviita sio rasmin, pamoja na kwamba tunavitumia.

Mhe. Spika, tulizungumzia suala zima la kuweka uwezekano wa kwamba tungeweza kuweka maeneo ambayo ya bandari zetu kuweza kufanya usajili wa vyombo mbali kwa mfano majahazi na vyombo vyengine ambavyo vinahitaji usajili. Wizara yangu ina mpango wa kuweka maafisa katika maeneo ya bandari hizo. Matarajio yetu ni kuona kwamba kwa yale mambo madogo madogo yakamaliziwe katika sehemu hizo na yale ambayo yatahitajika lazima kufika Makao Makuu basi yatashughulikiwa Makao Makuu moja kwa moja.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningetaka nilizungumze, Mhe. Abassi Juma Muhunzi na yeye alichangia na napenda nimshukuru pamoja na kwamba alikubaliana na mawazo ya Mhe. Abubakary kwamba sheria hii irejeshwe, lakini alitoa mchango mkubwa juu ya yale mambo ambayo yangehitajika kufanywa na wizara yangu kabla ya hatua hizo kuanza. Maelezo yake yote tumeyachukua lakini lile jambo ambalo lenye utata tutakaa pamoja na wenzetu Wanasheria kupitia Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuweza kuona kwamba hili jambo linapatiwa muafaka.

Mhe. Spika, nilisema kwamba nitatoa ufafanuzi zaidi kwa yale mambo ya jumla, basi ningependa niishie hapo. Mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wa Jimbo langu la Chaani tunauunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja na ningeomba wale wote watakaochangia wakosoe pale ambapo panapohitajika kukosolewa na wachangie lakini baadaye wauunge mkono ili tuweze kutekeleza sheria hii kama tulivyokusudia. Mhe. Spika, ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe mmechangia vipengele vinavyohusu sheria, Waziri tumekubaliana kwamba akafanye, kazi ili baadaye aje afafanue vizuri zaidi kesho.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi kwa kuwa Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi anahitaji kupata muda wa kuweza kujitayarisha ili kesho aje atoe majumuisho. Kwa hivyo naomba kutoa hoja kwamba uliahirishe Baraza lako tukufu hadi kesho tarehe 28 siku ya Jumatano saa 3:00 asubuhi. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Saa 12:37 jioni Baraza liliahirishwa hadi28/01/2009 saa 3:00 asubuhi)*